

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 20 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninayo Taarifa ya Mheshimiwa Spika ambayo inatolewa chini ya Kanuni 39(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Pili wa Bunge, Bunge lilipitisha Muswada mmoja wa sheria wa Serikali ambao ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2021*].

Kwa Taarifa hii, Mheshimiwa Spika anapenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Muswada huo umekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria ya nchi inayoitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 1 of 2021*].

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali na tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 104

Vijana wa Tanzania Kupewa Stadi Mbalimbali

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI aliuliza:-

Je, ni lini vijana wa Tanzania watapewa stadi mbalimbali za kuwaongezea ujuzi wa maarifa kuititia Mfuko wa Uwekezaji wa Wananchi Kiuchumi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, Tanzania Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia vijana ujuzi wa stadi za kazi na maarifa kama hatua mojawapo ya kuwawezesha vijana kumudu ushindani katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi, Serikali kuititia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi imetoa stadi mbalimbali za kazi kuongeza ujuzi kwa vijana kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya vijana 5,538 wamepatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi (*Apprenticeship*) katika

fani za ufundi stadi katika nyanja mbalimbali kupitia Taasisi ya Don Bosco na Vyuo vilivyoko chini ya *VETA*;

(ii) Serikali imeingia mikataba na *VETA* kwa kushirikisha ujuzi kwa vijana katika Mikoa yote nchini katika fani za ufundi wa magari, useremala, uashi, upishi, huduma za vyakula na vinywaji, ufundi umeme, uchomeleaji vyuma, ufundi bomba, uchongaji wa vipuri na ushonaji wa nguo. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 kufikia Februari, 2021 jumla ya vijana 10,178 walikuwa wamerasimishwa na katи ya hao vijana 28 ni watu wenye ulemavu; na

(iii) Vijana wanaohitimu elimu ya juu wanaendelea kupata mafunzo ya uzoefu kazini ambapo Serikaliimeendelea na zoezi la kuwashikiza wahitimu kwa waajiri. Kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Februari, 2021, wahitimu 1,203 wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati wamekamilisha mafunzo ya uzoefu kazini kupitia viwanda, taasisi na makampuni mbalimbali ya sekta binafsi na umma nchini. Wahitimu 2,037 wanaendelea kupata ujuzi na uzoefu katika taasisi mbalimbali ambazo ni za binafsi na za umma na katи yao, wahitimu 92 ni watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, programu zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinashauriwa kuhakikisha zinawajengea wadau wake stadi za ujuzi mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya programu husika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Latifa Juwakali, swalı la nyongeza.

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini ninaa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la kwanza, katи ya hao vijana 5,538 ambao wamepatiwa ufundi au mafunzo stadi ni wanufaika wangapi wanatoka Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, baada ya mafunzo hayo, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwatafutia miradi ama fursa mbalimbali ili waweze kujajiri na kuajirika? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza linataka takwimu na kwa hivyo mimi nitakupa muda umtafutie takwimu Mheshimiwa halafu umkabidhi, jibu swali la pili.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuhusu swali la kwanza, nikubaliane nawe lakini pia mbali na takwimu suala hili limekuwa likifanywa na Wizara ya Michezo, Vijana na Utamaduni kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, tutapata takwimu hizo na tutaziwakilisha kwa sababu suala hili kwa upande wa Bara na Zanzibar kuna *parallel program* lakini zaidi tunashirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili, ni kweli kwamba vijana hawa wanapomaliza kupewa mafunzo na stadi za kazi wanazopewa, Serikali imeweka mpango katika mifumo miwili.

Kwanza, kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo vijana hawa baada ya kupewa stadi hizi za kazi wanaweza kuwezeshwa katika hatua ya pili baada ya kuwa wamebuni miradi ambayo ni endelevu na ambayo inaweza ikawasaidia vijana kuweza kujikimu katika maisha yao lakini pia kuweza kufanya biashara au kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye sekta za kilimo. Kwa mfano, kwa kipindi cha mwaka wa jana katika halmashauri 84 yalitolewa mafunzo na kampuni tatu hizi hizi za vijana waliopata mafunzo na wakapewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kutengeneza vitalunyumba ambapo zoezi hilo limefanyika katika halmashauri 84. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili fedha hizi za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwenye halmashauri kwa maelekezo hayo hayo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri

wetu wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama wamekuwa wakisimamia ambapo fedha zimekuwa zikitolewa na halmashauri kuititia 4:4:2 kwa maana ya asilimia 4 kwa wanawake, asilimia 4 kwa vijana na asilimia 2 kwa watu wenye ulemavu katika halmashauri zote. Fedha hizi zinakusudia kuwapa vijana mikopo au fursa ya kuweza kuijendeleza katika maeneo ambayo watakuwa wameendelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo katika eneo hilo hilo ni agizo la Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mpango ambaa umewekwa kwamba katika Halmashauri zote yametengwa maeneo ya vijana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watakapotaka kujingiza kwenye kilimo au fursa zozote wanaweza wakapewa. Mathalani ukiangalia Kahama kuna eneo la Zongomela ambapo vijana waliopata mafunzo ya ufundi stadi wameweza kupata eneo ille na wanatengeneza samani mbalimbali ikiwemo *grill*, vitanda lakini pia wanauzu mbao. Ukienda eneo la Mvomero vilevile kuna *garage* ziko pale zimetengenezwa hata maeneo ya Misungwi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kifupi tu nimwambie kwamba vijana hawa wanapopata stadi hizi za kazi bado hawaachwi hivi hivi tunaendelea tena kuwalea ili kuhakikisha kwamba zile stadi na *skills* walizopata zinawasaidia katika kujikwamua kwenye maisha yao. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, sasa aulize swalii lake.

Na. 105

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA aliuliza:-

Serikali ilitoa shilingi 500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo, lakini kiasi cha shilingi 204,000,000 kilirejeshwa baada ya kufunga mwaka Julai, 2020.

(a) Je, ni lini fedha hizo zitarejeshwa ili ujenzi uendelee?

(b) Gharama ya ujenzi ni shilingi 1,500,000,000; je, ni lini kiasi cha shilingi 1,000,000,000 kitatolewa ili kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilipatiwa shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Halmashauri ambapo majengo yaliyojengwa ni Jengo la Wagonjwa wa Nje na Maabara na majengo yote mawili yamefikia asilimia 80 ya ukamilishaji. Aidha, katika fedha hizo zilizotolewa shilingi milioni 204 zilirejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kuvuka mwaka wa fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya fedha ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016.

(b) Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2021 Serikali imetoa shilingi bilioni 1 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ili kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Majengo yatakayo jengwa ni Jengo la Utawala na Jengo la Wazazi ambayo yamefikia asilimia 40 ya ukamilishaji, Jengo la kuhifadhi dawa na Jengo la kufulia ambayo yamefikia asilimia 60 ya ukamilishaji. Aidha, katika

mwaka wa fedha 2021/2022 Hospitali hiyo imetengewa shilingi milioni 300.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, swalii la nyongeza.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na pesa ambayo tumeipata hiyo shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa sababu majengo yanaelekeea kukamilika na tumefikia mwisho sasa, ni nini mpango wa Serikali kutupatia vifaatiba ili majengo haya angalau yaweze kuanza kufanya kazi haraka iwezekanavyo kwenye robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2021/2022?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa sababu hospitali hii bado ni sehemu ya kwanza itakuwa haiwezi kulaza wagonjwa, ni nini mpango wa Serikali kwenye kutupatia *ambulance* mpya na ya kisasa ili angalau wagonjwa wale ambao hawataweza kupata huduma kwenye Hospitali ya Wilaya waweze kukimbizwa na kupatiwa huduma sehemu nyingine kipindi tunaendelea na kukamilisha ujenzi wa awamu ya pili? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba majengo haya ya Hospitali ya Halmashauri ya Biharamulo yako katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Katika mpango wa bajeti wa mwaka 2021/2022, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya

kwenda kununua vifaatiba kwa ajili ya hospitali hizi mpya ambazo zinaendelea na ujenzi. Kati ya hospitali hizo, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ni moja ya hospitali ambazo zitatengewa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili tunahitaji kuwa na magari ya wagonjwa katika hospitali zetu za halmashauri na mipango ya Serikali inaendelea kufanyika ili kuona namna ambavyo tunaweza tukapata magari hayo na kuyafikisha katika halmashauri hizi. Kwa hivyo, Hospitali ya Halmashauri ya Biharamulo ni moja ya hospitali ambazo zitawekewa mpango wa kupata gari la wagonjwa ili tuweze kuboresha zaidi huduma za afya katika eneo hilo.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, swali lake linaulizwa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 106

Hitaji la Chuo Cha VETA Mbulu Vijijini

MHE. FLATEI G. MASSAY aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha *VETA* katika Jimbo la Mbulu Vijijini ili vijana wapate ujuzi?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA aliujibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi ikiwa na lengo la

kuwa na Chuo cha Ufundı Stadi katika kila mkoa na wilaya. Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitenga jumla ya shilingi bilioni 48.6 kwa ajili ya kujenga vyuo 29 vya VETA katika ngazi ya Wilaya ambavyo kwa sasa vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mbulu kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango ambacho pia hutoa mafunzo ya ufundi stadi. Chuo hiki kinaendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu utakaogharimu jumla ya shilingi milioni 605.2 ambao unatarajiwा kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea na juhudı za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA wilayani humo, nashauri wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini kuendelea kutumia vyuo vilivyopo maeneo yote nchini, ikiwa ni pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi - Tango na Chuo cha VETA Manyara. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swalı la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, kutoka Mbulu Vijijini sehemu ya Haydom kwenye Mbulu Mjini ni kilometra 90 na kwenda Babati ni zaidi ya kilometra 130. Kwa majibu yake haoni kwamba atakuwa amewaondolea fursa vijana wa Mbulu Vijijini kupata uzoefu na ufundi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili, kwa kuwa Mbulu Vijijini hatuna kabisa chuo, je, yuko tayari kutenga fedha sasa ili bajeti ijayo tuweze kupata chuo katika Jimbo la Mbulu Vijijini? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kapinga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kutoka Mbulu Mjini mpaka Mbulu Vijijini ni kilometra 90 lakini kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba Serikali inafanya juhudui mbalimbali za kutafuta fedha ili kuendelea na mpango wake wa ujenzi wa vyuo hivi vya VETA katika kila wilaya na mkoa.

Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itakapopata tu fedha tutahakikisha kwamba maeneo yote ikiwemo na Mbulu Vijijini yatajengewa vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa naomba kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa tuna vyuo vingi ambavyo viko katika Wilaya ile ya Mbulu kiumla. Tuna Vyuo vya Ufundji Stadi Mbulu, Haydom, Masieda, Jiendeze, *Integrity* na St. Jude Yuda Thadei. Vyuo hivi vyote vinaweza kutumika kwa ajili ya vijana wetu kupata uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, vyuo nilivyovitaja mwanzo vile vya Manyara vina nafasi ya wanafunzi kulala pale pale chuoni. Kwa hiyo, wanafunzi wetu hawa wanaotoka mbali wanaweza kupata fursa ya kupata ujuzi wao pale na kuondoa usumbufu huu wa kutembea au kwenda umbali mrefu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, swalii la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na shukrani nyingi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kufahamu juu ya Chuo cha VETA ambacho kimejengwa Wilayani Nyasa. Nafahamu kimeshafikia zaidi ya asilimia 95, ni nini mpango wa Serikali kuanza kutoa mafunzo ili vijana waweze kunufaika na chuo hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tunafahamu kwamba vyuo hivi ambavyo tayari ujenzi wake umekamilika, tuko katika mpango wa kuanza kutoa mafunzo mara moja. Suala lilloluweko mbele yetu sasa ni kuhakikisha kwamba tuna vifaa kwa ajili ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuko kwenye mchakato wa manunuzi ya vifaa hivyo na pindi tu manunuzi hayo yatakapokamilika, *program* zile za ufundishaji katika maeneo haya zitaanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, sasa aulize swalii lake.

Na. 107

Kupeleka Maji ya Mto Ruvuma Mtwara

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ya Mto Ruvuma kwa Wananchi wa Mtwara ili kuondoa shida ya maji iliyodumu kwa muda mrefu?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma ni mionganini mwa miradi mikubwa ya kimkakati ambapo Serikali inatarajia kuanza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2021/2022 kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika kuhakikisha wananchi wa Mtwara wanaendelea kupata huduma ya majisafi na salama, wakati ukisubiriwa utekelezaji wa mradi huo mkubwa wa kutoa maji Mto Ruvuma, Serikali imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali za kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Mtwara Mjini ikiwemo uchimbaji wa visima vinne, ufungaji wa pampu tatu, ujenzi wa matanki matatu, ulazaji wa bomba kuu kilomita saba na bomba la usambazaji maji kilometra 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vijijini, Serikali kuitia *RUWASA* inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji 81. Miradi hii itakapokamiliika itahudumia vijiji 285 ambapo jumla ya vituo vya kuchotea maji 1,562 vitajengwa/ kuboreshwa na inakadiriwa kunufaisha wananchi zaidi ya 454,375, hivyo, kuboresha utoaji wa huduma ya maji na kufikia wastani wa asilimia 79.91 kutoka asilimia 64 za sasa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali langu la kwanza: Serikali ilianza mpango wa kulipa fidia kwa wananchi wa Mtwara Vijijini waliopitiwa na bomba la maji kutoka Mto Ruvuma mwaka 2015. Nataka kujua, mradi huu umekwama wapi ikiwa tayari wananchi walishaanza kufanyiwa uthamini ili mradi huo uanze? (*Makof*)

Swali la pili: Fedha zilizotengwa ili kutekeleza mradi wa maji wa Mto Ruvuma ambapo wananchi walishaanza kupewa utaratibu wa malipo ya fidia mwaka 2015 zimeenda wapi? Serikali inawaambia nini wananchi wa Mtwara Vijijini kuhusu mradi huo? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli fidia hii ilianza kutekelezwa mwaka 2015. Mradi huu wa Mto Ruvuma ni ile miradi mikubwa ambayo mkakati wake lazima uwe madhubuti ili mradi usiishie njani. Hivyo fidia namna ambavyo baadhi wameshalipwa, wale ambaao bado hawajalipwa nao wanakuja kukamilishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, kufikia mwaka ujao wa fedha 2021/2022 tumeweka mikakati ya kuona kwamba, tunakuja sasa kukamilisha miradi ya maziwa makuu ikiwepo mradi wa Mto Ruvuma pamoja na miradi mingine. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Francis Komba Ndulane, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Kilwa kuna changamoto inayofanana na Wilaya ya Mtwara katika huduma hii ya maji:-

Je, Serikali ni lini itatekeleza mradi wa maji kutoka Mto Rufiji ili kuwaondolea changamoto ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Kilwa? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali ina mipango mikakati ya kuona kwamba Mto Rufiji iwe ni sehemu ya miradi mikubwa ya kutoka maziwa makuu na mito, kuona kwamba maji yale sasa yanakwenda kunufaisha wananchi. Hivyo, kwa watu wa Kilwa pia tunaendelea kuwasihii waendelee kutuvumilia kidogo, huenda mwaka 2021/2022 kadiri tutakavyokuwa tunapata fedha, watu wa Kilwa pia watapata maji kupitia Mto Rufiji. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, sasa auliuze swali lake.

Na. 108

Hitaji la Maji Kijiji cha Matandara – Nsimbo

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kijiji cha Matandarani Kata ya Sitalike?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Engineer Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa Magula ambao unahuisha ulazaji wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilomita 14.9, ujenzi wa tanki la ujazo wa lita 200,000 na nyumba ya mtambo wa kusukuma maji. Ujenzi wa mradi umeanza mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2021 kwa gharama ya shilingi milioni 545.62. Mradi huo utanufaisha jumla ya vijiji vitatu ambavyo ni Mtisi (Magula), Matandarani na Ibindi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, swali la nyongeza.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi tena niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Kijiji cha Matandarani hakina kabisa hata kisima kimoja na wananchi wanakunywa maji machafu siku zote; na kwa kuwa, mradi huu mpaka sasa hivi una asilimia 10 tu na mradi huu ni wa muda mrefu ambapo wananchi

wanauona, lakini juhudhi ambazo zinatakiwa zifanyike hazipo:
Je, lini mradi huu utakwisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, vijiji vyote ambavyo amevitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli havina maji kabisa: Mtisi hakuna maji kabisa, ukienda Kijiji kinachofuata cha Magula hawana maji kabisa; na huu mradi mmesema unaenda mpaka Ibindi, kata jirani, nako hakuna maji kabisa: Je, Serikali ina mkakati gani kupitia hii miradi na kuhakikisha inakwisha kwa haraka kwa sababu, wananchi wanapata taabu sana? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, amekuwa mfuatilaji wa karibu sana katika suala hili la tatizo la maji katika maeneo haya ya Vijiji vya Matandarani, Ibindi, Mtisi na Magula.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kupitia jitihada zake, mimi binafsi kama Naibu Waziri ninakuhakikishia mara baada ya hili Bunge tutakwenda pamoja mpaka kwenye mradi huu. Usanifu wa mradi huu unatuonesha utakamilika mwezi Septemba. Hata hivyo, tutajitahidi kwa hali na mali tufanye kazi hii usiku na mchana na kurejesha muda nyuma ili mradi huu sasa usiishe Septemba, basi tujitahidi hata ikiwezekana uishe kabla ya usanifu muda unavyoonekana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makate, sasa aulize swalii lake.

Na. 109

Mkakati wa Kutangaza Hifadhi ya Taifa Kitulo

MHE. FESTO R. SANGA aliuliza:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ili ifahamike kwa Watalii wa ndani na nje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ilianzishwa kwa *GN* Na. 279 ya mwaka 2005. Hifadhi hii ina sifa ya kipekee kwa kuwa na Jamii mbalimbali za maua na kwa nyakati tofauti Serikali imeendelea kuitangaza hifadhi hii na nyingine zilizopo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati iliyopo kwa sasa ni kuendelea kuzitangaza hifadhi zote za Taifa ndani na nje ya nchi ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Kitulo. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuzitangaza Hifadhi za Taifa kupitia tovuti na mitandao ya Kijamii (*Instagram, Facebook* na *Twitter*) pamoja na kuandaa video na filamu mbalimbali na vilevile kuna kuimarisha miundombinu ya barabara ndani ya hifadhi ili kurahisisha kufikika kwa maeneo ya vivutio ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine ni kuzitangaza hifadhi hizi kupitia chaneli maalum ya “*Tanzania Safari Channel*”; vile vite kuandaa safari za mafunzo kwa wanahabari, mawakala na wadau mbalimbali wa utalii kwa lengo la kuwapa fursa ya kuvielewa vivutio vya utalii na kuvitangaza ndani na nje ya nchi; kujenga sehemu ya malazi ya bei nafuu kwa ajili ya wageni wa ndani na nje ya nchi; na mkakati mwingine ni kuvutia wawekezaji kujenga kambi za watalii au *lodge* zenye hadhi za Kimataifa, ambapo maeneo manne ya uwekezaji yamebainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa maeneo ya uhifadhi, bajeti ya mwaka 2021/2022 pamoja na masuala mengine, imezingatia uimarishaji wa utangazaji wa utalii na kuboresha miundombinu ikiwemo barabara, viwanja vyta ndege na maeneo ya malazi ya wageni ili kuvutia watalii kutembelea maeneo hayo kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Festo Richard Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza: kwenye Hifadhi ya Kitulo kwa sababu ni hifadhi yenye upekee na hifadhi nyingine za Tanzania: Je, Serikali haioni haja kuwavutia zaidi wawekezaji kwa kupunguza gharama za uwekezaji; kwa sababu, gharama zimekuwa ni kubwa? Kwa maana, ukiangalia kuna wanamakete na Watanzania ambao wako tayari kuwekeza kwenye hifadhi hizi, lakini gharama kwa mfano za *environmental assessment* tu ni zaidi ya shilingi milioni 50, kitu ambacho kimekuwa kiki-*discourage* wawekezaji.

Sasa je, Serikali umuhimu wa kupunguza gharama ili wawekezaji wawe wengi kwenye hifadhi zetu na ziweze kutangazwa?

Swali la pili: Hifadhi ya Kitulo inaenda kupitiwa na barabara ya kiwango cha lami inayotoka Isyonje kwenda Kitulo kupitia Makete, lakini bado miundombinu ya ndani ya hifadhi siyo mizuri kwa maana ya barabara: Ni mpango upi wa Serikali kupitia Wizara ya Maliasili kuhakikisha kwamba miundombinu ndani ya Hifadhi ya Kitulo inaimarishwa ili tuweze kuvutia wawekezaji wengi zaidi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Sanga kwa kuwa na jitihada nyingi sana za kuhakikisha kwamba hifadhi yetu ya Taifa ya Kitulo inapaishwa vizuri, hasa kiuwekezaji, lakini pia kwenye maeneo ya utalii. Napenda nimweleweshe Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Wizara ya Maliasili na Utalii hatuna gharama yoyote inayohusiana na uwekezaji. Wawekezaji wa aina mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wanaalikwa kwenye maeneo yote ya uhifadhi kuja kuwekeza uwekezaji mbalimbali, ikiwemo ujenzi wa hoteli, *ma-tent, camps, hostels* mpaka na *lodge*. Sisi tunawaalika wawekezaji wote bila kubagua. Gharama kama gharama ni taratibu za uwekezaji ambazo haziko kwenye Wizara yetu, isipokuwa mwekezaji yejote anatakiwa kufuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa miundombinu Serikali imejipanga kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kuhakikisha kwamba maeneo yote ya uhifadhi yanatengewa fedha ya kutosha kuhakikisha miundombinu yote ndani ya hifadhi inaimarika vizuri ili kwenye upande wa utalii sasa tuweze kuhamasisha utalii na maeneo yale yaweze kupitika kwa urahisi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni hitaji la wananchi wa Kitulo la kuitangaza hifadhi hiyo kama kivutio ambacho kiko nchini kwetu; na kwa kuwa, hitaji hilo linafanana sana na hitaji la wananchi wa Katavi la kuitangaza *Katavi National Park* ambayo ina vivutio vingi sana vya asili vya utofauti akiwepo twiga mweupe anayepatikana kipekee sana katika Mkoa wetu wa Katavi:-

Je, Serikali ina mikakati gani mipya ya kuitangaza hifadhi hiyo ili weze kufahamika ndani na nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu kwa kifupi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali ina mpango wa kuipaisha hifadhi ya Katavi kwa kuzingatia bajeti iliyopo kwenye mwaka wa fedha wa 2021/2022. Eneo hili ni eneo zuri sana kwenye upande wa utalii.

Mheshimuwa Naibu Spika, hivyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Martha kwamba Serikali inatambua mchango wa Hifadhi ya Katavi na kwamba ni eneo zuri sana kwenye kuhamasisha utalii. Hivyo, tutajitahidi sana pamoja na maeneo mengine yote yaliyoko Tanzania ambayo yana vivutio kuhakikisha kwamba tunayatangaza ili tuweze kupata watalii wengi na kufikia namba ambayo imekusudiwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 110

***SIDO* Kutengeneza Mashine za Kuchakata Mazao**

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kupitia *SIDO* kutengeneza mashine zitakazosaidia kuchakata mazao ya Wakulima, kama vile mashine ya kutengeneza chips za ndizi, muhogo, sauce za nyama, karoti, pilipilihoho na mbogamboga kwa gharama nafuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exhaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuendeleza viwanda hususan viwanda vidogo sana na viwanda vidogo vinavyolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Serikali imeendelea kulijengea uwezo Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) ili kubuni na kuendeleza teknolojia mbalimbali kutokana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) lina Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (*Technology Development Centres*) katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Kigoma, Lindi, Iringa, Mbeya na Shinyanga kwa ajili ya kutengeneza mashine za kuchakata na kusindika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine hizo ni pamoja na za kutengenza chipsi za ndizi, chipsi za viazi na muhogo, mashine za kukausha mboga mboga na matunda mashine za kusindika nyanya, karoti na mashine kusindika pilipili kwa ajili ya achali kulingana na mahitaji. Aidha, mashine mbalimbali zinazotengenezwa na shirika la kuhudumia viwanda vidogo *SIDO* zinapatikana katika tovuti ya *SIDO* na husambazwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kuititia ofisi za *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya *SIDO* kutengeneza mashine hizo pia imekuwa ikitoa mafunzo ya usindikaji wa muhogo, ndizi, nyanya, karoti, pilipili na mbogamboga katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Bei za mashine hizo hutegemea na uwezo wa mashine yenye kwa maana ya *capacity* na pia mahitaji halisi ya mjasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* imeendelea kutafuta teknolojia mbalimbali za kisasa na nafuu ndani na nje ya nchi hii, ambazo zinaweza kutumika kutengeneza mashine kulingana na mahitaji ya wajasiriamali. Vile vile *SIDO* inasimika

mitambo ya kisasa yenye uwezo wa kutengeneza mashine kwa wingi na huisambaza kwa wajasiriamali kwa ghamra nafuu kwenye vituo vya kuendelezea teknolojia katika Mikoa ya Kigoma, Lindi na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha hili katika mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao, Serikali imeweza kuliwezesha *SIDO* zaidi ya bilioni nne kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo kwa ajili ya wajasiriamali ikiwemo maendeleo ya teknolojia na ujenzi wa majengo ya viwanda vya wajasiriamali wadogo. Naomba kutoa wito kwa wananchi wenye uhitaji wa mashine za kuchakata na kusindika mazao ya kilimo wakiwemo wananchi wa Jimbo la Vunjo, kuwasiliana au kuwasilisha mahitaji yao kwenye Ofisi zetu za *SIDO* zilizopo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuwahamasisha wajasiriamali kwenye maeneo yetu kutumia fursa zilizopo za uwepo wa vituo vya kuendeleza teknolojia yaani *TDC* vya *SIDO* ili kujinufaisha kiuchumi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa majibu mazuri na ya kina kuhusiana na swali hilo ambalo tumeuliza, lakini naomba niulize maswali mawili za ziada madogo. Swali la kwanza; kwa vile *SIDO* inalenga watu wa chini watu ambao wapo kwenye vijiji na kadhalika na hawa watu ni vigumu sana waweze kuelewa hivi vitu alivyovieleza kwa sababu hata mimi nilikuwa sivijui. Je, wana mpango gani wa kuiongezea *SIDO* uwezo wa kujitangaza na kutekeleza maonesho kwenye miji midogo midogo kama Mji wa Himo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusiana na mabanda ya viwanda au majengo ya viwanda. Kasi ya ujengaji wa majengo haya ni ndogo sana pengine tunaenda

na *too much sophistication*, lakini tukienda kwa mtindo mwingine naamini tutaweza tukaharakisha sana ujenzi wa haya mabanda. Je, kama wakienda na kasi hii kweli ni lini wanafikiria watatufikia sisi kule kwenye Mji wa Himo, Uchira na miji midogo midogo kwenye mikoa yetu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uelewa wa wajasiriamali wengi kuhusu huduma zinazotolewa na Shirika letu la Kuhudumila Viwanda Vidogovidogo (*SIDO*) bado si wa kuridhisha sana kwa sababu taarifa nyingi haziwafikii wale wajasiriamali wadogo. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei kwa mawazo mazuri kwamba sasa tuone namna ya pekee ya kuliwezesha shirika letu la *SIDO* kujitangaza zaidi kwa wajasiriamali wadogo ili waweze kutambua fursa na teknolojia ambazo zinatolewa na shirika letu la *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kimei kwamba tunaenda kuwezesha *SIDO* na tunaenda kuwatengea fedha zaidi kwa maana ya mwaka ujao wa fedha 2021/2022 kuwatengea fedha zaidi ikiwemo kwa ajili ya kujitangaza ili angalau wajasiriamali wengi waweze kujua fursa na huduma za teknolojia ambazo zinazotolewa na shirika letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo ya viwanda, naomba niwahakikishie Wabunge na Watanzania wote hasa wajasiriamali ambao wanataka kuwekeza katika viwanda kwa maana ya viwanda vidogo vidogo kwamba, tunakwenda kuwaongezea *SIDO* uwezo ili waweze kujenga majengo mengi zaidi ambapo humo wajasiriamali wetu wataweka viwanda vyao vidogo vidogo au mashine zao

ambazo wataweza kuchakata mazao ya kilimo mbalimbali kulingana na mikoa au mahitaji ya sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaenda kuwaongezea uwezo *SIDO* ili angalau waendelee kujenga majengo mengi zaidi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wajasiriamali. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Uhitaji wa viwanda kwa ajili ya kuchakata muhogo katika Jimbo la Vunjo unafanana sana na uhitaji wa huduma hiyo katika Jimbo la Buyungu. Jimbo la Buyungu na Wilaya ya Kakonko kwa ujumla ni wakulima wazuri sana wa zao la Muhogo. Tatizo letu ni upatikanaji wa mashine hizo za kuchakata na kuweza kupata unga na kuboresha thamani ya zao hilo, lakini pia ni bei...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali, je, ni lini tutapata mashine hizo za kuchakata unga wa Muhogo katika Wilaya yetu ya Buyungu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba kupitia shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo *SIDO*tayari tuna teknolojia mbalimbali na hasa za kuchakata mazao mbalimbali ikiwemo kuchakata muhogo. *SIDO* tayari kupitia ofisi za mikoa na hasa katika

Mkoa wa Kigoma tayari tuna mashine hizo za kuchakata muhogo katika ofisi za Kibondo *DC*, Kakonko, Kasulu na Uvinza. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kupitia Ofisi zetu za *SIDO*, Mkoa wa Kigoma aweze kuwasiliana nao ili kuona kama atapata mashine kulingana na mahitaji yake ambayo ye ye anaomba katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kama katika mashine hizo ambazo zipo katika Mkoa wa Kigoma itakuwa kwamba hazitoshelezi mahitaji yake basi nimhakikishie *SIDO* tupo tayari kuwasiliana nae ili tuweze kutengeneza mashine zinazokidhi mahitaji ya Mheshimiwa Mbunge na wajasiriamali katika Jimbo lake la Buyungu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anthony Mavunde, swali la nyongeza.

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa taasisi za *SIDO* na *TEMDO* zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara zimeonesha ufanisi mkubwa kwenye kutengeneza mtambo wa *destemming* na *crushing* ya zabibu ambayo inapelekea kutengeneza mchuzi wa zabibu ambao umeonekana una tija kubwa sana kwa wakulima. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuziwezesha taasisi hizi mbili ili zitengeneze mashine nyingi zaidi za kuchakata mchuzi wa zabibu ili wakulima waondokane na kuuza zabibu na badala yake wauze mchuzi wa zabibu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anthony Mavunde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali kupitia taasisi za *SIDO* na *TEMDO* tumekuwa tukiawezesha ili waweze kubuni na kutengeneza teknolojia mbalimbali ambazo

zinachakata mazao ya kilimo ikiwemo zao la zabibu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sasa imeamua kwa dhati, kwanza kuziwezesha taasisi hizi kifedha, lakini pia na kuongeza uwezo kwa maana ya Rasilimali watu ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, tayari tumeshawezesha *SIDO* kama nilivyosema zaidi ya bilioni nne lakini pia *TEMDO* zaidi ya milioni mia tano ili waweze kusanifu na kutengeneza teknolojia mbalimbali ikiwemo za kuchakata zabibu.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema kwa wengine kwamba kwa wale ambao wana hitaji teknolojia maalum kulingana na mahitaji ya mazao yao kama hili la zabibu, basi naomba nimkaribishe Mheshimiwa ndugu yangu Anthony Mavunde, katika ofisi zetu za *SIDO* ili tuweze kuona namna ya kukamilisha mahitaji yake ambayo yatafaa kwa ajili ya kukamua zabibu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo Mbunge wa viti maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 111

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Tandahimba-
Newala – Masasi hadi Nachingwea**

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi hadi Nachingwea kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA
M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara nchini *TANROADS* ilikamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtwara -Tandahimba - Newala - Masasi hadi Nachingwea yenyе urefu wa kilometra 255 mwaka 2015. Mpango wa Serikali ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kulinganana upatikanaji wa fedha. Hadi sasa Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi huo katika sehemu ya Mtwara hadi Mnivata yenyе urefu wa kilomita 50 kwa gharama ya Shilingi Biliioni 89.591.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na mipango ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki ya Mnivata - Tandahimba - Newala - Masasi hadi Nachingwea kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021 jumla ya Shilingi Biliioni 10 zilitengwa kwa ajili ya malipo ya mkandarasi wa barabara kwa sehemu ya kwanza ya Mtwara - Mnivata na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mnivata - Tandahimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara nchini imeendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hiyo ili kuhakikisha kuwa inapitika kwa majira yote. Pia napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, baada ya Mheshimiwa Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu wa Tano kuiomba Benki ya Maendeleo ya Afrika kutukopesha fedha za ujenzi wa sehemu hii ya Mnivata - Tandahimba - Newala - Masasi yenyе urefu wa kilometra 160, benki hiyo tayari imetembelea barabara hiyo na kuna dalili nzuri benki hiyo kugharamia ujenzi wa sehemu hiyo ya barabara. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuulizwa maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa barabara hiyo sasa inaitwa kwa jina la dhihaka kwamba ni barabara ya kuombea kura na kwamba katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema jumla ya Shilingi Bilioni 10 zimetengwa kwa bajeti ya mwaka 2020/2021 na sasa imebaki miezi miwili, naomba kuuliza swali, ni lini hasa ujenzi huo unaanza na kukamilika kwa kuwa hata Mkandarasi na ukusanyaji wa vifaa haujaanza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na ubovu wa barabara hiyo vyombo vyia usafiri vimeduwa vikitoza nauli kubwa. Umbali wa kutoza Sh.750 unatozwa Sh.3,000 na kuendelea. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mtwara namna inavyoweza kukomesha ama kuwasaidia kumudu gharama za usafiri ili waweze kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinawahitaji kusafiri? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Mtwara kwa kuwasemea wananchi wake katika jambo muhimu sana la mawasiliano ya barabara. Kwenye swali lake la kwanza amesema ni kweli kwamba zimetengwa Shilingi Bilioni 10 na muda wa bajeti ya mwaka huu imeyoyoma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tu baada ya maswali na majibu tutakaa naye kwa sababu hapa kuna mchakato

fedha zipo zimetengwa kama kuna changamoto kama nilivyosema hakuna taarifa kule eneo la Mtwara hasa TANROADStuwasiliane, tumpe majibu sahihi ili aweze kueleza wananchi wake ni lini barabara hii inaanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anasema nauli imepanda kwa sababu ya ubovu wa barabara kutoka 750 hadi 3,000 na nini kauli ya Serikali. Kauli ya Serikali ni kwamba, Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami kama ambavyo ilivyoahidi kwenye llani ya Chama Cha Mapinduzi. Naomba niwaambie wananchi wa Mtwara na maeneo ya jirani kwamba sasa barabara hii haitakuwa barabara ya kura itakuwa jambo halisi na litatekelezwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii ya Mtwara inafanana kabisa na ahadi ya Serikali kupitia llani ya Uchaguzi katika barabara ya kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Babati kupitia Sukuru – Olkasmenti - Simanjiro – Kibaya, Wilaya ya Kiteto. Je, Serikali ni lini itaanza ujenzi wa barabara hii ili kurahisisha huduma kwa wananchi wa Manyara? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Mbunge wa Vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba kazi inaendelea ilikwishaanza baadhi ya barabara tathmini imekamilika na ujenzi unaendelea. Zile barabara ambazo hazikufanyika mwaka wa fedha 2020/2021, zimewekewa

mpango mkakati wa bajeti ijayo 2021/2022. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Vijana, Mkoa wa Manyara, watu wa Manyara wasiwe na wasiwasi mpaka Simanjiro, tutatekeleza llani ya Uchaguzi kama ilivyoelekezwa na kama ambavyo ndio maagizo ya Viongozi wetu Wakuu hasa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, sasa aulize swali lake.

Na. 112

Barabara ya Kibena mpaka Madeke Kilometra 125

MHE. EDWIN E. SWALLE aliuliza:-

Barabara ya kutoka Kibena (*Stop Lupembe*) mpaka Madeke C Mfiji, kilometra 125, imeshafanyiwa usanifu na upembizi yakinifu tangu mwaka 2015.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi wa Uchukuzi, *Engineer Msongwe* majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kibena - Lupembe - Taweta yenyewe urefu wa kilometra 125 ni Barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Njombe. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara imekamilisha kazi ya upembizi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya

taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha huu wa 2020/2021, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 5.96 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Kibena – Lupembe yenye urefu wa kilometra 50. Aidha, wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa vipande vingine, Wizara yangu inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nina maswali mawillii madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa barabara hii imekuwa ikipata ahadi nyingi sana za Serikali hasa kila wakati wa Uchaguzi mwaka 2015 imeahidiwa haikujengwa na leo inaahidiwa tena ndani ya Bunge lako Tukufu, wananchi wa Lupembe wanapenda kujua kuna utofauti gani wa ahadi za nyuma ambazo hazikutekelezwa na ahadi hii ya leo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi ambaao wataathirika na barabara hii hasa katika maeneo ya Nyombo, Kidegembye, Matembwe, Lupembe Barazani, Igombola, Mfiringa mpaka Madeke? Ahsante

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Msongwe* majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za Serikali si za kubahatisha na namuomba nimuhakikishie kwamba ahadi ninayomwambia leo ni ahadi ya ukweli, awasiliane na uongozi wa TANROAD watamweleza wako kwenye taratibu za mwisho kabisa kutangaza hii barabara hizi kilomita 50 ili

zianze kujengwa kwa kiwango cha lami na hasa tukitambua ni barabara ambayo inaunganisha mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro kuititia Mlimba Ifakara hadi Mkumi. Kwahiylo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge.

Swali lake la pili ni kuhusu fidia ni kweli tathmini ilishafanyika watu walishatambuliwa na gharama za ulipaji wa fidia ulishahakikiwa nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wote wa vijiji na kata alizozitaja watalipwa fidia yao kabla ya ujenzi kuanza. Hili litakwenda sambamba wakati ujenzi utakapokuwa unaanza wanafanya *mobilization* Serikali itakuwa inaendelea na kuwalipa ama kuwalipa fidia wananchi ambao watakuwa wameathirika na mradi huu ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Azan Zungu swalii la nyongeza

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru mvua hizi zinazonyesha nchi nzima zinanyesha nazo Dar es Salaam hali ya barabara za Dar es Salaam ni mbaya na nikisema ni mbaya uchumi wa Dar es Salaam ukianguka ni uchumi wa Taifa unaanguka mapato ya Dar es Salaam ndiyo yanasaidia kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Jimbo la Ilala leo Kariakoo haipitiki, Upanga haipitiki, Soko la Ilala halipitiki wananchi wanauza bidhaa zao sasa barabarani. Mwarobaini ni pamoja na mradi wa *DMDP II* kuweza kuitishwa haraka kusaidia wakazi wa Dar es Salaam na hasa Jimbo la Ilala.

Sasa naiomba Serikali lini sasa Serikali itaanza kutekeleza mradi huu ambao tayari umeshawasilishwa na TAMISEMI *menu* yote ya mahitaji ya barabara ipo tayari Hazina ni lini Serikali inatoa kauli kwa mradi huu unaanza lini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Msongwe swalii hilo linahusu Majiji yote hapa nchini ikiwemo Jiji la Mbeya, Tanga, Mwanza majiji yote

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, katika majiji yetu tuna barabara za aina mbili ziko barabara ambazo ni kweli zinasimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi lakini tunasaidiana na Wizara ya TAMISEMI kwenye baadhi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba kumekuwa na changamoto nydingi hasa kipindi cha mvua pale ambapo barabara zetu nydingi zinakuwa zimekatika lakini kama Mheshimiwa Zungu alivyosema Mbunge wa Ilala tayari upo mpango wa kuzitengeneza barabara hizi zikiwepo barabara zote za Majiji ya Dodoma Jiji la Mbeya, Jiji la Arusha na hata Jiji la Mwanza. Pengine rai yangu kubwa kwa wananchi ni kuhakikisha kwamba mengi ya matatizo tunayopata ni kwasababu aidha tumejenga kwenye mikondo ya maji kwa hiyo tunabadilisha mwelekeo wa maji. Lakini wakati fulani pia mifereji hii haisafishwi na kusababisha maji yanajaa na hivyo kutoka kwenye mikondo yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Zungu tuna mpango kabambe kama Serikali wa kuhakikisha kwamba suala hili tunalifanyia mkakati wa kudumu ili tuweze kuachana na hii adha katika Wizara ya Ujenzi na Wizara ya TAMISEMI ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga Mbunge wa Mbinga Vijijini sasa aulize swali lake.

Na.113

Ujenzi wa Barabara ya Mbinga – Litembo- Kigonsera Hadi Matiri

MHE. BENAYA L. KAPINGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Makamu wa Rais kwa Wananchi wa Mbinga ya kujenga barabara ya Mbinga – Litembo – Kigonsera hadi Matiri kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Msongwe* majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Liuka Kapinga Beyana, Mbunge wa Mbinga Vijiji kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kuitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) tayari imeanza kutekeleza kwa awamu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara tajwa kwa kuanzia na sehemu ya Mbinga – Mbaji – Litembo yenye urefu wa kilometra 24. Hadi sasa jumla ya kilometra 4.89 zimekwishajengwa kwa kiwango cha lami. Kazi hiyo itaendelea kwa awamu kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, wakati Serikali ikiendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili iweze kuitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 674.896 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Kigonsera – Matiri hadi Kilindi yenye urefu wa kilometra 35.32, Serikali inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali ili iweze kuitika majira yote ya mwaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Liuka Kapinga Benaya swalil ya nyongeza.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nishukuru kwa Serikali kuzitamka barabara hizi lakini kwa namna majibu yalivyosemwa yanatofautiana kabisa na uhalisia ahadi hizi zilitolewa na Mheshimiwa Rais Samia Hassan Suluhi mwaka jana. Ujenzi wa kilomita nne unazosema ulijengwa miaka ya nyuma sana, nikiri mwaka jana kulikuwa na ukarabati wa eneo korofi kama mita chache sana siyo

ujenzi. Sasa swalı langu la msingi lilikuwa lini tutaanza kutekeleza lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi hizi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wetu?

Mheshimiwa Spika, swalı la pili Serikali ilitoa ahadi hapa kwamba tutaanza kujenga barabara ya Kitai hadi Kigonsera kilomita tano juzi nimepita pale hakuna kilichofanyika wananchi wananiuliza. Je, Serikali mnawaambia nini wananchi wa Jimbo hili la Mbinga Vijijini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Eng. Msongwe majibu kwa swalı hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati huo akiwa Makamu haingekuwa imeanza kutekelezwa lazima itaanza kutekelezwa katika awamu hii ya bajeti tunayoiendea.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge uvute subira lakini kama tulivyosema ahadi hizi zote ambazo zimeahidiwa ni ahadi ambazo zinatakiwa zitekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili kuhusu barabara ya Kitai, Litui barabara hii ni kati ya barabara za kimkakati ambayo inaenda inapita kwenye makaa ya mawe ya Ngaka na atakubaliana nami Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kilometa tano zimeshajengwa na naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba muda si mrefu kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha barabara hiyo tena inaendelea kujengwa itatangazwa mapema sana kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha na kwa kuhakikishia Mheshimiwa Mbunge unaweza ukawasiliana na *TANROAD* watakuambia taratibu wako kwenye hatua za mwisho kabisa ili mkandarasi aanze kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalı lako kwamba barabara zilijengwa muda wa nyuma ndiyo mpango wenyewe kwamba tayari tulishaanza kujenga na kwa hivyo

tayari hizo kilomita tano tunazitambua tulizijenga na bado tutaendelea na hasa baada tena ya Mheshimiwa Rais kuongezea ahadi yake.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mbinga wafahamu kwamba barabara zao zitajengwa kwa kiwango cha lami kama Serikali ilivyoahidi na kama ilivyo kwenye mpango ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa muda wetu umekwenda na tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka kwa Serikali.

Nilete tangazo la wageni tulionao Bungeni siku ya leo tutaanza na wageni watatu wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo na hawa ni washindhi wa tuzo za mitindo na ujasiriamali Afrika kutoka Jijini Dar es Salaam.

Kwanza ni ndugu Riya Fenandes ambaye ni mbunifufura bora wa mwaka Afrika, hongera sana tunasubiri tuenze kuona haya mambo mazito hapa na Wabunge wako tayari kabisa kama unavyowaona kuja kuona namna gani unaweza kutusaidia ubunifufura wa mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mavazi.

Mheshimiwa Bashungwa anao wageni wengine pia wawili ndugu Jesca mshama ambaye ni mjasiriamali bora wa mwaka Afrika, hongera sana jamani huyu anaongoza Afrika nzima kuwa mjasiriamali kwa hiyo, wajasiriamali wa humu ndani naamini tutajifunza kwa huyu binti yetu Jesca Mshama.

Ndugu Polycap Makoi ambaye ni mbunifufura bora anayenukia Afrika huyu nadhani ni anayeinukia hawa watu wamesema ananukia sasa sijajua kama. Nadhani anayeinukia sasa mbunifufura bora wa mwaka Afrika anatoka Jijini Dar es Salaam. Halafu mbunifufura bora anayeinukia Afrika pia anatoka Dar es Salaam kwa hiyo, vijana wetu wanatutoa kimasomaso. (*Makofii*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Bashungwa ni Watendaji Wakuu wa Mwananchi *Communications* Ltd kutoka Ubungo jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Kaimu Mtendaji Mkuu ndugu Bakari Machumu, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Patrobas Katambi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira kutoka Mkoani Shinyanga ambo ni ndugu David Nkulila Mheshimiwa Mstahiki Meya Manispaa ya Shinyanga na ndugu Geofrey Mwangulumbi ambaye ni Mwenyekiti wa Manispaa karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Jane Jerry Mtate kutoka Taasisi ya Urejesho wa maadili ya Taifa *TUMATA* ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi wao Mtume Joseph Goliamma, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaa ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na ndugu Isaya Njendaluzi, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaa ni wanamaombi kutoka makanisa mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Stella Ikupa kutoka Jijini Dar es Salaam ambaa ni Mkurugenzi wa Kituo cha *Salt* ndugu Rebeca Lady na Outrich Manager wa *Salt* ndugu Fides Uwiso, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili la wageni tutaendelea na ratiba iliyombele yetu. Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - OFISI YA RAIS, TAWALA ZA
MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano majina yameshaletwa hapa na vyama vyenye uwakilishi hapa Bungeni ambavyo vinastahili kuchangia siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Jerry Silaha ajiandae.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru nichukue nafasi hii kwanza kumpa pongeza kwa kupata nafasi hii nzito, lakini tunaamini Mwenyezi Mungu atamuongoza na atamsaidia katika kazi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimoombwe Mheshimiwa Waziri kwa vile umeingia sasa wataalam halmashauri zetu nikisema wa nchi nzima wanahitaji wapewe *training, training* za *innovation, training* za teknolojia, *training* ambazo wataifanya Tanzania iweze ku-score zaidi kwenye *human development index* tunaboresha huduma za afya tunaboresha huduma za elimu lakini lazima kuwe na *training* za ziada ili waweze kufanyakazi vizuri na kuivusha nchi hii iwe sasa iende katika kutambulika katika HDI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam jipya yeye pamoja na Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuweza kukusanya mapato kwa 98% kwa mwaka takriban *billion* 60. Hakuna halmashauri yoyote katika nchi hii inayokusanya bilioni 60 kwa mwaka kama Jiji jipya la Dar es Salaam la llala ambalo lina Majimbo matatu ya Segerea, llala na Ukonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jiji hili bado barabara zetu ni mbaya nimesema kwenye swali lile la muda uliopita sitaki kuchukua muda mwingi kwenye suala la barabara. Tunalo tatizo kubwa sana tumerudishiwa kukusanya *property tax*, *property tax* hii tunarudishiwa kukusanya si mali yetu tunakusanya lakini mapato haya yanakwenda Serikali Kuu ambalo ni jambo zuri lakini gharama za kukusanya hatulipwi kuna *running cost* za mafuta, kuna *running cost manpower*, kuna *running cost* hela nyngi sana ambazo tunatakiwa tuzipate nikucombe Mheshimiwa Waziri hili alitazame ili tuweze kulipwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo jiji liliviyunjwa halmashauri ya Manispaa ya llala ilikabidhiwa miradi yote na mali zote za Jiji la Dar es Salaam ambazo ziko katika paramita za Jiji jipyia la Dar es Salaam *parking fee* ambayo ni halali ya kukusanya na Jiji la Dar es Salaam tunagombania na TARURA, TARURA wanataka na sisi tunataka nikucombe tu Mheshimiwa Waziri uone umuhimu TARURA wakichukua hizi pesa hawazirudishi kuboresha hizi barabara. Kwa vile hawaboreshi barabara ni bora tuzikusanye sisi ili tuwape watengeneze barabara za Mkoa mpya wa Dar es Salaam kwa maeneo ambayo pesa hizi zinakusanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikucombe sana Mheshimiwa Waziri ultazame hili na mapambano ambayo tunapambana sasa hivi katika Jiji la Dar es Salaam kuhusu mapato. Mapato ya Jiji la Dar es Salaam Jipyia kwa mwezi kwenye *fee* ya *parking* 1.1 billion shillings ni hela nyngi sana. Sasa hii ni halali ya wakazi wa Dar es Salaam si halali ya TARURA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikucombe lingine TARURA wanafanyakazi vizuri sana wana wataalamu wazuri CO wao mzuri ma-engineer wazuri lakini hawana pesa. Pesa wanazopewa na Serikali wanaopewa pesa za *maintenance*. hawapewi pesa za kutengeneza barabara nimeona kwenye vitabu sasa hivi kuna pesa zimetoka za maendeleo. Lakini naomba u-revisit na Hayati Rais Magufuli

alitoa agizo siku alipokuja kufungua soko la Kisutu Jiji jipyia la Dar es Salaam lipewe pesa zaidi za barabara ili uchumi ukue na tuweze kusaidia maeneo mengine nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla, Waziri wa Fedha yuko hapa, *fee ya ada ya simu, miaka yote tunapigania mapato ya simu*, Ethiopia miradi mikubwa inaendeshwa na ada na tozo katika simu. Tukitoza shilingi 50 tuna-*card holders* wa *simcard* Tanzania sasa hivi zaidi ya milioni 52, tuchukue watu wachache milioni 30; *only thirty* milioni wale ambao wataweza kulipa shilingi 50 kwa siku *we end up getting* bilioni 540. Tutafute vyanzo vipyia, *TRA* msidumae tu kukamata Bharesa, Mohamed Dewji, sijui *Enterprises* nani, tafuteni vyanzo vipyia, *there is a lot money kwenye simu. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitizama hii sintofahamu ya bando ambapo tumechukua kama mwezi mzima au wiki tatu fedha zimepotea. Hebu *TCRA* fanyeni *forensic audit* kwenye *eaverage users* per kila mtu mtizame shilingi ngapi ambazo makampuni hayo yamechukua ili muweze kuwadai zirudi katika Mfuko wa Serikali na zilete maendeleo katika Taifa letu. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe masuala ya wananchi kulipa ada ya ziada ya simu ni uzalendo. Leo hatuandiki barua, hatuna gharama ya *stamp*, leo mtu yuko Mwanza anauliza soko la Pugu la ng'ombe ni shilingi ngapi, leo mtu yuko Mwanza anauliza soko la samaki ni shilingi ngapi, hii ni nafasi nzuri tuwe na kodi ya uzalendo. Tukisema shilingi 50 kwa watu milioni 30 tunaenda kupata bilioni 540. Tukisema tukiweka shilingi 100 kwa siku tunapata triliioni moja na bilioni themanini. Haya ni mapato ambayo yatasaidia kuchochaea maendeleo ya nchi yetu na maendeleo ya Dar es Salaam na majimbo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ije sasa na mikakati ya kuboresha miundombinu. Nimeuliza swali hapa lakini naendelea kusisitiza kwa vile nina muda umuhimu wa

kuboresha miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kibamba, Ukonga, Ilala, Segerea miundombinu ni mibovu, kuna maeneo hayapitiki katikati mjini. Leo tumeoneshwa wabunifu ambao wameshinda tuzo za Afrika, wanapokuja kupewa hizi zawadi, wale wanaokuja na hizi zawadi wanashangaa barabara za wabunifu Tanzania. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ione umuhimu wa kuboresha miundombinu hii. Fedha zipo, tubadilishe aina na namna gani ya kutafuta kodi za Watanzania. Fedha ziko nyingi sana tubadilishe mfumo wa kukusanya kodi ili sasa mapato haya yaweze kupatikana kwa wingi sana na yaweze kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *DMDP II*, ni mradi muhimu sana kwa Taifa na kwa Dar es Salaam. Mradi huu haupo Dar es Salaam tu, uko nchi nzima. Dar es Salaam inatajwa sana kwa sababu kwa sababu ni D inaanza na Dar es Salaam na mradi huu upo kwenye umwagiliaji, Kilimo, kuboresha masuala mengine ya utalii na vitu vingine. Kwa hiyo, naomba sana tuendelee kuboresha miundombinu tupate maendeleo katika Taifa letu. Tuboreshe Dar es Salaam, tuijenge Dar es Salaam ili iweze kusaidia mikoa mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, biashara Dar es Salaam zimekufa, wafanyabiashara wa Dar es Salaam wanaondoka wanakwenda nchi zingine kufanya biashara sababu wanashindwa kupita kwenye barabara katikati ya mji. Jimbo la Ilala lina wakazi wengi wanasema wa chache ni kweli lakini kuanzia asubuhi saa kumi na moja mpaka saa tatu usiku tunaudumia watu milioni mbili katika kieneo kile, utaona uchumi ambao unaweza ukawa *generated* kwa watu wale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pengine nimkumbushe Mheshimiwa Waziri a-train watu wake katika *innovation* na teknolojia mpya waweze kuwa na uelewa mkubwa kwenye mambo ya afya, elimu na katika mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi, atafuatiwa na Jerry Silaa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema mpaka kufikia siku ya leo. Napenda niwatakie Ramadhan Kareem Waislam wote nchini Tanzania, wawe na mfungo bora na wenye amani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka niwashukuru wapiga kura wangu wote wa Mkao wa Dar es Salaam, kwa kweli wamenifanyia jambo kubwa sana. Nawashukuru sana nami nawaaidi mbele yako kwamba nitawatendea haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee pia niwapongeze na kuwashukuru wagombea wenzangu 300 wa Mkao wa Dar es Salaam kwa kunipa *support* kubwa sana kwa sababu pamoja na kujiombea wao walikuwa wananiombea na mimi pia. Nashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye Wizara ya TAMISEMI, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kuteuliwa kwake na sina mashaka naye maana ni ndugu yangu ambaye ninauhakika na utendaji wake wa kazi. Pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hii ya TAMISEMI, nina hakika kwamba watatutoa pale tulipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwenye mchango wangu na utajikita katika maeneo manne; elimu, afya, barabara na masoko kama muda utakuwepo. Kuhusiana na

suala nzima la elimu nitaanza kwanza na hoja ya walimu. Walimu wana masikitiko makubwa, walimu wa shule za msingi na sekondari waliostaafu wana madai yao ya nauli huu sasa ni mwaka wa tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu hawa Tanzania nzima Shule za Msingi na Sekondari wanadai fedha zao za nauli, wamelitumikia Taifa hili kwa amani kwa utulivu na kwa moyo wao wote na kwa sababu kazi ya uwalimu ni wito na moyo. Leo hii walimu wanastaafu wanahangaika wanakwenda kwa Wakurugenzi, kuna wengine wanawapa majibu mazuri, lakini kuna wengine wanawapa majibu yasiyofaa, wanawaambia nendeni TAMISEMI fungu lenu haliko katika halmashauri. Hii ni kero kubwa, naomba Serikali sasa itoe majibu walimu hawa stahiki yao ya nauli au mizigo ipo au haipo. Kama imefutwa basi ni bora waambiwe watulie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu hawa wanataka kuja huku Dodoma, mimi wananiuliza wewe mwalimu mwenzetu umetoka hapa kwenye shule ya msingi leo umekwenda Bungeni unashindwa kututetea hata sisi walimu wenzi tunapata tabu. Mimi nasema walimu wenzangu leo wanisikie, naomba Serikali iwaangalie walimu hawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba niishauri Serikali wangu, walimu hawa miaka ya nyuma walikuwa wanalipwa kwenye halmashauri zetu nikiwepo mimi, nimelipwa fedha yangu ya mizigo milioni moja laki tatu kwenda kwetu Lindi sikuwa na tatizo lolote, huu mpango uliyokuja kubadilka wa kutoka huku kuja kwenye Serikali Kuu ndiyo shida ilipoanzia. Sasa naomba kuuliza hii shida itaendelea kuongezeka mpaka lini? Niombe Serikali sasa iwe na mpango. Mheshimiwa Waziri mdogo wangu, naomba akija hapa aje na majibu, walimu wake wanateseka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya walimu, sasa nizungumzie suala la elimu ya shule ya msingi. Niombe Serikali sasa ije na mpango maalumu wa kukarabati sasa shule za msingi zilizo kongwe. Nimeona

imekarabati vizuri shule za sekondari zilizo kongwe, lakini sasa twende kwenye mpango maalumu wa kukarabati shule za msingi zilizo kongwe. Kuna shule za muda mrefu, kwa mfano Shule ya Msingi Kisiwani, Kigamboni sasa hivi majengo yake baada ya ujenzi wa barabara yamekuwa mafupi mno kiasi kwamba imekuwa kama vibanda. Niombe Serikali katika mpango wake wa ukarabati waiangalie Shule ya Msingi ya Kisiwani, Kigamboni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo Shule ya Mchikichini, Mbagala, pale kuna uwanja mkubwa ambao Samatta aliweka *television* kwa ajili ya kuangalia, lakini ukienda kwenye majengo ya shule ile inatia huruma, mabati yote yamekwisha kwa kutu. Pia ipo Shule ya Nzasa, Mbagala ambayo ina historia kubwa ya kutoa wanafunzi wengi kwenda sekondari; wazazi wengi walikuwa wanaigombania shule hiyo ili watoto wao waufaulu, leo hii shule hiyo baadhi ya majengo ni chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Shule ya Msingi Baruti katika Halmashauri yangu ya Ubungo inahitaji ukarabati. Pia ipo Shule ya Msingi Buguruni na Shule ya Msingi *Mbezi Beach*. Shule ya Mbezi haiendani na mazingira ya *Mbezi Beach* naomba shule iendane na mazingira ya *Mbezi Beach*. Pia Shule za Msingi za kwanza kabisa Uhuru na Msimbazi nazo zinahitaji ukarabat. Hizi nimetoa kama mfano tu lakini shule zote kongwe naomba ziangaliwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke eneo hilo niende kwenye eneo la afya. Naipongeza Serikali kwa kujenga hospitali za wilaya 102 nchi nzima, ni jambo kubwa, naipongeza sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naomba waangalie baadhi ya hospitali katika Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zimezidiwa. Hospitali ya Palestina Sinza kwa kweli ni ndogo lakini inategemewa sana; mgonjwa yejote anayetoka kwenye hospitali ndogo anakwenda Palestina, kama Mungu akijalia itakapoisha Hospitali yetu ya Wilaya ndio atapelekwa huko.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele imeshagongwa.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba sana na Hospitali ya Mbagala Zakiem na Vijibweni ziangaliwe kwenye bajeti. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mnaochangia lengo la Kanuni zetu kuelekeza kwamba uzungumze na kitinipamoja na wewe kutazama huku mbele. Ndiyo maana Kanuni hizo hizo zinakataza kusoma ili uwe unanitizama mimi natoa ishara gani. Ukishaona nimewasha hii *microphone* maana yake muda wako umekwisha, ukichelewa inabidi nizungumze kwamba muda wako umekwisha. Kwa hiyo, tuangalie huku mbele wakati tukichangia ili ukiona tu nimewasha ujue muda wako umekwisha.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jerry Silaa atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ajiandae.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nami niungane na wenzangu kumpongeza sana dada yetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu na wenzake wote kwa nafasi na fursa waliyoipata kutumikia Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitaukeleza kwenye maeneo matatu lakini kwanza ni kwenye Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam lina historia ndefu kuanzia mwaka 1920 lilipopata hadhi ya kuwa mji mpaka lilipokuwa Manispaa ya Dar es Salaam mwaka 1949 na lilipopata hadhi ya kuwa Jiji tarehe 10 Desemba 1961. Mafunzo tuliyoyapata kutoka mwaka 1972 mpaka mwaka 1978 kwenye Madaraka Mikoani na mafunzo tuliyoyapata

kuanzia mwaka 1996 mpaka 2000 kwenye Tume ya Jiji, naamini tunaweza kuyatumia kwa upana wake katika kuhakikisha tunatengeneza mbinu bora zaidi ya kutengeneza mazingira ya uongozi na utawala kwenye Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa kuanzisha ama kwa kuipandisha hadhi Manispaa ya llala kuwa Jiji la Dar es Salaam. Tunapozungumzia masuala ya majiji, tunazungumzia maisha ya watu na makazi kwa maana ya *urbanization*, lakini niseme tu kwamba Dar es Salaam kwa kipindi kirefu imekuwa ikiendeshwa bila *master plan*. *Master plan* ya mwisho iliandikwa mwaka 1979 na kwa bahati mbaya hizi *master plan* huwa zinatakiwa kuhuishwa kila baada ya miaka mitano. Hata hivyo, *master plan* hii ilikuja kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali mwaka 1984 miaka mitano muda ambao ultakiwa *master plan* hii ihuishwe lakini tokea wakati huo jiji hilli limekosa *master plan*. Naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwamba mwezi Juni, 2020 katika Gazeti la Serikali tumetangaziwa *master plan* ya Jiji la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumzia *master plan* ya Jiji la Dar es Salaam tunazungumzia Mkoa mzima wa Dar es salaam, lakini tunazungumzia wilaya za jirani ambazo kutokana na ongezeko la makazi, sasa zimeungana na Jiji la Dar es Salaam. Wilaya za Bagamoyo, Kibaha, Kisarawe na Mkuranga, zote sasa zimeungana na Jiji la Dar es Salaam. Sasa tumepata Jiji pale kwenye Manispaa ya llala imekuwa Jiji la Dar es Salaa lakini juzi tumeona Manispaa ya Temeke nayo imeomba na ina vigezo vya kuwa jiji naamini Kinondoni nayo itafika wataomba jiji na naamini kuna siku Ubungo nao wataomba jiji, tutakuwa na majiji mengi. Dhana hasa ya kuwa na jiji ni ya kupata mamlaka yenye uwezo wa kusimamia *master plan* hii ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko Mheshimiwa Mbunge hapa alichangia kwenye mpango wenzetu kwenye majiji mengine wamewahi kutafuta namna bora zaidi ya kuhakikisha majiji haya yanakuwa na miundombinu ya uhakika na uongozi ambao unaweza kusaidia maisha ya

wakazi wa jiji lile kuwa maisha yanayoendana na maeneo mengine. Ziko nchi zimetengeneza Wizara za masuala ya jiji, ziko nchi zimetengeneza mamlaka ya kusimamia jiji. Niombe Serikali iiangalie Dar es Salaam na maeneo yanayozunguka maana jiji hili ndio linazalisha zaidi ya asilimia 70 ya mapato ya nchi yetu iweze kutengeneza mfumo ambao utasaidia kuboresha makazi ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu hapa amesema, leo Dar es Salaam tunavyozungumza mvua zimenesha, Dar es Salaam haipitiki, maisha ya wananchi yamekuwa ya tabu. Leo mtu kutoka kule Mzinga Magore, Bomba Mbili Majohi, Mpemba Majohi, Mkolemba anatumia zaidi ya shilingi 1,000 kupanda bajaji imfikishe kwenye eneo la kupata usafiri kwenda mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitaungana na wenzangu kuendelea kuisii Serikali iangalie umuhimu wa Mradi wa Dar es Salaam wa *Metropolitan Development Project (DMDP II)*. Nami niseme tu pamoja na kuungana na wenzangu kwamba tunapozungumza kwenye bajeti ya TAMISEMI, dada yetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni mchapakazi, hilo hatuna shaka na ana Manaibu Waziri wazuri lakini wenzetu hawa ni watumiaji wa bajeti kama sisi wengine tujipange vizuri kwenye kuishauri Serikali jinsi ya kupata fedha kwenye bajeti ya Wizara ya Fedha na bajeti kuu ya Taifa ili miundombinu ya Dar es Salaam iweze kuboreka, wananchi wale waendelee kuzalisha uchumi na mapato ya Taifa hili yazidi kuboreka kupitia miundombinu ya barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge katika kipindi cha kampeni na katika michango yetu mingi humu ndani tunasema kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana kwenye sekta ya afya, elimu na sekta nyingine zinazosimamiwa na Wizara ya TAMISEMI. Zimejengwa zahanati nyingi, vituo vya afya vingi, hospitali za wilaya, shule Kongwe zimekarabatiwa na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya inaendelea. Naomba kusema jambo moja hasa katika nyakati hizi ambapo miradi yetu mingi hii inatekelezwa kwa *force account*, kazi hizi zimefanywa na

Wakurugenzi na watendaji wa halmashauri zetu nchi nzima. Sikatai, yawezekana wako watendaji wachache wenye upungufu lakini wako watendaji wengi wanaofanya kazi nzuri ya ujenzi wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Serikali, nawaomba; Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati za Fedha na Utawala kwenye Halmashauri zetu; na kamati hizi ndiyo Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wote ndani ya Halmashauri. Nawaomba sana, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Wale watumishi wenye upungufu tuwachukulie hatua kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma na Sheria ya Utumishi wa Umma; na wale wanaofanya vizuri tuwapongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusimbebeshe Waziri wa TAMISEMI mzigo wa kuwa *disciplinary authority* ya mpaka Mtendaji wa Kata majukumu ambayo ni ya kwetu kule Halmashauri. Tusigueze Bunge hili ikawa ni sehemu ya kuja kusulubu watu ambao bahati mbaya wengine hawana uwezo wa kuja kujitetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iendelee kusimamia nidhamu ya watumishi, lakini na sisi tuwaangalie tuwaangalie wenzetu amabo ni wadau wenzetu...

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jerry Silaa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa msemajji, lakini kwanza nampongeza kwa alivyoanza. Ila naomba amalizie kwa kusema Dar es Salaam isiwe mamlaka, iwe na Wizara ya kuiendesha Dar es Salaam. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sasa unaipokea hiyo taarifa ambayo imeku kwa namna ya wazo jipya! (*Kicheko*)

MHE. JERRY W. SILAA Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili; na ametujenga, ndiyo maana nikasema iko Miji ilichukua mbinu tofauti hili Serikali iangalie maeneo haya, kwa maana ya Wizara, kama ni *Dar es Salaam Metropolitan Authority* ili tupate mamlaka nzuri ya kusimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya na Mheshimiwa Rose Vicent Busiga ajiandae.

MHE. HAWA S. MWEIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya TAMISEMI. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya na kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia hotuba katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nampongeza Mheshimiwa Waziri Ummey kwa uteuzi. Sina mashaka na utendaji wake, ninaamini kabisa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atasimamia Wizara hii sawa sawa ili mambo yawezee kwenda sawa sawa huko chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote mazingira bora ya kufundishia na kujifundishia yanategemeana sana na uwepo wa miundombinu rafiki na wezeshi. Hali hii huko chini haipo. Ninaposema hali hii huko chini haipo, ni ukweli usiopingika, miundombinu ya kufundishia siyo rafiki kabisa.

Mimi natokea Mkoa wa Tabora ambaeo ni moja kati ya mikoa iliyoko pembezoni na ni moja kati ya mikoa ambayo ina changamoto kubwa sana za miundombinu ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mkao wa Tabora ni moja kati ya mikoa mitatu ya juu ambayo inaongoza kwa watoto kupata ujauzito. Hii inatokana na watoto kutembea umbali mrefu kufuata shule zilipo. Vile vile Jimbo la Tabora Mjini ni moja kati ya majimbo ambayo yana changamoto kubwa sana ya Shule za Sekondari. Mtoto anatoka umbali mrefu mno kufuata shule ilipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa Kata chache za Tabora Mjini. Kuna Kata ya Kakola ambayo haina kabisa Shule ya Sekondari, haina! Watoto wa Kakola, anatoka Kata ya Kakola umbali wa zaidi ya kimometu 30 kufuata shule kwenye Kata ya Uyui. Anapotembea kutoka Kakola kuja Uyui, siyo kwamba anatembea kwenye barabara, ni pori kwa pori mpaka afike kwenye Kata nyingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yanayomsibu mtoto wa kike kwenye maeneo hayo ni mengi sana. Tutalaumu wazazi, lakini mwisho wa siku wazazi pia wanajitahidi kwa kadri inavyowezakana. Naiomba sana Serikali, iangalie uwezekano wa kipeleka Shule za Kata kwenye maeneo ambayo hayana Shule za Kata hasa kweye kata za pembezoni katika Jimbo la Tabora Mjini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule nyingine za Kata ziko katika Kata nyingine. Kwa mfano, Kata ya Gongoni ambayo mimi ndio natokea, Kata ile tunaambiwa kuna shule pale, lakini shule hii iko kule Lwanzari ambako ni Kata ya Ng'ambo. Kwa hiyo, mtoto anapofaulu katika Shule za Kata ya Gongoni anatakiwa moja kwa moja aende Lwanzari, atembee zaidi ya kilomita 20 kufuata Shule ya Sekondari ya Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii taarifa kwamba kila Kata ina Shule za Sekondari, kwa kweli siyo sahihi. Tatizo hili lipo kwenye kata nyingi. Kata ya Kanyenye; Shule ya Sekondari ya Kata ya Kanyenye inapatikana katika Kata nyingine kabisa ya tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, Wizara iangalie...

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami Mbunge ninayetoka Mkao wa Tabora. Anasema kutoka Gongoni kwenda Lwanzari ni kilometa 20, hapana, ni kilometra nne. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga unaipokea taarifa hiyo?

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, inategemea na Gongoni sehemu gani? Kwa hiyo, asichukulie Gongoni ya hapa mpaka pale kwamba ni kilomita nne. Kwa hiyo, naomba atulle kwanza, naye atawezekuchangia kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo kwa shule ni kubwa sana. Kata ya Itonjanda katika Jimbo la Tabora Mjini ni kata ambayo ina changamoto kubwa sana ya Shule ya Sekondari. Kuna Shule ya Sekondari moja pale *Itonjanda Centre*, lakini wazazi wa Kata ile katika Kitongoji cha Kilino waliamua kwa nguvu zao kujenga Shule ya Msingi. Walipata msaada wakajengewa madarasa mawili na ofisi ya mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujengewa madarasa yale, watoto wa Kitongoji cha Kilino wanatosha darasa la kwanza na la pili peke yake, basi. Ukitaka kumuendeleza mtoto wako madarasa yanayofatia ni lazima uende *centre*. Kutoka Kilino kwenda pale *centre* ni umbali mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wale waliamua kujichangisha wenyewe, wakaweka mawe, wakanunua na *cement*. Kwa masikitiko makubwa *cementile* imekuwa jiwe, kwa sababu Serikali imeshindwa kuwasaidia kuendelea kujenga madarasa yanayofuata ili watoto wao wawzeze kupata elimu, ukizingatia kitongoji kile watu wanaoishi kule

ni wafugaji wa jamii ya Kisukuma, walioamua kwa dhati ya moyo wao kwamba watoto wao waende shule, lakini wakisoma darasa la kwanza na pili, biashara imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie aje aone hilo eneo, aone ni namna gani Wizara inaweza kusaidia watoto wale ili waweze kuendelea na masomo badala ya kuendelea kuwa wafugaji maisha yao yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Tabora Mjini zina zaidi ya watoto 2,000 katika shule moja. Tunaposema elimu bora ndugu zangu, ni pamoja na kuangalia idadi ya watoto katika shule husika. Wakati sisi tukiwa tunasoma; mimi nimesoma Shule ya Msingi Isike, darasa langu lilikuwa na wanafunzi 48 peke yake mpaka namaliza darasa la saba, lakini leo darasa moja lina watoto zaidi ya 100 na kitu. Hii idadi ya watoto 2,000 kwenye hizi Shule za Msingi, ni kipindi ambacho tuko kwenye kampeni, ndiyo idadi hiyo ilikuwepo. Sijui sasa hivi watoto waliosajiliwa kuingia Darasa la Kwanza hali iko namna gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, miundombinu ya madarasa haipo, siyo rafiki kabisa, watoto wanabana, watoto wanasoma asubuhi na jioni na elimu ya mchana siyo elimu nzuri hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya kwenye suala la elimu, namwomba sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu atusaidie katika Mkoa wetu wa Tabora katika zile shule 300, naomba sana, chonde chonde, Mheshimiwa Waziri atuangalie kwa jicho la tatu Mkoa wa Tabora hasa Halmashauri ya Tabora Mjini ili tuweze na sisi kupata hizo shule ziweze kusaidia wananchi wetu kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Sekta ya Afya.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Ya pili! (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, atafuatiwa na mheshimiwa Rose Vicent Busiga na Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi nikushukuru sana kwa hii nafasi. Vile vile nichukue nafasi hii kipekee kumshukuru sana Waziri wa TAMISEMI, dada yetu Mheshimiwa Ummy pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamfahamu vizuri sana dada yetu Mheshimiwa Ummy, hatuna wasiwasi kabisa na utendaji wake. Pia tunawafahamu Manaibu wake vizuri sana, hatuna wasiwasi kabisa na utendaji wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina mambo matatu ambayo nahitaji kuishauri Serikali. Jambo la kwanza nitashauri kwa upande wa afya ya msingi, jambo la pili nitashauri upande wa barabara na madaraja na jambo la tatu nitashauri kuhusu suala la ugatuzi wa madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Jimbo langu la Manyoni Mashariki lina zaidi ya vijiji 60. Katika vijiji vile 60 nina vijiji 29 ambavyo vina Zahanati. Vile vile nina Kata 19 na katika Kata hizo, nina Kata mbili ambazo zimejengewa Vituo vya Afya. Kwanza nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutujengea Vituo vya Afya viwilli; Kituo cha Afya cha Kintinku ambacho tayari kimeanza kutumika na Kituo cha Afya cha Nkonko ambacho tayari kilishakamilika, lakini bado kuna changamoto za hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Waziri, lakini naomba nimkumbushe mambo mawili. Jambo la kwanza, kwenye Vituo vya Afya viwili ambavyo vimejengwa hususan Kituo cha Afya Nkonko tayari kimekamilika, lakini bado hatuna wataalam. Tulipeleka mtaalam mmoja ambaye ni Daktari (*Medical Doctor*),

hakuweza kuripoti. Kile Kituo cha Afya ni kikubwa sana, kinahudumia zaidi ya Kata sita. Naishukuru tena Serikali kwa kutupa hiyo nafasi, lakini bado kile Kituo cha Afya hakitumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba niishauri Serikali, kwa sababu tuna tatizo la hao wataalam kwenda kwenye Vituo vyetu vya Afya, nadhani tunahitaji kuja na mbinu mbadala. Naishauri Serikali husasan Wizara ya TAMISEMI tuangalie jinsi gani tunaweza tukafanya *mapping* ya wale vijana waliomaliza Shahada za Umdatari kwenye kanda husika, kwa mfano, Kanda ya Kati ili tunapowapangia vile vituo, tupange kulingana na kikanda. Hii itapunguza kasi ya vijana kutowasili au kutoripoti kwenye vituo yao. Naomba nilishauri hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nawaza kuhusu *balance* kwamba, kati ya kujenga Kituo cha Afya na Zahanati kipi kianze? Natambua kwamba Sera yetu ya Afya inatambua kila Kata lazima iwe na Kituo cha Afya, kila Kijiji lazima kiwe na Zahanati, lakini katika llani ya Chama cha Mapinduzi vile vile imebaini kwamba kila Kata inatakiwa iwe na Kituo cha Afya, lakini kila Kijiji kiwe na Zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nini? Ni wakati gani sasa tunahitaji kuanza kujenga Kituo cha Afya na ni wakati ambapo tunahitaji kuanza kujenga Zahanati? Hoja yangu inajikita kwenye eneo langu la Jimbo la Manyoni Mashariki ambapo nina vijiji zaidi ya 60 lakini nina Zahanati 29 tu; nina Kata zaidi ya 19 na Vituo Afya viwili. Nadhani Mheshimiwa Waziri unahitaji kuangalia zaidi jinsi ya *ku-balance* unapofanya maamuzi aidha uanze *ku-exhaust* Zahanati kwenye Kata *then* twende kwenye kujenga Kituo cha Afya, badala ya kujenga Kituo cha Afya kwenye Kata ambayo haina Zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nalisema hili? Kuna vijiji vipo mbali sana na kupata huduma za afya. Ningetamani kuona kila Kijiji kinapata Zahanati, *then* ile Kata ambayo tayari ina Zahanati *i-qualify* kupata Kituo cha Afya. Lengo letu ni kupunguza umbali wa watu kupata huduma za afya, lakini

vilevile ku-promote suala *health seeking behavior* ili watu wasikimbilie kwenye dawa za kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la barabara. Naishukuru Serikali kwanza kwa Kuanzisha *TARURA*, nilishasema huko nyuma; na kwa Jimbo la Manyoni Mashariki tuna mtandao wa barabara zaidi ya kilomita 1,000 na bajeti yetu kwa mwaka tunapata takribani milioni 600. Mwaka huu tumekumbwa na matatizo makubwa sana ya kuharibika kwa barabara, barabara ya Kintinku Makanda takribani kilomita 30 imejifunga kuanzia Januari mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makanda kuna mnada mkubwa sana ambao unachangia pato la Wilaya yetu ya Manyoni, lakini tuna barabara ya kutoka Iseke - Mpapa - Simbanguru – Mangori, ilijifunga kwa muda mrefu sana. Vile vile tuna barabara ya kutoka Chikuyu - Chibumagwa - Mahaka kwenda Sanza, nayo ilijifunga kwa muda mrefu sana. Tunahitaji kufanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni muda muafaka, watu wengi wamesema tunahitaji kuipa nguvu *TARURA*, naunga mkono hilo. Kwa upande wa Manyoni Mjini ningemshauri Mheshimiwa Waziri hasa kwa mijini, wilaya ambazo tunazo, Makao Makuu ya Wilaya, sidhani kama bado *TARURA* wanahitaji kuendelea kukarabati kwa kiwango cha vumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kuona katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri wanatenga angalau kilomita moja kwa ajili ya kujenga barabara za mijini, Makao Makuu ya Wilaya kwa kiwango cha lami, kuliko kuja na barabara za vumbi kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Hizi barabara za changarawe na vumbi tuzipeleke vijijiini, Natamani kuona tunaboresha Makao Mkuu yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanjari na hilo, vile vile natamani kuona mnapokuja na mpango wa kujenga barabara za lami kwenye maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya tuangalie jinsi gani tutaweka taa za barabarani kwa

ajili ya kuboresha miji yetu na vilevile kuwafanya wafanyabishara weweze kufanya kazi kwa muda mrefu na pia itaboresha usalama wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni suala la ugatuza wa madaraka. Mimi ni muumini wa ugatuza wa madaraka, nimehusika sana katika mchakato wa kuandaa Sera ya Ugatuza Madaraka. Wote mnatambua kwamba suala la ugatuza wa madaraka lilianza miaka ya 1998 ambapo tulianza na *D by D Policy Paper*, ambayo imekaa kwa zaidi ya miaka 20, lakini hatujawahi kuwa na Sera ya Ugatuza wa Madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *D by D Policy Paper* ndio ilitumika kama sera ambayo tumeitumia sana kuja na *program* ya kwanza ya maboresho ya Serikali za Mitaa na *program* ya pili ya maboresho ya Serikali za Mitaa ambayo iliisha 2014. Kuanzia mwaka 2019, natambua TAMISEMI walianza mchakato wa kutengeneza Sera ya Taifa ya Ugatuza wa Madaraka. Hoja yangu ni nini? Napenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, mchakato wa ile sera ya ugatuza wa madaraka imefikia wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, namshukuru Mheshimiwa Waziri, katika bajeti yake ameweza kutenga fedha kwa ajili ya *program* ya kuimarisha Serikali za Mitaa na Mikoa, yaani *Regional and Local Government Strengthening Program*. Napenda kujua kwamba ni kwa jinsi gani sasa Wizara inakuja kuwahusisha wadau wa maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba katika kuandaa hii *program* na hata hii Sera ya Ugatuza wa Madaraka, wadau mbalimbali walihusika sana wakiwepo *USAID, UNICEF, EU, DFID, JICA* na wengine: Je, Mheshimiwa Waziri amejipangaje kuhakikisha anawahusisha hao wadau ili kiasi cha *one point five billion* ambacho tumekipanga kwenye bajeti yetu tuweze kupata nguvu vilevile ya wadau ambao walihusika sana katika kuhakikisha kwamba suala la ugatuza wa madaraka linaenda kupata kipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake na ninaomba niseme kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimwa Rose Vicent Busiga, atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

MHE. ROSE V. BUSIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia tena kwa mara nydingine. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ametulalia siku ya leo.

Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Ummey Mwalimu kwa namna ambavyo ameendelea kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana pamoja na timu yake nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nikikaa kimya nitakuwa sijawatendea haki watendaji wenzangu nchi nzima wa Kata na Vijiji kwa sababu Wizara hii ya TAMISEMI inawagusa wao.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka niliwasilisha wasilisho langu la kuomba Wizara ya TAMISEMI iangalie vizuri namna ambavyo inaweza kuwasaidia Watendaji wa Kata pamoja na Watendaji wa Vijiji kulingana na jinsi ambavyo wanafanya kazi katika mazingira magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wazi kabisa watendaji hawa ndio wanaosimamia maendeleo katika kata zao, katika vijiji vyao, lakini pia nikijikita kwenye suala la ukusanyaji wa mapato, Watendaji hawa wa Kata na Vijiji ndio wanaokusanya mapato na wanokusanya mapato katika mazingira magumu sana. Nawea kutoa mfano mmoja tu, katika ukusanyaji wa mapato wa kodi ya jengo. Kodi ya jengo ilikuwa ni ngumu sana kuikusanya kwa upande wa TRA, lakini Watendaji wa Kata na Vijiji waliweza kukusanya kodi ya jengo vizuri na wakafikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni nini Serikali ifanye; naiomba Serikali yangu kuptitia Wizara ya TAMISEMI, namwomba Mheshimiwa Ummy Mwalimu aweze kuwasaidia watendaji wa kata waweze kupatiwa pipipiki kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa maendeleo katika kata zao. Hii itaweza kuwafanya watendaji hawa wafanye kazi kwa kujituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali yangu iangalie ofisi zao. Ofisi zao zinatia aibu, hazifai. Mimi mwenyewe nikiwa Mtendaji wa Kata siku moja mvua ilinyesha, nilitaka kuangukiwa na lile boma. Kwa hiyo, mimi mwenyewe ni shahidi mkubwa, ofisi zinazotumika na wao ni haya majengo ambayo ni *ma-godown*. Kwa hiyo niiombe sasa Serikali waweze kuwasaidia Watendaji wa Kata waweze kupata ofisi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia Watendaji wa Kata hawa ndio wakurugenzi kwenye kata zao. Niiombe Serikali iangalie namna ya uendeshaji, watendaji waweze kupata motisha ya kila mwezi kama wanavyopata waratibu wa elimu kata. Ukiangalia mtendaji huyu anafanya kazi katika mazingira magumu. Naiomba Serikali kwa uchungu mkubwa, wawaangalie sekta hii ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri, Mheshimiwa Ummy, yeye mwenyewe amekuwa shahidi wa watendaji, wanalia kila siku awatazame. Naamini dada yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Ummy, kwa namna anavyojuua kuchapa kazi mwaka huu wa 2021 kilio cha watendaji kitakwenda kufutika. Namwomba mtani wangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, asiniangushe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Ofisi hii ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kable ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ametujalia uzima hata leo tukawa kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana, nikianza na Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya TAMISEMI, kwa sababu wanaitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi wamezungumza habari za *TARURA*. Ni kweli *TARURA* ndiye mkombozi mkubwa kwa sekta ya uchukuzi na mawasiliano katika maeneo yote vijijini na asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge hapa tunatoka majimbo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie kuhusu *TARURA* kwa sababu kwanza kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema *TARURA* ina kilometra 108,946, lakini fedha wanayopata *TARURA* kwa mwaka wa 2021 ni shilingi bilioni 275.03, sawasawa na asilimia 35 tu ya uhitaji wa bajeti nzima ya *TARURA*. Ili *TARURA* iweze kusimama, lazima iwe na zaidi ya shilingi bilioni 700 ambapo tunaweza tukakarabati kilometra hizi 108,946. Kwa bahati mbaya sana, fedha zinazotolewa hadi sasa zimetolewa bilioni 172.85, sawa na asilimia 63 ya fedha zote bilioni 275 na bado kuna utofauti wa bilioni 102.8. Kwa vyovypote vile kwa hali ilivyo katika majimbo yetu mengi vijijini hayapitiki na ni mvua zinaponyesha sana kila sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niiombe sana Wizara, Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali nzima, ione umuhimu wa kuongeza fedha katika sekta hii ya *TARURA*. Watendaji wake wote wanafanya kazi nzuri sana akiwemo *CEO* wao pamoja na watendaji wengine, licha ya kwamba kuna upungufu mdogomdogo ambayo mimi naweza nikayasema. Kwa mfano, maamuzi mengi yanafanyika mikoani, tunatamani ifanyike *transformation TARURA*,

kwamba badala ya maamuzi mengi kufanyika mikoani, basi yafanyike ngazi ya halmashauri, ngazi ya wilaya ambako ndiko wataalam wapo. Kwa sababu sasa hivi barabara nyingi zinaharibika vijijini, lakini anayefanya maamuzi yuko mkoani ambapo mkoani kule barabara ni nzuri. Kwa hiyo kunakuwa kuna *delaying technique* ya kufanya barabara hizi zisitengenezeke kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano rahisi tu ni Jimbo langu la Busokelo. Busokelo kule mvua tunapata kwa mwaka mzima, zaidi ya milimita 2,000 kila mwaka, tunapumzika mwezi Septemba pekee. Ukipumzika mwezi Septemba tafsiri yake bajeti tunazopitisha hapa Bungeni, tarehe Mosi, Julai zinatakiwa zianze kutangazwa tenda, lakini zinakuja kutangazwa mpaka mwezi Novemba ama Desemba. Kwa hiyo utakuta kipindi cha kufanya *procurement system* zozote zinakuwa ni muda mrefu sana na wakati utekelezaji wake unakuwa kipindi cha masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana mara tu Bunge likipitisha fedha za Serikali, manunuvi yaanze mara moja badala ya kusubiri kufikia mwezi Desemba ama Januari ambapo barabara nyingi zinakuwa zimeharibika na zinakuwa zimekata mawasiliano katika kata mbalimbali, kitu ambacho hakikubaliki kwa ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia *TARURA* unazungumzia pia mifumo inayotumika katika manunuvi. Kuna Mfumo mmoja unaitwa *TANePS*, huu mfumo umekuwa ni changamoto kubwa sana, unasimamiwa na *TCRA*. Unaweza ukasajili wewe mkandarasi ama *Engineers* ambao wanakuwa kwenye huo mfumo, lakini matokeo yake baadhi ya *passwords*, tenda na *documents* kwenye huo mfumo, zinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utakuta inachukua muda mrefu sana mpaka tena huo mfumo usimame ili kuweza ku-*process* manunuvi hayo. Kwa hiyo nitoe wito na ushauri kwa Serikali kwamba kama inawezekana huu mfumo uweze kuwa *revised* badala ya jinsi ulivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara moja kwa wastani ni kati ya shilingi milioni 25 mpaka milioni 30, lakini kwa sasa barabara moja ya *TARURA* inatengenezwa kwa shilingi 2,524,461 kwa kilometa, hiyo ni shilingi lakini kwa kilometa moja. Wakati wenzetu wa *Road Fund* kupitia *TANROADS* wao ni zaidi ya fedha hizi. Kwa vyovyyote barabara zetu hazitawenza kutengenezeka vyema kwa uwiano huu ambao tuko nao mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa liliopo hapa tuna kitu tunaita *data backlog maintenance*, maana yake inahitaji barabara nydingi zitengenezwe kipindi cha mvua, kitu ambacho siyo rahisi. Kwa hiyo inabidi zitengenezwe kipindi ambacho siyo cha mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia *TARURA* hii kuna asilimia 30 ambazo Waheshimiwa Wabunge inawezekana wengi tunafahamu, wengine hatufahamu, ambazo ni maalum kwa vikundi, tunaita *special groups*, maana yake vijana, wenye ulemavu, wazee na wanawake ambayo kila bajeti ya *TARURA* lazima kuwe na asilimia hizo 30, lakini ni hal mashauri chache sana zinazotenga fedha hizi ili kuvizeshesha hivyo vikundi kupata fedha, lakini si tu kupata fedha, vifanye kazi za *TARURA* kwa asilimia 30. Kwa hiyo nisisitiza kwa Mheshimiwa Waziri kwamba hili pia ni muhimu kulisimamia katika Wizara yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ina mifumo mingi sana. Nilikuwa naorodhesha mifumo hapa, iko zaidi ya mifumo 14 na mifumo yote hii inaisaidia TAMISEMI. Hata hivyo, mifumo hii haitakuwa na maana sana kama gharama za kiuendeshaji zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niishauri Wizara kwamba kuna haja ya kupunguza mifumo ambayo iko TAMISEMI na wakati mwingine inakuwa ni *redundant* kwa maana kwamba mingine haifanyi kazi ipasavyo. Kuna kila sababu ya kuanzisha mfumo ambao uta-*integrate* na hii mifumo iongee, iwasiliane, ndipo tutakapoona haja ya kuwa

na mifumo hii. Kwa hivi sasa ilivyo ni mifumo mingi sana na inatengeneza gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza habari za *TARURA*, wamezungumza habari za malipo kuchelewa, wamezungumza habari nyingi, lakini tukiwa na mfumo mmoja ambao huo utakuwa chini ya *Kitengo cha Monitoring and Evaluation*, maana yake *M&E* ambao kila bajeti tunazopitisha hapa utakuwa na *component* ya kila mradi.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge popote utakapokuwa, awe kiongozi yeote ngazi ya wilaya ama mkoa ama Taifa, una uwezo wa ku-trace back mradi wako na hata ukajua *progress*, ukajua kama bajeti imetolewa ama hajijatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hatuna mifumo hii ndiyo maana *CAG* anapokuja na taarifa zake utakuta fedha nyingi zimeshapotea wakati tulikuwa na uwezo wa kufanya *monitoring and evaluation* kwa maana ya ufuatilaji na tathmini kabla fedha hizi hazijatolewa. Nitoe wito, kwa sababu *monitoring and evaluation* kila mradi ukiwa nayo, hakika tutafikia malengo yetu kama Wabunge. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere, kengele ya pili imeshagonga kwa hiyo muda wake wa kuchangia umekwisha.

Ahsante sana Mheshimiwa Fredy Mwakibete.

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Flatei Gregory Masei ajiandae.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi siku ya leo kuweza kuchangia katika bajeti hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Waziri na Manaibu wake kwa kupata nafasi ya kuongoza Wizara hii nyeti katika Taifa letu, Wizara ambayo inatazamwa na Watanzania karibu asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja za msingi ambazo nataka nichangie. Kuhusu *TARURA*; fedha inazopata ni ndogo sana, tunaiomba Wizara longeze fedha kwenye *TARURA* na ikiwezekana tuangalie kama tunaweza kuiwezesha, *of course* tunatambua *TANROADS* wanapata asilimia 60 mpaka 70 na *TARURA* wanapata asilimia ndogo ambazo zinaweza kuwafanya wakatengeneza barabara chache huku wakiwa na mtandao mkubwa wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe Wizara iliangularie kwa jicho la tatu. Ikiwezekana, kama hatuwezi kupata fedha za ndani, basi angalau tuangalie hata fedha za nje, tuweze kuboresha kuongeza Mfuko huu wa Fedha. Mfano mdogo nikichukulia Wilaya yetu ya Igunga, tunapewa fedha bilioni moja kama na milioni 200. Wilaya ina majimbo mawili, jimbo langu peke yake madaraja ambayo yanahitaji kujengwa ni zaidi ya manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Daraja Ia Mto Manonga pale kwenye Kijiji cha Mondu; kuna Daraja la Mazila kule kama unakwenda Buhekela kwenda kuunga Uyui, kule kuna madaraja matatu. Kila daraja moja linagharimu milioni 300 mpaka 500. Hapa kwenye haya madaraja manne ni zaidi ya bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukisema tukatengeneze madaraja haya, hatuna bajeti ya kutengeneza barabara za mitaa. Hata tukienda kutengeneza barabara kuunganisha wilaya yetu na wilaya zingine, madaraja ndiyo kiunganishi cha barabara hizi tunazozitengeneza. Sasa tuiombe Wizara iongeze fedha kwa TARURA, lakini pia ituongezee fedha katika Wilaya yetu ya Igunga kwa ajili ya kujenga Madaraja kama ya Mondo, Ncheli, Mazila kule Buhekela na Madoke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe pia TAMISEMI waangalie utendaji kazi wa TARURA wenyewe. Hata kama fedha tunazipata, lakini bado wanapaswa kuwasimamia kwa karibu katika kuleta tija na ufanisi wa kazi zao. Hata kama ni fedha ndogo lakini bado usimamizi unatakiwa uwe wa hali ya juu. Wakiachwa wakajiendea wenyewe kazi na hizi fedha tunazowapa hatutaona tija ya fedha wanazozipata. Kwa hiyo niombe wasogeze jicho kwa ukaribu kuweza kuwaangalia namna gani wanaweza *ku-perform* katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta nyiningine ambayo nataka kuchangia leo ni sekta ya elimu. Jimbo langu ni jipya na Mheshimiwa Waziri anatambua niliingia mwaka 2015, nilianza na ujenzi wa sekondari, kata nane hazikuwa na sekondari. Nimeweza kufanikisha kujenga kwa nguvukazi ya sisi na wananchi, angalau tuna madarasa mawili mawili. Nimefurahi kuona kwenye bajeti hapa imetengwa fedha, milioni 700, kujenga sekondari kwenye kila kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nimwombe Mheshimiwa asije na ile programu ya kugawa kila halmashauri watoe mara shule mbilimbili, tatutatu au waje kama vile walivyofanya kwenye sekta ya afya, wanatoa zahanati tatutatu. Wakija na hiyo programu tutaathirika wengine kwa sababu mzigo tulionao ni mkubwa, hatufanani kwenye ujenzi wa sekondari za kata; kuna wengine wamekamilisha na wengine hatujakamilisha. Kwa hiyo waangalie uwiano wa kugawa fedha katika hizi shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nilimsikia Mheshimiwa Mbunge wa Dar es Salaam alisema, wao Dar es Salaam hawahitaji mbegu kwa sababu hawana mashamba. Kwa hiyo huwezi kuniambia utagawa shule kila mkoa, kila hal mashauri, kwa sababu kuna maeneo mengine wana shule mpaka za maghorofa, kwa hiyo ukiwapelekea ni kama vile unawaongeza tu mzigo na hela ambazo hazina kazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watuletée kwenye mahitaji kama kwetu ambako watu wanataka fedha hizi tujenge hizi shule. Mfano, tumejenga Shule za Sekondari Buhekela, Manonga, Mwamala, Tambarale, Ugaka; tumejenga Shule ya Sekondari imepewa jina la Seif Gulamali, tumejenga Shule ya Sekondari Borogero, ni shule mpya. Tunaomba fedha hizo walizotenga watupatie tuweze kuzikamilisha na wananchi wale wa vijiji wahisi kwamba na wao wana haki sawa kama vile watu wengine ambao wanapewa migao ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia pia kwenye ujenzi wa mabweni. Hivyo hivyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, shule zetu vijana, watoto wa kike, wanatembea karibu kilometra tatu mpaka tano, mpaka kumi kufuata shule. Ukienda kuangalia kwenye kata zetu, tuna kata kubwa, tuna Kata inaitwa Mwashiku, kutoka kwenye kijiji kwenda kwenye shule ya kata mtoto wa kike anatembea umbali wa kilometra kumi, saba au tano, kufuata shule. Hivyo, wakituwekea bweni tutapunguza adha kwa mtoto wa kike kutembea...

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gulamali, kuna taarifa; Mheshimiwa Mbunge.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa na mimi ni Mbunge wa Jimbo la Igunga Mjini pale, ambaye ni Mbunge mwenzangu, kwenye

hizo kilometa kumi wanazotembea wanafunzi wakiwa wanakwenda shuleni, wanakutana na mito imeja maji na hakuna madaraja ambayo anasema Mheshimiwa. Kwa hiyo kama anavyosema Mheshimiwa kuhusu *TARURA* waongezewe fedha kuweza kujenga hayo madaraja, naomba kumpa taarifa hiyo Mheshimiwa. Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Kweli TAMISEMI kumekucha. (*Kicheko*)

Mimi mwenyewe nataka nimpe taarifa Mbunge, sasa hapo ndio mtihani; Mheshimiwa Gulamali, malizia mchango wako.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nimeipokea taarifa hiyo. Niseme tu, tupewe fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni haya, lakini itasaidia kuwaokoa watoto wa kike na mimba na uhai wao, lakini pia utawapa utulivu na kuweza kufaulu na wao kufikia malengo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la ajira katika sekta ya elimu. Wapo Walimu wanajitolea kufundisha katika hizi sekondari; hao wangepew kipaumbele cha kwanza. Mtu anafundisha mwaka mmoja, miaka miwili, miaka mitatu, zikija kutoka ajira wale wanakosa wanapata wengine ambao hata hawakuwahi kufikiria kujitolea. Kipaumbele cha kwanza wafikiriwe Walimu wanaojitolea kufundisha. Kwenye Wilaya ya Igunga wapo Walimu wa aina hiyo wengi sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri alichukue hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikumbushe katika sekta ya afya; alipokuja Waziri Mkuu jimboni, Kituo cha Afya cha Choma cha Nkola aliahidi kutupa milioni 300 kwa ajili ya kupanua majengo ya maabara, jengo la mama na mtoto na mambo mengineyo. Nikumbushe ahadi hii, TAMISEMI watupe hiyo fedha tuweze kujenga hayo mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alipopita Rais wakati akiomba kura, alisimama Ziba akawaambia wananchi nipeni

kura, mpeni kura Mbunge, wapeni kura Madiwani, hapa Ziba tutajenga kituo cha afya. Kwa hiyo niwakumbushe ahadi hizi za viongozi wetu wa Kitifa wasizisahau. Tunahitaji hizo fedha na tumeona wametenga fedha kwenye bajeti, kwa hiyo katika kupanga kwenu kupeleka fedha basi watupe Choma, Ziba, Kitangiri na Uswaya. Vituo hivi vya afya vitatusaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nipende kusema, pia Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. Magufuli, wakati anapita kwenye kampeni alisimama pale Ziba akawaambia wananchi wa Ziba na Igunga kwamba hapa Ziba panafananafanana kuwa na wilaya na mkitupa sisi tutawapa Wilaya.

Vilevile pia alipofika Nzega alisema hapa panafananafanana na mkoa. Tulikuwa tumeomba Mkoa wetu wa Tabora ndiyo mkoa mkubwa kuliko mikoa yote Tanzania, ukifuaatiwa na Mkoa wa Morogoro, mkoa wetu una zaidi ya *square meters* 75,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Igunga kwenda Tabora Mjini ni kilometra 200; tunaomba huo Mkoa; tunaomba watupatie Mkoa wa Manonga ambao Makao Makuu yatakuwa pale Nzega. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa atupatie huo mkoa ili tuweze kurahisisha huduma za wananchi, tusogeze huduma za wananchi karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata taarifa hivi karibu za Hati ya CAG natambua kuna maeneo ambayo yamezungumzwa sehemu mbali mbali katika Taifa hili. Lakini hata wilaya yetu ya Igunga imeguswa tumeona pale tumepewa hati chafu hii si sifa nzuri, na hii haipendezi, lakini niwaombe Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alivyopita alimtumbua yule Mkurugenzi. Ninamshukuru sana kwa kumtumbua yule lakini najua bado majibu yapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nakuomba TAMISEMI muangalie kwa macho manne manne mtumbue

sana. Mlete pale viongozi wengine, mlete wakurugenzi na wadau wengine, ninakushukuru kwa kunipa muda wako ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa...

MHE. SEIF KHAMIS S. GULAMALI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili niweze kuchangia katika wizara hii. Jambo la kwanza, kwanza nawapongeza sana, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri lakini pia Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wote kwa namna ambavyo wamekuwa wanaisimamia hii wizara na wanatekeleza majukumu yao. Hii ni moja ya wizara kubwa ambayo inagusa Maisha ya watanzania kila mahali. Kwa hiyo ni wizara ngumu lakini naamini mungu atakuwa pamoja na nyinyi ili muweze kufanikiwa na kufikia matarajio ya watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba nishauri kwasababu ya ukubwa wa hii wizara na kwa umuhimu wa Wizara ya TAMISEMI ni muhimu tufike mahali tuingie kwenye mikataba ya utendaji. Mikataba ya utendaji itatusaidia kwamba kila halmashauri sasa, halmashauri iangalie mapato ndani, iweke kipaumbele angalau kimoja au viwili kama ni kujenga kituo cha afya mwaka huu wanajenga kituo cha afya, kama ni kujenga ni shule wanajenga shule. Katika halmashauri zote hizo baada ya miaka mitano tutakuwa tumefika mbali sana. Kwa hiyo, nafikiri hili ni jambo la msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, *TARURA*, *TARURA* ni muhimu sana, *TARURA* ndiyo imebeba barabara mbalimbali zilizopo mijini na vijijini. Kwenye Jimbo langu la

Vwawa wananchi wa Jimbo la Vwawa ni wakulima, wakulima wa kahawa, wakulima wa mahindi wa mazao ya chakula na biashara na wanazalisha kweli kweli na ndio maana Mkoala wa Songwe Kitaifa unashika nafasi ya tatu kwenye uzalishaji wa chakula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili waweze kuendelea kuzalisha na huduma mbalimbali ziweze kuwafikia wakulima tunahitaji barabara zao ziimarishwe, zifike mpaka vijijini kule ili wale wananchi sasa waweze kupata pembejeo kwa wakati waweze kusafirisha mazao yao kwa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kufanya hilo barabara kama ile barabara ya kutoka lyula kwenda Idunda kwa muda mrefu imekuwa haipitiki. Wananchi wale wa Idunda kwasababu ya mvua nyangi daraja lilikatika barabara haipitiki wanakosa huduma mbalimbali naomba barabara hii iyangaliwe. Kuna barabara ya kutoka Ichenjezya kwenda Mbozi *Mission*. Kuna barabara ya kutoka Ichenjezya kwenda Msia hizi barabara ni muhimu sana kwasababu zinaenda katika maeneo ya uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna barabara ya kutoka Chimbuya, Ukwile kwenda Chizumbi pale kuna daraja kubwa lilikatika wananchi wale wanakuwa hawana mawasiliano kipindi cha mvua ni muhimu *TARURA* wakaongezewa fedha ili waweze kujenga haya madaraja, wajenge barabara hizi zipitike kwa wakati wote na tunaamini uzalishaji utakwenda vizuri sana katika hali kama hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nydingine ambayo inatoka njiapanda ya lyula inaenda mpaka lyula, ile barabara ni muhimu sana, sasa hivi imeharibika kabisa, utakuta kwamba wanashindwa kupeleka mbolea, wanashindwa kusafirisha kahawa, wanashindwa kupata huduma mbalimbali naomba hili nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nydingine ya kutoka Ihanda inaenda mpaka Ipunga pamoja na kwamba

imekarabatiwa bado kuna mambo hayajakaa vizuri katika eneo hilo. Kwa hiyo, ushauri wangu ni vizuri *TARURA* ikaongezewa mgao wa fedha, sasa hivi wanapata asilimia sijui 30, sijui 32 tukifika asilimia 40, *TANROADS* wakachukua asilimia 60 wale wakachukua 40 basi itasaidia sana katika kuweza kusimamia barabara mbalimbali zinazoenda katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu afya, nashukuru sana, naishukuru sana Serikali ilitupatia Mkoa wa Songwe kujenga Hospitali kubwa ya Rufaa ambayo inajengwa pale mpaka sasa hivi bado haijaanza. Naamini Serikali itachukua hatua kuhakikisha ile hospitali kubwa inaanza kufanya kazi. Lakini ile hospitali ni ya rufaa, tunahitaji tuwe na vituo vya afya, vituo vya afya katika Jimbo la Vwawa ambalo lina kata 18 tunavituo vya afya viwilli tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba Mheshimiwa Waziri ikikupendeza basi Kata kama ya Ihanda ambayo inawakazi wengi sana tupatiwe kituo cha afya. Katika lile eneo ili kiweze kuhudumia wananchi wa Ihanda lakini pia na wasafiri wengi ambao wanaenda mpaka Tunduma wanapovuka mipaka kukiwa na ajali watakuwa na uwezo wa kupata huduma katika lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Msia tunahitaji kituo cha afya lakini pale Hezya tunahitaji Kituo cha Afya, na Luanda tunahitaji Kituo cha Afya. Katika kipindi hiki tukiweza kupata Vituo vya Afya kama vinne au vitano vitatusaidia sana katika kuimarisha huduma za afya katika maeneo yale na mkipeleka na watumishi na madawa nina imani wananchi wa Jimbo la Vwawa wataendelea na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie kwenye upande wa elimu. Jimbo la Vwawa linashule za Sekondari zaidi ya 35. Tuna shule za msingi zaidi ya 90 katika Jimbo la Vwawa. Lakini shule za kidato cha tano ni chache, tulioomba katika kipindi kilichopita tukataka baadhi ya shule zipandishwe hadhi ili ziwe za kidato cha tano na ziweze

kuchukua wanafunzi. Na katika hilo Serikali ilitoa fedha kidogo za kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukapata Shule ya Msia, Shule ya Msia Sekondari ikapatiwa fedha kidogo kujenga madarasa. Shule ya Simbega Sekondari ikapatiwa fedha, lakini Mlangali ikapatiwa fedha yale majengo wananchi nao wakachangia matofali, wakachangia ujenzi wamejenga madarasa yamekamilika mpaka leo bado, bado zile shule hazijaanza kupokea wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Watoto wetu wanahitaji kwenda kidato cha tano sasa ni vizuri basi hizi shule zikasajiriwa na zikapokea wanafunzi wa kidato cha tano mwaka huu watakaotoka maeneo mbalimbali tutakuwa tumechangia sana katika kuendeleza elimu ya Watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia kuna watumishi wengi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ambao hawako katika mfumo wa malipo ya Serikali, wapo kwenye mikataba inakuwa ni mzigو mkubwa sana kwenye halmashauri na hii inatokana kwamba tulipoondoaa wale madereva ambao hawana vyeti na watu wengine Halmashauri imebaki haina baadhi ya watumishi ikalazimika kwenye ajira za ndani. Hebu Mheshimiwa Waziri lifanyieni hili kazi ili nalo liweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambao ningependa nichangie ni kuhusu Mkoa wa Songwe, Mkoa wa Songwe ni Mkoa wa mwisho kuanzishwa hapa Tanzania ni mkoa mchanga pamoja na uwezo mkubwa sana wa kiuchumi. Lakini mkoa huu bado unahudumiwa na Mamlaka ya Mji Mdogo hatuna Halmashauri ya Mji, hatuna Manispaa limekuwa ni ombi la muda mrefu, tumeomba angalau tupate Manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Manispaa vigezo vitakuwa havijafikia basi tuangalieni kwenye Halmashauri ya Mji ili Mkoa kama Mkoa uwe na halmashauri ya kuweza kuwahudumia lakini kwa hali ilivyo sasa hivi hali si nzuri.

Mheshimiwa Waziri naomba hili mlipe uzito ili angalau Mkoo wa Songwe tupate Halmashauri ya Mji ama Manispaa ya Mkoo wa Songwe itatusaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tumeomba, tulimuomba Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alipokuja tulimuomba eneo la kujenga soko, soko la mkakati, soko litakaoongeza mapato kwenye halmashauri. Akatukubalia lile eneo la kujenga soko likaanzishwa pale, ikatengwa eka hamsini pamoja na kujenga stendi ya Mkoo wa Songwe. Tunaomba haya yote yakapewe uzito unaostahili, mkayaweke katika mtazamo ili kusudi wananchi wale wa Jimbo la Vwawa wakaweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo la mwisho ambalo ningependa kuchangia katika siku ya leo ni kuhusu Wenyevitii wa Vitongoji na Mtaa. Hawa watu wanafanya kazi kubwa wanakutana na wananchi wanatatuwa kero nydingi wanashiriki kwenye maendeleo lakini hawana posho. Hebu wafikirieni hawa watendaji hawa itatusaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tuangalie Madiwani umefika wakati sasa Madiwani wawe na mshahara wa kudumu kuliko kutegemea kaposho. Wawe na wenyewe na mshahara hiyo itatusaidia sana kwasababu sisi Wabunge ili tuweze kufanya kazi tunawategemea sana Waheshimiwa Madiwani ili tuweze kushirikiana na kuchocheara maendeleo kila mahali. Kwa hiyo nakuomba Mheshimiwa Waziri liangalieni hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine mengi naamini Wizara ya TAMISEMI mtatekeleza majukumu yenu vizuri mtashirikiana, Wakurugenzi watatekeleza majukumu yao nchi hii itaweza kusogea mbele na tutaweza kufikia maendeleo yale ambayo tunayatarajia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kusema kwamba, naomba kuunga mkono hoja. Nawashukuru sana kwa nafasi, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo, Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza nianze kuwapongeza Wizara hii ya TAMISEMI, nimpongeze Mheshimiwa Ummy kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Dkt. Festo hongereni sana. Najua nyinyi ni wachapakazi na kwasababu tumeshafanyakazi kwa awamu, yaani miaka mitano iliyopita najua uchapakazi wenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si vibaya nikushukuru sana Mheshimiwa Ummy ulipokuwa Waziri wa Afya kwa kweli ulifanya kazi vizuri na najua utendaji wako wa kazi. Niishukuru pia Serikali kwa kunijengea Hospitali ya Halmashauri ambayo kimsingi haikuanza kazi ila kwa kweli imemalizika lakini yapo mambo machache ambayo tungependa yakamilike. Ziko fedha ambazo kimsingi zilishafika kwenye *account* za halmashauri lakini bahati mbaya sana fedha zile zimeondoka kutokana na kwamba muda wa bajeti ulishafika kwa hiyo, wakati wa mwaka mwingine fedha zikachukuliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe zile fedha zikirudi basi hospitali hiyo itakamilika na hatimaye kuanza kazi kwasababu ni hospitali hiyo tunaitegemea tu ya Halmashauri ya Mbulu. Na kwa hiyo, nishukuru sana lakini kingine nikushukuru pia kwa kituo cha afya cha Dongobeshi ni hicho kituo kimoja tu. Lakini ombi langu unajua unaposhukuriwa Mheshimiwa Waziri tuna *principal* za kushukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakristo kuna sala ya Baba Yetu tunasema Baba uliyе Mbinguni unamshukuru Mungu, unasema jina lako litukuzwe unamshukuru Mungu, unasema mapenzi yako yatimizwe unamshukuru Mungu lakini baadaye huyu Mungu unamuwekea ombi unasema utupe riziki za kila siku sasa Mungu anapenda sifa na anamjalia mja wake anapomuomba. Sasa nimekusifia na nyinyi mawaziri ili

haya maombi yapitie hii sala na mtume basi huko vijjini ili mambo yaende vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu ni kujengewa vituo vya afya, Mbulu vijjini kama Jimbo tuna kituo kimoja tu acha afya kama Mke wa Mkristo kwa hiyo maana yake ni huyo tu, Wadongobesh ndiyo kituo kimoja. Na sisi kama Halmashauri ya Jimbo la Mbulu Vijiini wananchi wamejenga Vituo vya Afya viro hatua mbalimbali; kuna Kituo cha Afya cha Getere ambao wameshazeeka kwa hiyo, tukipata fedha kidogo tunamalizia. Kuna kituo cha afya cha Maretadu na tuna zahanati nyingi tumeshajenga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ujue kwamba tukishajenga vituo hivi mkishatupatia zile fedha na sisi watumiaji wazuri wa fedha mkishatupa katika halmashauri yetu. Kuna Zahanati ya Galabadi, Zahanati ya Halsha, kuna Zahanati ya Hanaj na maboma mengine ambayo yapo kimsingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pia nishukuru umetupa fedha katika zahanati tatu nimeziona juzi. Lakini mkituungezea basi ni wazi kwamba kwa jimbo la Mbulu vijjini tunaweza kuihudumia wananchi wetu kwa afya zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara hii ya TAMISEMI saa hizi majimbo yetu ya vijjini yameanza kuwa na kata zake ni kubwa, kwa miaka zaidi mitano tunaenda mwaka wa sita hapajatokea kabisa ugawaji wa Vijiini na Vitongoji na Tarafa. Sasa niombe muangalie kwenye bajeti yenu ijayo muweze kutenga fedha za kugawa Vijiini na Vitongoji na Kata kwasababu zimekuwa kubwa sana hazitawaliki. Na sisi tuna Tarafa ambayo tunaiomba sana mara nyingi tunaleta maombi kwenye tuna Tarafa tunaiita ya Hedayachini kule kuna Wahadzabe eneo lao ni kubwa sana ina kilometra 245. Kwa hiyo, ni Tarafa ambayo kwa kweli ukiangalia tunahitaji jambo dogo tu kuwapatia ule uwezo wa kugawanya Tarafa hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na TARURA, umezungumza katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri

umeonyesha kwamba kuna jambo la ugatuaji wa madaraja *D by D* nitaizingatia sana. Lakini ni ngumu kwasababu moja kwenye Jimbo la Mbulu vijiji kwa sababu tu ya miundombinu ya barabara ambayo kimsingi haiwezi kwasababu kwanza *TARURA* pesa zake zinazopatikana ni kidogo sana, sisi kwa mara ya mwisho tumepewa milioni 671 na tuna barabara zetu zenye urefu wa kilometra 1,093.7. Kwa fedha hizi kwa kweli hatuwezi kujenga hizi barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo korofii ambayo kimsingi imekuwa na shida tunatakiwa tujenge madaraja kumi yenye jumla ya shilingi bilioni 11 hasa umepewa Milioni 66. Nimpongeze sana Meneja wangu wa *TARURA* wa Wilaya anajitahidi sana kufanya kazi na nishukuru umempa gari lakini shida iliyopo pale ni kwamba hakuna namna yoyote ya kujenga hizo barabara. Lakini nishukuru sasa pamoja na hayo yote nimeona kuna kama kamillioni kadhaa kameongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa niombe tumeweka madaraja yetu mfikirie namna ya kuyajenga kwasababu kuna shule kama saba sasahaziendeki kutokana na miundombinu. Kuna daraja la Masyeda, kuna daraja la Getere na Miodad hayawezi kabisa kupitisha wanafunzi na kwasababu mvua ikinyesha tu hizo shule tena hazifikiki kwasababu umbali ule na makorongo yamejaa. Kwa hiyo, naomba TAMISEMI wafikirie na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi tumeleta maombi ya kupandisha mji wetu wa Haydom kuita Manispaa aah na ni hii mji wa Haydom. Tumeleta maombi yetu na Mji wa Dongobesh tumeleta maombi tufikirie na hilo lakini mwisho kabisa najua dakika zimekwisha tuna ahadi za kilometra 5 ya mji wa Haydom, tuliahidiwa na viongozi wetu naomba tumejenga kilometra 1.8 naomba sasa tuweke fedha ili walau zile kilometra za ahadi za Mheshimiwa Rais ziweze kutimilizika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa nishukuru pia kwa utendaji wenu wa kazi lakini niwakumbushe

pia pamoja na wewe Mheshimiwa Ummy unakumbuka umefika Haydom na umefika Dongobesh zile ahadi zetu tulizoziweka pale ukonisaidie sana kuzitimiza na kwasababu umeingia TAMISEMI Mungu akubariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida Gallos atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Angelina Malembeka ajiandae.

MHE. TAUHIDA C. GALLOS Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuweza kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI. Nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake. Mheshimiwa Waziri dada yetu dada Ummy Mwalimu nikupongeze kwa nafasi hii uliyopewa ya Wizara hii ya TAMISEMI. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa tunakufahamu hatuna mashaka na uwezo wako tunaamini kwenye Wizara hii utatuvusha vizuri. Hatuna mashaka kwasababu hufanyi majaribio juu ya kazi hii tunajua umekuja kufanya kazi na utachapa kazi. Ikiwa sisi kama wenzio kuna baadhi ya mambo tukwambie ili uweze kuyafanyia kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri pamoja na pongezi lakini kwa sehemu lazima tukupe pole, pamoja na pongezi zote zilizo toka hapa kwa Wizara hii tukupe pole.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaendelea kukuombea unajua kwa sehemu kubwa wanawake wenzio ndani ya Bunge tunavyokuunga mkono. Tutaendelea kukuombea Mwenyezi Mungu akujalie, akutie nguvu, akupe ujasiri, uweze kuisaidia Taifa letu. Uweze kutuvusha kama wanawake, uweze kutuvusha kama wabunge wenzio tuweze kwenda salama kwenye eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya TAMISEMI ni kubwa na ina mambo mengi. Mheshimiwa Waziri kwanza kabisa nianze kwa kusema wizara hii pamoja na kazi nydingi inayofanya tunaomba mpate muda wa kufanya vipindi kwenye TV hususani wa kutoa elimu kwa wananchi. Wananchi wengi hawafahamu tafsiri ya Hati Chafu na Hati Safi, wengi wao wanatafsiri tofauti na ilivyo ndani ya tafsiri ya Hati Chafu na Hati Safi. Niombe ukipata fursa kama kutakuwa na vipindi andaeni vipindi vyta kuwaelewesha wananchi tafsiri za Hati Safi na Hati Chafu. Kwasababu tafsiri hii inaenda ni kitaalam zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanaposikia Halmashauri nydingine imepata Hati Chafu wakiamini kwamba kuna mambo mabaya, mabaya yaliyopitiliza lakini kuna baadhi ya Halmashauri zinapata Hati Safi iwaje ndani ya halmashauri hizo zina upigaji na miradi mibovu ambayo tunaishuhudia ndani ya macho yetu. Fursa hiyo tumeipata Wabunge kwasababu tunaenda kukagua miradi, wakati tunakwenda kukagua miradi tunakutana na Hati Safi ingawa halmashauri hiyo ina miradi mibovu na utekelezaji wa miradi ya wananchi ipo sifuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Waziri takribani wapigaji wote wana utalaamu wa kutengeneza hati safi kwasababu wanazifahamu zinapatikana viyi. Mheshimiwa Waziri tunaomba kwenye haya yafanyanyieni uchunguzi wa kina lakini wapeni taaluma ya kutosha wananchi wapate kujua tafsiri za Hati Safi na Hati Chafu. Watu ambao wanapata Hati Chafu wanakuaje na wanaopata Hati Safi inakuaje wakapata zile Hati. Hata sisi tunavyopangiwa Kamati kuna muda zilikuwa zinatupa shida kutafsiri hizi Hati, lakini kwa kuwa tunapewa elimu na taaluma ya kutafsiri hizi Hati huwa tunaelewa kazi zinakwendaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la asilimia 10 ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Waziri tunakuomba shughulika na hizi asilimia 10 za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hili ndiyo jibu la

Watanzania. Kama mikopo itatolewa ipasavyo, kama wanawake, vijana na wenyе mahitaji maalum watawezeshwa ipasavyo, Tanzania tutapiga hatua, Halmashauri zitasaidia viongozi wetu kufanya kazi vizuri. Mheshimiwa Waziri ana mambo na kazi nydingi, namshauri atenge vipaumbele aone ataivusha vipi Tanzania, afanye kazi kwa kumsaidia Rais wetu. Nashauri Waziri aweke vipaumbele kwamba ndani ya mwaka mmoja au miwili vitu gani anaweza akavifanyia kazi na vikaleta jibu ndani ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote nilizokaa ndani ya Bunge hili nimekuwa mjambe wa Kamati ya *LAAC*, sikuwahi kuona kuna jibu sahihi kuhusiana na asilimia 10. Pamoja na sheria tulioipitisha kwamba lazima kila halmashauri watenge fedha lakini bado jibu halipo. Halmashauri hazifikishi fedha kwa walengwa, fedha za mikopo ya wanawake, vijana na watu wenyе mahitaji maalumhaziendi ipasavyo. Naomba Wizara walichukue na waliangalie kwa jicho la kipekee ili liweze kufanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna jambo tofauti, kuna baadhi ya Wakuu wa Mikoa wanashindwa kuelewa kwamba wao ni sehemu ya zile halmashauri, wanadhani halmashauri ipo peke yake na wao wako peke yao. Kuna muda wanapoitwa utashangaa Mkuu wa Mkoanawaambia halmashauri wajibikeni wakati ule ni uwajibikaji wa pamoja, wanajihisi wao siyo sehemu ya zile Halmashauri. Kuna baadhi ya Wakuu wa Mikoa wanafurahi wanapoziona halmashauri zinafanya vibaya na kuzitia madoa wakati wao ni sehemu ya halmashauri zile kufanya vibaya. Kama utapata muda itisha mkutano wa pamoja, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, wajue wanaisimamia Serikali ndani ya mkoanapa swa kwenda pamoja kwa faida ya wananchi na siyo kujinu faisha wao na kutengeneza migogoro ndani ya mikoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie suala zima la elimu, Wabunge wengi wamechangia, liangalie lili vyokuwa la pekee, kila Mbunge anayesimama kwa namna yoyote ile

lazima ataigusa elimu. Kuna shule ndani ya Tanzania hii mwalimu yupo mmoja na tatizo ni dogo tu linaweza likapata ufumbuzi, kuna njia rahisi za kupata ufumbuzi. Kuna walimu unawapeleka Liwale, mwaka juzi nilichangia na hili nillilzungumza, unamchukua mwalimu wa Dar es Salaam, mtoto aliyezaliwa Dar es Salaam unampeleka Liwale anashindwa kufanya kazi lakini Liwale ileile kuna walimu wanaomba nafasi zile hawapewi nafasi za kufanya kazi na wapo tayari kusaidia Liwale, wapo tayari kusaidia eneo lao. Unamchukua mtoto wa Kahama unaenda kumpeleka Tanga akafanye kazi, uwezo wa kusema tunamtafutia nyumba hatuna, uwezo wa kusema tunamtafutia usafiri hatuna, unapomuacha kwao Shinyanga afanye kazi atakaa kwa mzee wake na kula ataisaidia Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itengeneze njia mbadala za kusaidia Serikali. Mheshimiwa Ummy Mwalimu kati ya watu nilliofurahishwa na hii nafasi uliyopewa mmoja mimi, naamini utachukua maoni yetu na kuyafanya kazi. Suala la kuwapangia walimu waende kwenye sehemu sahihi halihitaji fedha wala bajeti bali linahitaji mpango na mpango wenyewe ni rahisi. Mchukue watoto ndani ya mkoa husika wanaotaka kufanya kazi sehemu ile wapeni nafasi wafanye kazi, tuache mambo haya yanayoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la elimu, kero yangu nyingine kubwa inayonisumbua ni kuhusu vibali. Nadhani halmashauri ndizo zinazotoa vibali kwa nini mpaka leo Tanzania tunatoa vibali vyta kuanzisha *bar* na shule iko hapo hapo? Tunatengeneza nini? Tuangalie hatujengi watoto wa Tanzania bali tunawabomoa. Unapotaka kutoa kibali cha *bar* angalia mazingira husika, unampelekeaje mtoto *bar* na shule ipo hapo hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi/Vigelegele*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Angelina Malembeka atafuatiwa na

Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, umenisahau.

NAIBU SPIKA: Sawa, Mheshimiwa Abubakari Asenga atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka, Mheshimiwa Timotheo Mnzava ajiandae.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa kukumbukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy na Manaibu Mawaziri wake wote kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya na tunaendelea kuwashukuru sana kwa mchango wao kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe taarifa kuhusiana na wananchi wangu wa Jimbo la Kilombero ambapo jana kuna mvua zilinyesha na Mto wetu Lumemo ulijaa maji na maji mengine yakamwagwa kwenda kwa wananchi. Namshukuru Mheshimiwa Jenista kwa ushauri na msaada anaoendelea kutupatia kukabiliana na hali hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingi tumetoa hapa na michango mingi tunayotoa katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inataka kutumia tu pesa. Nina maoni kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara waangalie vipaumbele vya kuwekeza kwenye miradi mikakati ya kuzalisha mapato ya halmashauri. Watafute fedha katika bajeti yao wawekeze katika halmashauri ambazo zimeandika maandiko, zime-*qualify*, zina Hati Safi; kama Halmashauri ya Mji wa Ifakara wanasesma tukiwekeza bilioni tano katika soko

baada ya miaka miwili, mitatu zile fedha zitarudishwa kwa sababu Mji wa Ifaraka una biashara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunazungumzia mahitaji lakini wazo langu la kwanza la msingi nataka kuwaomba muwekeze. Kwa mfano, sisi tuna andiko letu kuhusu soko la Ifakara. Soko la Ifakara pale mjini mvua ikinyesha ni balaa tupu na linakusanya *millions of money* kwa siku. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunataka zahanati, hospitali na kadhalika lakini pia wanaweza kuweka vipaumbele katika kuchangia miradi mikakati kama vile stendi, soko na kadha wa kadha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, Mji wetu wa Ifakara una mitaa 33, nimeona kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri ameitaja ni zaidi ya mwaka mmoja mpaka sasa hivi hakuna Mtendaji wa Mtaa hata mmoja. Nimekaa na Wenyeviti wa Mitaa, barua imeandikwa na mimi nimekumbushia. Sasa Mheshimiwa Waziri kwa kweli mitaa 33 hauna Mtendaji wa Mtaa hata mmoja zaidi ya mwaka mmoja, Wenyeviti wanafanya kazi wenyewe, kwa kweli ni jambo ambalo linakarahisha. Tunaomba utusaidie na ile barua nitakuletea nakala unisaidie pamoja hizo posho za Wenyeviti wa Mitaa nazo wanalamika sana kwamba zinachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kubadilisha kanuni ya mikopo hii ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Sasa tumeambiwa watu watano, mwenye ulemavu mmoja anaweza kukopeshwa, hii ilikuwa changamoto kubwa sana kwa upende wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nalotaka kuchangia ni kuhusu *TARURA*. Kwa mfano, Jimbo langu la Kilombero ni wakulima wa mpunga na miwa, barabara zetu zote ili tuzimalize lazima tuchonge, tuweke kifusi, tushindilie. Zamani halmashauri yetu ilikuwa na vifaa vya kufanya kazi hizo, kwa sababu watu wa *TARURA* ni ma-*engineer*, kwa nini Wizara msione uwezekano wa kununua vifaa vinne tu wanaseme ma-*engineer*, wakivipata katika halmashauri na

wilayani hata dharura za ukarabati wa barabara zikitokea watafanya. Kwa mfano, Jimbo la Kilombero tuna milima ina vifusi kibao mpaka wilaya nyingine zinakuja kuchukua vifusi kutoka kwetu. Tupate *grader*, shindilia (*roller*), *excavator*, *tipper*; vifaa vinne tukipata kama halmashauri mwaka mzima tutaweza kutengeneza barabara zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba *TARURA*, najua imepata bajeti ndogo sana, kwa mfano kwetu sisi kuna shilingi milioni 454 haiwezi kufanya kazi ya jimbo zima. Pamoja na kuongezewa bajeti lakini tungewekeza hizo fedha, kwa mfano, tukitengewa *one billion* tukapewa *grader* na *excavator* tutatafuta hata *tipper* zitachukua kifusi zitakwenda kumwagia kwenye barabara za wananchi mwaka mzima tunafanya hiyo kazi, Mbunge unapewa fedha za Jimbo unaweza kununua mafuta ukaweka kwenye *grader* ukaenda ukachonga, ukaweka kwenye *tipper* ukaenda kumwaga kifusi wananchi wakaendelea kupata huduma za barabara. (*Makofi*)

Mji wa Ifaraka unakua kwa kasi sana kiasi kwamba Jumamosi na Jumapili benki hazifungwi. Tunaomba hawa *TARURA* watuwekee taa za barabarani, zile lami za Ifakara Mjini zina mashimo, tuongezewe lami kwa mfano barabara za Posta kwenda Hospitali ya *St. Francis*, CCM zamani kwenda kwa Salewa, naomba tuweze kuwekewa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kwenye *TARURA*, tunaishukuru Serikali tunajengewa na *TANROADS* barabara ya Kidatu kwenda Ifakara. Katikati ya barabara hizi kuna Stendi Kuu kwa mfano Mwaya, Kidatu na Ifaraka Mjini, barabara zile za kuunganisha kutoka barabara kubwa kwenda kwenye stendi zile au masoko ni za *TARURA*. Kwa hiyo, kwa sababu kuna mradi mkubwa lami wa kilometra 66.9 ambao utatuunganisha na Mkoa wa Morogoro, *TARURA* waunganishe stendi na hiyo barabara kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme jambo moja kubwa sana tunaomba Waziri atusaidie na hapa kweli nitamshika kidogo ushungi, ni kuhusu mgawanyo wa mali

katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara na Halmashauri ya Mji wa Mlimba. Sisi ni Wilaya ya Kilombero, tuna Jimbo la Mlimba na Jimbo la Kilombero. Jimbo la Kilombero lina Halmashauri ya Mji wa Ifakara na Jimbo la Mlimba lina Halmashauri ya Mji wa Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali paligawanywa mali Kata 9 za Mji wa Ifakara na Kata 26 za Jimbo la Kilombero. Baadaye Mheshimiwa Rais akatengua mgawanyo huo akaiongezea Halmashauri ya Mji wa Ifakara Kata 10 na Mlimba akaipunguzia ikabaki na Kata 16. Sasa mgawanyo ulifanyika wakati Halmashauri ya Mji wa Ifakara ina Kata 9, Makao Makuu ya Wilaya yote yale ya Halmashauri ya Ifakara ndiyo yalikuwa Makao Makuu ya Wilaya yana nyumba za Serikali, nyumba za taasisi, nyumba ya Mkuu wa Wilaya na ofisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelisema mara kadhaa hili tunaomba zile nyumba za Serikali ambazo ziko Ifakara zitumiwe na Halmashauri ya Mji wa Ifakara kwa sababu Halmashauri ya Mlimba ni mpya imeanza kujenga kila kitu na juzi Serikali imepeleka *one billion* kujenga makao makuu ya halmashauri mpya. Sasa hapa Halmashauri ya Mji wa Ifakara inabidi tuenze kuomba upya fedha Serikalini tujenge tena nyumba za Serikali na za Wakuu wa Idara. Hivi Mheshimiwa Waziri navoyozungumza TAKUKURU wamepangishiwa nyumba halmashauri, Mbunge nimetafuta ofisi ya vyumba viwili naambowi nyumba zote zinamiliikiwa na Halmashauri ya Mlimba wakati zipo Halmashauri ya Ifakara, imebidi nimuombe Mkuu wa Wilaya kanimegea kichumba ndiyo ofisi ya Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachokiomba chonde chonde kwa sababu mnapeleka fedha Mlimba, basi hii Halmashauri ya Mji wa Ifakara iweze kutazamwa vizuri na ipate hizi nyumba zote, zibadilishwe au zifanyiwe hata tathmini ikipatikana kama ni shilingi bilioni 2, 3, Halmashauri ya Mlimba wapewe fedha hizo sisi tupewe zile nyumba ziendelee kutumika kwa sababu sasa hivi zina popo na zimekuwa mapori wakati huo Mkurugenzi wa Ifaraka hana

nyumba; nyumba kagaiwa Halmashauri ya Mlimba ambayo ni kilometra 20 kutoka Ifakara. Hii ni Serikali moja lazima kwa kweli tujipange pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi ambalo naomba kuchangia ni michango ya elimu ya madawati na viti. Kule tunagombana na wananchi kwa sababu ukienda wana-*play video* ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli amemwita Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Elimu kawafokea Ikulu hataki michango ya shule. Tena ana-*play* kabisa anasema Mbunge wewe wa CCM umekuja, angalia Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli huyu, apumzike tu kwa amani, wanalalamika wanachangishwa wapeleke viti na meza wakati wamemsikia Mheshimiwa Rais anasema hataki michango na mwenye mchango apeleke kwa Mkurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu pamoja na kwamba hawana sekondari na wanataka sekondari, wanasema walau hii michango ingejuja wakati tunavuna mpunga sio Januari na Februari tunaenda kulima tunachangishwa tunaambiwa Sh.50,000, Sh.60,000 na lazima uje na kiti na meza. Mheshimiwa Waziri amesema atanunua madawati, atatusaidia madarasa, katika uongozi wake akiweza kutatua changamoto hii ya michango atakuwa ametusaidia kiasi kikubwa sana. Naomba utoke ufanuzi wananchi wanaruhusiwa kuchangia namna gani? Kama Serikali inasimamia ile elimu bila malipo tuambije wazi kwa sababu kuna mkanganyiko. Maelekezo ya Serikali yanatoka kwamba Februari ikifika wanafunzi wote waingine *form one*, Mkuu wa Wilaya hana bajeti, Mkuu wa Mkoa hana bajeti, anarudi kwa Wenyevitii wa Vijiji anaenda kuomba michango ambapo mwanakijiji mmoja akitoa anataka na wenzake wote watoto hata kama ana uwezo ama hana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu afya. Sisi Ifakara tuna hospitali ya *St. Francis*, ni hospitali ya *Mission*, Serikali itatuchukua muda mrefu sana hata kama tunajenga hospitali yetu kuifikia hospitali hii. Hospitali hii ina gharama kubwa, inahudumia Jimbo la

Mlimba, Ulanga, Malinyi, Kilombero na wakati mwingine mpaka Mikumi, zamani walikuwa wanapewa *OC* shilingi milioni 4 au 5, lakini sasa hivi imeshuka mpaka Sh.100,000. Umeme wanatumia shilingi milioni 10 kwa mwezi hawajapunguziwa. Tunaomba Serikali muiangalie hospitali ya *St. Francis* ili iweze kupunguza gharama wakati tunajenga hospitali yetu ya Jimbo. Jimbo letu lina Kata 19, tuna vituo vitatu vya afya, hivi navyozungumza Kituo cha Mang'ula wodi ya kina mama bado ina changamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Angelina Malembeka atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nichukue nafasi hiyo kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie na suala zima la utumishi kuhusiana na suala la uhamisho. Kumekuwa na tabia ya kuwaambia watumishi akatafute mtu wa kubadilishana naye. Kwa kweli kitendo kile mimi binafsi naona kwamba ni kumsumbuu mtumishi lakini pia kumfanya asifanye kazi zake. Mtu yuko Mwanza anataka kwenda Mtwara anaambiya akatafute mtu wa kubadilishana naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukulia mfano wa walimu ule muda ambao alitakiwa awe anafundisha inabidi atoke aende kwenye halmashauri kuangalia kama kuna mtu anayetaka kuja Mtwara na halmashauri nyingine zipo mbali na kituo cha mtumishi. Naomba Wizara iwe na mbinu mbadala, badala ya kumwambia mtumishi akamtafute mwenzie wa kubadilishana naye basi Wizara iangalie nani anataka kwenda Mtwara apelekwe na yule wa Mtwara

anayetaka kwenda Mwanza apelekwe badala ya jukumu lile kumuachia mtumishi mwenye ahangaike nalo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nizungumzie posho za Madiwani, imekuwa ni utaratibu kila Bunge tukija tunazungumzia posho za Madiwani. Wale ni wenzetu tunafanya nao kazi, tunapokuwa tunasema halafu hawatekelezewi tunaonekana pia Wabunge hatuna maana tuna ubaguzi. Naomba Wizara isimame kidete kushughulikia posho za Madiwani na ikiwezekana wawape mshahara maalum ijukane Diwani ana mshahara shilingi ngapi kwa mwezi halafu hizo posho aendelee kuchukua kutokana na vikao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu kuna vikao vya Madiwani vinafanyika hawapewi hata hiyo posho yenewe ya kikao, wanasema halmashauri haina fedha. Madiwani wanakopwa, wanakwenda kwenye vikao wengine wanatoka mbali nauli hawana, wanapata usumbufu lakini wapo chini zaidi kwa wananchi hata mwananchi akimwambia tunataka timu yetu ya kwenye mtaa tupate mpira fedha ya kununua mpira hana. Kwa nini tuisiwafikirie Madiwani ili na wao waweze kufanya kazi zao kwa umakini zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la uandikishaji wanafunzi wa darasa la kwanza. Halmashari nydingi zimeonesha kwamba zinaandikisha watoto wengi lakini ukifuatilia wanapofika mwisho ile idadi inapungua na inapungua kuanzia darasa la tano, la sita mpaka darasa la saba. Ukiangalia sababu kubwa ni utoro na mimba za utotonii au mimba zisizotarajiwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niziombe basi halmashauri ziweke mkakati wa dhati kati ya halmashauri na wazazi kuhakikisha wale watoto wanaoandikishwa wafike shule na ikibidi kama kushtaki basi na mzazi naye ashtakiwe. Kuna wazazi wanaojua kabisa mtoto wangu haendi shule na yeye yupo kimya, kama elimu imetolewa bure kwa nini halmashauri ziandikishe watoto 600 halafu mwisho wa siku watoto wako

200 hao wengine wamekwenda wapi? Ni lazima tujizatiti kuhakikisha kwamba wanafunzi walioandikishwa wamalize kama ilivyotarajiwa badala ya kuwa na sifa kwamba tumeandikisha watoto kadhaa lakini mwisho wa mwaka tunajikuta watoto wako kidogo kwa sababu ya utoro na mimba zisizotarajiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumzie suala la uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Zipo halmashauri zilizofanya vizuri lakini kuna halmashauri zingine hazitoi zile asilimia 10, wanajipangia wanavyotaka wao. Ukiangalia makusanyo yao ya mapato ya ndani hayalingani na zile pesa wanazozitoa. Ni vizuri suala hili lisimamiwe ili zile asilimia 10 zitolewe kama zilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika utoaji wa asilimia hizi haki itendeke kuna vikundi ambavyo viko ndani ya halmashauri havijawahi kupata mikopo hii.

TAARIFA

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hii kero ya asilimia 10 kwa halmashauri zote nchini Tanzania ili imalizike inatakiwa kuwepo na akaunti mbili benki; akaunti hiyo ya asilimia 10 na akaunti ya Halmashauri. Kila fedha ya halmashauri inayoingia kwenye akaunti ile asilimia 10 iende kwenye akaunti. Hilo ndiyo itakuwa suluhisho ya kero hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere huo ni ushauri kwa mchangiaji au ni taarifa kwa mchangiaji?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angelina Malembeka, malizia mchango wako.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Taarifa hiyo nimeipokea kwa mikono miwili kwa sababu inaleta tija kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgao huo huo wa asilimia 10 napenda kuongezea kwamba utaratibu ufanyike. Kwa sababu kuna Halmashauri ambazo unakuta kuna kikundi kinapata mara mbili mpaka mara tatu lakini kikundi kingine mpaka miaka mitano inapita hawapati. Kama wanakosea kufanya utaratibu mwafuate, mwaeleze jinsi gani wafanye ili na wao wapate ile mikopo. Badala ya kuwa wanaomba miaka yote hawapati lakini makundi mengine yanapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, pia ni vizuri basi Halmashauri zijipange tuone zile fedha za marejesho zinazorudishwa, ziko wapi na zinafanya nini? Isiwe kila mwaka wanapanga shilingi milioni tano, mwaka unaofuatia milioni tano, mwaka unaofuatia milioni tano, lakini zile zinazorudishwa hazionekani ziko wapi na zinafanya nini? Ni vizuri zionyeshwe na tujue zinafanya nini; kama zinaongezwa kwenye mikopo au zinafanya kazi nyininge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie pia suala zima la ukarabati wa shule kongwe na baadhi ya Vyuo vya Ualimu. Kazi imefanyaika nzuri sana, lakini hapa hoja yangu ni kwamba, tusiwe tunasubiri tu kukarabati shule kongwe na zile zilizopo ukarabati mdogo mdogo uwe unaendelea kufanyaika ili kuondoa madhara makubwa. Kwa sababu unapokuta labda jengo limebomoka mlango mmoja, siyo tunasubiri mpaka milango yote ivunjike na madirisha yote yavunjike, haitaleta tija. Ni vizuri hizo shule ambazo bado ni mpya lakini zimeanza kuonesha matatizo zianze kukarabatiwa mapema ili kuondoa athari kubwa kwa siku za baadaye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala zima la ukamilishaji wa maboma ya majengo

mbalimbali yaliyoanzishwa na wananchi. Wananchi waliitikia mwito wa kujitolea wakajenga nyumba mblimbali; kuna nyumba za walimu, zahanati, shule na vituo vy a afya. Sasa yale maboma kwanza yanawatia uchungu wananchi. Wameacha shughuli zao ku-support Serikali halafu Serikali mpaka sasahivi wanayatazama. Ni vizuri tujipange ili yale majengo yaliyoanzishwa na wananchi yakamilike ili waweze kuyatumia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ili niache fursa kwa wenzangu kuchangia, nizungumzie suala zima la mama wajawazito na watoto hususan kwenye vituo vy a afya. Kuna maeneo ambayo wanasema huduma hii inatolewa bure, lakini ukienda unakuta huduma hizo zinalipiwa kwa njia ya ujanja ujanja. Mtoto ana tatizo hili, anaambiwa chukua karatasi nenda kanunue kitu fulani. Mtoto ana tatizo hili, nenda kanunue dawa fulani, wakati hizo dawa wakati mwingine zinapatikana kwenye lile eneo na wazee wanafanyiwa mambo hayo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pia tujipange tuangalie jinsi gani ya kukamilisha hili zoezi bila kutia kero kwa wananchi kwa sababu kama tumekubaliana elimu bure, afya bure kwa wale ambao wana sifa za kupata wapate bure kweli. Siyo wanaenda pale wanalipishwa kumwona daktari na kadhalika, halafu na dawa zenyewe hawapati wanaambiwa wakanunue. Hiyo siiafiki, tujipange vizuri, Halmashauri zifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na afya yangu, leo naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujaalia uzima. Kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uteuzi

wa kuwa Waziri kwenye Wizara hii. Odo Ummey tuna imani kubwa sana nawe, tunaamini kwamba utaifanya kazi yako vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waheshimiwa Manaibu Waziri kwa kuendelea kuaminiwa, lakini pia najua mna timu nzuri sana TAMISEMI. Mmepata Katibu Mkuu mzuri, Profesa Shemdoe, mtu mahiri, mtu makini san ana pia anaye Naibu Katibu Mkuu kama ndugu yangu Ndugu Gerald Mweri, tuna uhakika na kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie muda huu kushauri mambo machache kwenye eneo la TAMISEMI. Jambo la kwanza ni upande wa TARURA. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu TARURA, nami naendelea kusema na tutaendelea kusema kwa sababu ni kitu muhimu sana kwenye maendeleo ya Halmashauri zetu hasa kwa sisi ambao tunatoka maeneo ya vijijini. TARURA inafanya kazi nzuri, lakini lazima tukubaliane kwamba ziko changamoto zinahitaji kufanyiwa kazi ili kazi hii nzuri inayofanywa na TARURA iweze kuwa na matokeo mazuri kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ya kwanza ni fedha. Tuseme tutakavyosema lakini pesa wanayopewa TARURA ni ndogo, wanahitaji kuongezewa fedha ili waifanye kazi yao vizuri. Jambo hili siyo kwa TAMISEMI tu, ni jambo la Serikali. Tunahitaji Serikali itusikie kwamba tunahitaji kuona TARURA ikiongezewa fedha iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hoja ya baadhi ya watu wakihoji kwa nini TARURA au barabara zimetolewa Halmashauri na TARURA imesimama yenye we inajitegemea? Kwa upande wangu, kuirudisha TARURA Halmashauri ni kurudi hatua moja nyuma na wala siwezi kushauri jambo hilo. Ninachokionba hapa kifanyike kuwe na mahusiano mazuri kati ya Halmashauri ya TARURA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani ndio waliokwenda kuomba kura, ndio tunaojua

mahitaji ya wananchi, ndio tunaojua vipaumbele vya watu wetu. Lazima *TARURA* watushirikishe Halmashauri zetu kwenye kuteua barabara za kufanya matengenezo. Isiwe hisani kwamba akijisikia aseme, asipojisikia asiseme. Watushirikishe tushauriane ili twende tukaangalie maeneo kulingana na mahitaji na vipaumbele vya watu wetu kwenye Halmashauri zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako ukurasa wa 118 nimeona unazungumzia mradi wa barabara kwenye maeneo ya uzalishaji hasa kwa maeneo ya kilimo. Umeongelea eneo la kule nyanda za juu kusini peke yake. Yako maeneo mengi ya uzalishaji ambayo yana shida kubwa ya barabara. Katika Mkoa wa Tanga, milima ya Usambara ni maeneo muhimu sana hasa kwa kilimo cha chai. Barabara ni mbovu sana, tunahitaji miradi ya namna hii ifike kwenye maeneo yale pia tuwasaldie wananchi. Tunapoteza chai nydingi sana ya wananchi wetu kwa sababu ya ubovu wa barabara, inachelewa kufika kiwandani, watu wetu wanapata hasara. Tunaomba sana mtusaidie kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Asenga ameshauri hapa kuhusu vifaa, hata kama siyo kwenye *level* ya Halmashauri, basi hata kwenye *level* ya mkoa angalau *TARURA* kwenye ngazi ya mkoa kuwe na vifaa. Haiwezekani tukipata dharura tuanze kuhangaika kukopa kwa Wakandarasi na mkiwakosa wananchi wapate hasara. Angalau kila mkoa basi kuwe na vifaa, ikitokea dharura wafanye kazi kwa kutumia wataalam tuliokuwanao kwenye *TARURA* kwa vifaa walivyokuwa navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 Serikali ilitoa maelekezo ya kuhamisha Halmashauri zote ambazo walikuwa wanafanya kazi kwenye maeneo ambayo ni nje ya maeneo yao ya utawala kwenda kwenye maeneo yao ya utawala. Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ni moja ya Halmashauri ambazo tulihamisha Makao Makuu ya Halmashauri yetu, lakini tuna changamoto kubwa sana ya usafiri kutoka kwenye Tarafa kwenda kwenye Makao Makuu ya Halmashauri mpya

tuliyopeleka sasa. Naomba mtusaidie *TARURA* wawe na programu maalum ya barabara za kuunganisha angalau Tarafa na Makao Makuu hizi mpya za Halmashauri ili wananchi wetu waweze kufika vizuri na kwa urahisi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kwenye upande wa afya. Tunaishukuru Serikali, imefanya kazi nzuri na kazi kubwa sana kwenye Sekta ya Afya. Korogwe tumepata Hospitali ya Wilaya, tumepata Kituo cha Afya cha Mkumbara na sasa tunajenga Kituo cha Afya cha Kerenge, lakini kuna vituo vya afya vikongwe vya muda mrefu. Ninacho Kituo cha Afya kule Korogwe cha Bungu kimejengwa mwaka 1977 mpaka leo hakijawahi kufanyiwa ukarabati, hakina huduma ya upasuaji, kutoka huko kwenda Hospitali ya Wilaya ni zaidi ya kilometa 55. Naomba pamoja na kazi nzuri mnayoifanya tuangalle maeneo haya, tusogeze huduma, tuboreshe vituo hivi vikongwe viweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko ahadi za viongozi. Waziri Mkuu alipita Korogwe akaahidi kusaidia ukarabati wa Kituo cha Afya cha Bungu. Aliahidi Kituo kipyaa cha Afya kule Mashewa, tunaomba ahadi za viongozi zikatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 kwenye bajeti ya TAMISEMI nilisema na mwaka huu narudia tena, hamtutendei haki kwa namna mnavyogawa hizi rasilimali tulizokuwa nazo. Huyu ndugu yangu wa Korogwe Mjini hapa ana viji 34 na vitongoji jumla 34, mimi nina viji 118; ana shule za Msingi 34, mimi nina shule 138; unaposema kila wilaya au kila jimbo lipewe maboma tisa, hamtutendei haki. Sisi wengine tunaumia, tuna maeneo makubwa. Hata kama ni kigezo cha watu, pia tuna watu wengi. Tumefuatilia kwenye hizo Halmashauri nyingine, hawana watu wengi namna hiyo. Tunaomba mtuangalle sisi ambao tuna maeneo makubwa, tunaumia Zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi hasa kwa upande wa Halmashauri za vijiini. Halmashauri za vijiini zimekuwa ni maeneo ya watu kwenda

kuanza kazi na kuondoka kwenda kwenye maeneo mengine mazuri wanayoyataka wao. Sekta ya Afya na Sekta ya Elimu tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Naomba mtusaidie kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawaomba TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, hebu tuweke utaratibu mzuri wa mtu kuhama kutoka kwenye Halmashauri moja kwenda kwenye Halmashauri nyingine. Hii tabia kila mtu akitaka kuhama anaandika moja kwa moja, inakuja kutoka Wizarani amehamishwa, mnatuumiza. Tuna shule zina walimu watatu, kuna zahanati ina mtumishi mmoja au wawili, tunawaomba mtusaidie kupunguza changamoto hii ya watumishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshauri Mheshimiwa Waziri kwenye eneo la kusimamia mamlaka ya Serikali za Mitaa. Tuna ripoti ya CAG imetoka juzi; moja ya maeneo ambayo hatukufanya vizuri ni kwenye Halmashauri. Namwomba sana dada yangu, hatafanya kazi yake vizuri TAMISEMI kwa kukimbizana kwenye ziara katika kila Halmashauri. Kwa siku uende Halmashauri tatu au nne, hakuna kitakachofanyika kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, imarisheni sekretarieti za mikoa ili ziwasaidie kuzisimamia Halmashauri. Katibu Tawala wa Mkoa ajue ana jukumu la kusimamia Halmashauri na Mkurugenzi ajue kwamba ye ye *immediate boss* wake ni Katibu Tawala wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkao ajue kwamba Halmashauri ikiharibu, naye hatabaki salama. Tuna sekta zote, tuna idara zote pale kwenye Sekretarieti ya Mkao, zinafanya nini? Kwa nini mpaka tusubiri Waziri au Katibu Mkuu aje? Tuimarishe Sekretarieti za Mikoa zikusaidie wewe na Katibu Mkuu kuzisimamia Halmashauri zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuimarisha Sekretarieti za Mikoa, tunacho kitengo cha ukaguzi wa ndani kwenye Halmashauri zetu. Mimi naomba TAMISEMI mtafakari upya namna ya kufanya kazi na kusimamia hiki kitengo vizuri.

Mambo yote anayoyasema CAG kwenye Taarifa zake siyo mapya. Wakaguzi wa ndani wameshayaibua kwenye Halmashauri zetu, lakini mwisho wa taarifa ya Mkaguzi wa Ndani ni nini? Hatua za taarifa za Mkaguzi wa Ndani zinachukuliwa na nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja ya kukiimarisha hiki kitengo sambamba na kuwajengea uwezo Madiwani wetu kwenye Kamati za Fedha na kwenye Mabaraza ya Madiwani kuzifanyia kazi vizuri taarifa za Wakaguzi wa Ndani ili mambo yaweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niwaombe, tunazo sheria; hebu TAMISEMI fanyeni kazi ya kupitia sheria. Ziko baadhi ya sheria zinatusababishia kupoteza mapato kwenye Halmashauri zetu. Leo tunapozungumza sisi watu wa Korogwe na watu wa kule Nyanda za Juu Kusini, kuna mgogoro mkubwa sana kwenye kupata ushuru wa mazao kwenye zao la chai, lakini shida ni sheria tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuziangalia sheria, lakini pamoja na sheria hiyo, iko changamoto nydingine kwamba kampuni inafanya kazi kwenye Halmashauri lakini Makao yake Makuu yako kwenye Halmashauri nydingine.

Kwa hiyo, kwenye kupata *Service Levy* tunakuwa na mgogoro mkubwa sana. Tunaomba TAMISEMI mtusaidie kutoa mwongozo wa namna ya kwenda na vitu kama hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna imani na Mheshimiwa Waziri kwamba wataifanya kazi hii vizuri. Tuna imani nanyi kuwa mambo yanakwenda kukaa sawa sawa. Tunachowaomba, tusaidieni kuzisimamia Halmashauri zetu vizuri. Tusaidieni kuwaimarisha *TARURA*, tusaidieni kuimarisha Idara ya Afya kwenye Halmashauri ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Selemani Zedi ajienda.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa machache niliyonayo kwenye Wizara hii muhimu ambayo inakwenda kuwashumia Watanzania walio wengi. Kwa kuanza, nami naomba niungane na wenzangu kwenye suala zima la *TARURA*. Kwenye suala zima la *TARURA* nitaomba niende kwenye muktadha tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitisha hapa hii taasisi ya *TARURA*, mwaka 2017, Serikali ilituhakikishia kwenda kutoa ushirikiano wa kutosha kwa watumishi wetu ili waende wakatimize wajibu na majukumu yao kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Hata hivyo, ninapata kigugumizi na sijui ni kwa nini? Serikali baada ya kuletewa *TARURA* ikatoa watumishi, wahandisi (*engineers*) waliokuwa kwenye Halmashauri ikawapandisha na kuwapa nafasi mbalimbali; Meneja wa Wilaya, Meneja wa Mikoa na Wakurugenzi. Baada ya kuwakabidhi majukumu hayo, watu hawa tunavyoongea mpaka leo hii, muda huu nimesimama, dakika hizi ninazoongea, watu hawa kuanzia Meneja wa Wilaya, Meneja wa Mikoa na Wakurugenzi wote, miaka minne kasoro hakuna hata mtu mmoja mwenye barua ya kuthibitishwa kazini kwenye nafasi hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu watu hawa wana barua za kukaimu. Wanakaimu miaka minne kasoro, lakini Serikali mpo, halafu ni Ofisi ya Rais, ambayo inakwenda kuhudumia Watanzania walio wengi kwenye Sekta muhimu inayokuza uchumi wa Taifa letu kutokana na kilimo! Mtu ambaye amethibitishwa kazini ni mtu mmoja tu, Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA*, baba yangu Victor ndiye amethibitishwa kazini. Mtu ambaye alifanya kazi hii kwenye Taifa letu na ninatambua mchango wake mkubwa, amelitumikia Taifa lake, akastaafu, lakini akarudishwa tena kwa mkataba, yeye ndio mwenye barua ya kuthibitishwa kazini, wenzake wote wana barua za kukaimu mpaka leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Ummy, nakuamini katika uwajibikaji na uchapaji kazi. Kama tunataka kuwasaidia Watanzania na kukuza uchumi wa Taifa letu na watumishi wetu waweze kufanya kazi vizuri kwenye taasisi hii, naomba ukitoka hapa, kesho tunahitimisha bajeti yako, nenda kaanze na suala zima la kuhakikisha watumishi wetu wote wa ngazi ya Wilaya na Mkoa, Wakurugenzi wapate barua zao za kuthibitishwa kazini. Kama mnaona hawafai, waondoeni, tafuteni watu wanaofaa, wapeni mamlaka waweze kufanya kazi. Siyo kuwakaimisha watu miaka minne, ni kitu ambacho hakiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazokwenda kutokana na kukaimisha watu hawa na kutokuwa na mamlaka ya kwenda kutimiza wajibu na majukumu yao ripoti ya CAG inatuambia kutokana na udhaifu huo, *TARURA* kwa miaka mitatu mfululizo, nitaisema miili tu mfululizo, imebaki na bakaa. Yaani fedha ambazo zimebaki bila kwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019 *TARURA* walibaki na bakaa ya shilingi bilioni 72.3 ambazo leo Wabunge tunapiga kelele humu ndani zingeweza kwenda kufanya kazi. Hakuna mtu wa kufanya maamuzi, yuko mtu mmoja pale, kazi zimelala, fedha zinarudi, halafu bado sijui tunataka kufanya nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019/2020 shilingi bilioni 1.5 ziko pale, zimerudi. Barabara tunalalamika, miundombinu ni mibovu, wananchi wanakuwa barabarani kwa kukosa huduma za barabara, akina mama wajawazito wanashindwa kwenda kujifungua watoto wao, wanajifungulia barabarani kwa sababu tu ya jambo dogo ambalo tunatakiwa tulisimamie ili watu wetu waweze kupata hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu twende tukafanye hii kazi ya kwenda kuwathibitisha hawa watu kazini ili tuweze kufanya kazi ya kulijenga Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala zima la posho za Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Vijiji. Tuna chaguzi mbili; tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu. Madiwani tunafanya nao uchaguzi pamoja. Tukija kwenye suala la malipo tunawabagua Madiwani wakalipwe na Halmashauri kwenye mapato ya ndani, wakati watu hawa ndio tunaokwenda nao katika uchaguzi wetu. Ni kitu gani kinachosababisha Madiwani wetu wasiwekwe kwenye mfumo wa Serikali wa kulipwa mishahara yao na posho zao ili waweze kutimiza wajibu na majukumu yao? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani leo ndio watendaji wetu wakuu kule chini. Sasa hivi tuko humu Bungeni, vikao vya Mabaraza ya Madiwani vinaendelea kule. Wao ndio wanaojua nini kinachoendelea kwenye kata zao, lakini watu hawa hawathaminiwi, tumewasahau. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali, tuone ni namna gani tunawatoa Madiwani wetu kuwaleta kwenye Serikali Kuu; mishahara walipwe na Serikali Kuu na vikao vyao pia vigharamiwe na Serikali Kuu ili tuachane na biashara ya kuendelea kuwakopa Madiwani kila mwaka na kila vikao na vikao vingine havifanyiki kwa sababu Wakurugenzi wanakuwa na kigezo cha kwamba hakuna fedha, kwa hiyo, siwezi kuitisha baraza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la Wenyeviti wetu wa Vijiji, Mitaa pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe. Watu hawa nao pia ni watu ambao wanafanya kazi kubwa sana. Tukae tukijua Wenyeviti wa Vijiji pia ndio wanaoishi huko na ardhi zetu za vijiji ambavyo leo vimekuwa na migogoro mikubwa, chanzo kikubwa pia ni Wenyeviti wetu wa Vijiji kwa sababu hawana chochote mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanakwenda kule wanatafuta ardhi na Mwenyekiti akiambiwa bwana, Mwenyekiti mimi nina shilingi 50,000 hapa, wewe nikatie hapa kidogo tu. Mwenyekiti anaona sasa hii shilingi 50,000 wakati wewe umenisahau, nifanye nini? Anamkatia eneo pale, anachukua shilingi 50,000 yake, maisha mengine

yanaendelea, tunakuja kurudi kwenye timbwili la kuanza kusuluhiha migogoro kwamba mimi nilipewa na Mwenyekiti wa Kijiji, huyu anasema hii ilikuwa ni hifadhi, huyu anasema vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Wajumbe wa Vijiji pamoja na Mitaa, watu hawa tukiwatoa Madiwani wakaenda Serikali Kuu, tuwarudishe Wenyeviti wetu wa Vijiji walipwe na Halmashauri kwa sababu tunakuwa tumeipunguzia Halmashauri mzigo wa kulipa Madiwani na hivyo waende wakaanze kuwalipa Wenyeviti wetu wa Vijiji kupitia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la ahadi ya shilingi milioni 50 kila Kijiji. Uchaguzi wa mwaka 2015 kwenye llani ya Chama cha Mpainduzi mliwaahidi Watanzania kuwapatia shillingi milioni 50 kila kijiji ili waweze kukuza uchumi kwenye maeneo yao.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

TAARIFA

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ahadi iliyotolewa ilikuwa ya mwaka 2015 – 2020, nasi tulienda tukawaeleza wananchi juu ya jambo hilo kwamba tulahirisha kufanya mambo mengine. Kwa hiyo, llani inayoteklezwa sasa ni 2020 - 2025. Kwa hiyo, hayo ya nyuma hayako kwenye *tender* hiyo sasa hivi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru naomba niendelee, nam-*ignore* tu Mheshimiwa

Getere. Nimefunga, kwa hiyo, naomba aniache tu nisije nikatengua swaumu yangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaahidi wananchi wetu shilingi milioni 50 kwa ajili ya kwenda kuhuisha uchumi wao kwenye maeneo yao, lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambaye ye ye ndiye anaye-dea/na vijiji vyetu, sijaiona hiyo milioni 50 humu. Nakumbuka mwaka 2017, nilichangia kwenye bajeti kuu ya Serikali na nikaambiwa...

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe Taarifa mzungumzaji anayeendelea kwamba, ahadi ya milioni 50 ya kwenye ilani ya mwaka 2015 ilitekelezwa kwa namna mbalimbali ikiwemo kupeleka mikopo kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri. Kwa sababu ya utekelezaji wa namna hiyo ndio maana wananchi walikiamini tena Chama Cha Mapinduzi kikashinda kwa kishindo kwenye uchaguzi wa mwaka 2020. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hizi ahadi kila ahadi ilikuwa inajitegemea. Waliahidi vituo vya afya, waliahidi maji kumtua mwanamke ndoo kichwani, waliahidi barabara ambazo wameshindwa kuwathibitisha hata watendaji wa *TARURA* na waliahidi milioni 50. Kwa hiyo, tunachokitaka nataka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI milioni 50 ya kila Kijiji ambayo ilani yao hiyo, kama watakuwa wanaandika ilani kila baada ya miaka mitano wanasema hii ilipita hatuwezi kutekeleza tunaanza na mpya, Waheshimiwa basi kwa kweli, tusiendelee kuwaibia Watanzania kwa style hii, lakini kama tunaendeleza yale yaliyokuwa yamebak...

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hii itakuwa Taarifa ya mwisho. Mheshimiwa Agness Mathew Marwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa Taarifa kwa muongeaji kwanza anatoa lugha ya maudhi, lakini kingine anatakiwa ajue kwamba, mpaka sasa hivi muda bado. Mama atayatekeleza yote, kwa hiyo, aache kashfa. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti malizia sekunde zako chache zilizobaki.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikushukuru. Hata ninyi wenye mmepteana huko, yaani hamjui nini ambacho mnakifanya, kwa hiyo, mimi niwashauri tu na najua Mheshimiwa Mama Samia ni mwanamke ambaye anaweza kusimama na anasimama. Nina hakika atakuwa amenisikia na atakwenda kuwapoza Watanzania hiyo milioni 50 ili isiwe ahadi ya uwongo. Naye tunamwamini na mwanamke siku zote akimuahidi mtoto wake kwamba, nitakuletea pipi, basi akitoka akirudi anakuja na pipi, atakwenda kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika chache ama sekunde chache zilizobaki, naomba niendelee na suala zima la mikopo ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu kama wenzangu walivyosema. Mikopo hii kwenye halmashauri zetu nydingi imekuwa ni mikopo kichefuchefu naweza nikasema. Kwanza vikundi vinavyokopeshwa vina walakini na vikikopeshwa fedha hizo hazirudi, zikichukuliwa zimechukuliwa jumla. Ukihoji hakuna maelezo yoyote ya kina ya kutosha yanayokwenda kutoa majibu kuhusiana na mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii tulisema tuwapatie wanawake wetu na vijana na watu wenye ulemavu ili kuweza kupunguza familia tegemezi ambazo

Serikali imekuwa ikiendelea kutoa mchango kwenye kupitia mfumo wa TASAF kwenda kuzisaidia familia tegemezi ama familia maskini. Kwa hiyo, niilombe sana Wizara ya TAMISEMI iweze kuona na kufuutilia suala zima la mikopo hii ya asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda wako na Mungu akubariki sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Kunti, ila Waheshimiwa Wabunge tusianze kumtwika Rais wetu mambo ambayo hajaahidi, ikiwa ni pamoja na hili la milioni 50 halipo kwenye ilani aliyokuwa anainadi 2020 - 2025. (*Makofii*)

Tuelewane vizuri kwamba, Mbunge ye ye ameamua kuweka mchango wake hapo kwa maana ya 2015/2020 watu wasije wakaanza kumdai Rais Samia Suluhu Hassan kwamba, ameahidi milioni 50 kila Kijiji, hiyo ahadi haipo kwa sababu, alipita kwenye majimbo yetu na hakusema hilo na ilani yetu haisemi hilo.

Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Santiel Kirumba ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango katika hoja ambayo iko mbele ya Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu ambaye hapo nyuma alikuwa ni Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga na sasa tumemkabidhi Jimbo la Tanga Mjini na kazi inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze rafiki yangu Mheshimiwa Sillinde na Ndugu yangu Dugange kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, lakini kipekee nimpongeze sana Katibu Mkuu Profesa Riziki Shemdoe. Huyu ni kijana wangu anatoka kabisa pale Mlalo, kwa hiyo, hayo ni matunda ya Mlalo. Pia niwapongeze Ndugu Magembe na Ndugu Gerald Mweri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu ujikite sana kwenye eneo zima la elimu na nitaanza katika ngazi ya Halmashauri ya Lushoto ambayo ni halmashauri ya nne nchini kwa kuwa na shule nydingi za msingi. Halmashauri ya Lushoto ina shule za msingi 168, shule hizi ni nydingi sana ambazo nadiriki kusema kwamba kwa ngazi ya Halmashauri tunashindwa kuziendesha sisi wenyewe, hivyo, tunaiomba Wizara na Mheshimiwa Ummy yeye alikuwa Mbunge wa Viti Maalum anajua, watusaidie tutengeneze Kanda Maalum ya Kielimu ya Lushoto, vinginevyo Mara zote mtatuona shule za Lushoto zikiwa za mwisho katika mitihani mbalimbali kwa ngazi zote kuanzia msingi mpaka sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Lushoto imetawanyika sana kwa sababu ya safu ya Milima ya Usambara, kwa hiyo, hata jiografia yake ni ngumu sana kufikika kila mahali na hiyo pia inachagiza hata watumishi mara zote wanapoletwa Lushoto, hasa Wlimu, wanahama na kuhamia Wilaya nyagine za bondeni ama mkoani kwa ujumla. Kwa hiyo, tatizo kubwa ni jiografia ambayo sasa inaathiri utoaji wa elimu na upatikanaji wa elimu bora, kwa hiyo, niombe sana, ukiangalia mgawanyo wa baadhi ya halmashauri, kwa mfano nitasema Mafinga Mjini kwa ndugu yangu, shemeji yangu, Mheshimiwa Chumi, shule za msingi katika Halmashauri ya Mafinga ni 28, ukienda pale Korogwe Mji ni 36, ukienda Pangani ni 36, lakini ukienda Mlele kwa Mheshimiwa Kamwelwe pale wana shule 13 katika halmashauri nzima, utawezaje kutoa mgao sawa na halmashauri yenye 168? Hii kwa kweli ni dhahiri kwamba, jambo hili lazima liratibiwe upya na tuweze kuwa na mgawanyo ambao unaeleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye Walimu; Walimu waliokutwa na vyeti *fake* katika Halmashauri ya Lushoto walikuwa 216, lakini hatujarejeshewa idadi hiyo, isipokuwa tulikuwa tunapata tu mgawo huu wa kawaida wa Walimu 16, Walimu 24, Walimu 60 na katika awamu hizi zote tatu za nyongeza ya Walimu. Kwa hiyo, niombe sana kwamba, wale ambao wametoka kwa sababu ya vyeti *fake* 2016 tungepata idadi kamili ile irudi ili iweze kusaidia katika

eneo hilo. Hivi ninavyozungumza tuna uhaba wa Walimu 1,274 katika Halmashauri ya Lushoto kwa hiyo, utaona kwamba ni tatizo kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie katika eneo lingine ambalo hili ni la kitaifa.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kuangalia muda nilisema Taarifa ya Mheshimiwa Agness Mathew Marwa ingekuwa ya mwisho. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa ambalo tunalo katika mgawanyo wa hizi fedha ambazo zinakwenda kwenye *capitation*. Serikali imeweka utaratibu mzuri tu ambao tangu mwaka 2016/2017 tulitenga zaidi ya shilingi bilioni 219, lakini mwaka 2017/2018 bilioni 220, mwaka 2018/2019 shilingi bilioni 286, mwaka 2019/2020 shilingi bilioni 288 na mwaka 2020/2021 shilingi bilioni 298. Ni jambo jema kabisa kila mwanafunzi kati ya wanafunzi milioni kumi n amia tano wa shule za msingi wanapata Sh.10,000, lakini pia wanafunzi milioni 2,200,000 wa shule za sekondari pia wanapata shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja iko pale kwenye ile pesa kuna shilingi 4,000 hii inakatwa kwa ajili ya vitabu, inayokwenda shulenii ni shilingi 6,000 ambayo na yenye we ina mgawanyo wake; kuna ambazo zinakwenda matumizi ya ofisi asilimia 35 kwenye ile shilingi 6,000; taaluma asilimia 30 kwenye shilingi 6,000; mitihani asilimia 15 kwenye shilingi 6,000; huduma ya kwanza asilimia 10 na ukarabati asilimia 10 ambapo ukiangalia asilimia 10 hizi ni kama shilingi 600. Sasa sijui ukarabati wa Sh.600 tunakarabati nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja yangu iko kwenye zile shilingi 4,000 ambazo zinakuwa *retained* kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Ni masikitiko makubwa kwamba, ndani

ya kipindi cha miaka hii mitano vitabu vimeanza kusambazwa takribani miezi mitatu iliyopita, mimi ndio nimeona vitabu kwenye Halmashauri ya Lushoto. Bahati mbaya sana vitabu vyenyewe vimekuja kwa *ratio* ya wanafunzi watatu kwa kitabu kimoja. Sasa ninajuliza kwamba, hizi hela zote zilizotengwa kwa miaka mitano ambazo ni takribani shilingi 200,000,000,000, zimefanya kazi gani na ziliwuwa zimebekwa kwenye akaunti gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vitabu vimechapishwa kwa mara moja tu, tutaona kabisa kwamba hapa kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuna tatizo, lakini pia kwenye Wizara inayosimamia sera, kwa maana ya Wizara ya Elimu, kuna tatizo. Tukumbuke kwa mara ya kwanza walichapa vitabu vya shilingi 144,000,000,000 ambavyo vilikuwa vimekosewa na vikaondolewa kwenye mzunguko. Hatujawahi kuambiwa ndani ya Bunge hili kwamba, wale waliotia ile hasara wamechukuliwa hatua gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali huko za watu, wahujumu uchumi na kadhalika, lakini katika eneo hili hatujawahi kuona shilingi 144,000,000,000 ambazo vitabu vimechapishwa havina ubora, lakini pia vimekosewa, havikuwa na maudhui, wala havikuwa vinafuata hata mtaala husika, vimeondolewa katika mzunguko kimya kimya na vimewekwa kwenye maboksi vimeachwa huko huko kwenye shule wala hawajavikusanya, hatuambiwi hasara hii ambayo Taifa tumeipata ni watu wangapi wamewajibika kwa kosa hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana hizi ni zama za kuambiana ukweli. Tunaomba kabisa kwamba tusicheze na elimu, kwa sababu haya matatizo yote tunayoyaona sasa hivi ni kwa sababu tulikuwa tunaifanya elimu kama ni jambo ambalo sio la msingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana tupate majibu na hizi ni takwimu sahihi kabisa kutoka Serikalini

huko. Watueleze pesa zetu hizi za vitabu kwa miaka mitano na vitabu vimepelekwa katika awamu hii, tena miezi mitatu iliyopita na bado vimepelekwa kwa *ratio* ya watoto watatu kwa kitabu kimoja kwa mujibu wa halmashauri yangu.

Ningependa sana kuona kwamba kama tunasema kila mwanafunzi anapata Sh.4,000 kwenye *capitation*, tulitaka kuona kwamba wanafunzi nchi nzima wanapata vitabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwa kuwa sasa tunakwenda katika ulimwengu wa TEHAMA ningeomba sana kwamba kwenye *capitation* hii tuangalie sasa uwezekano wa kuanza kwenda kupeleka *ipad* ama *computer* mpakato kwa wanafunzi ili waanze kusoma kwa kujifunza mambo ambayo yanabadilika katika dunia hii ya leo. Tunakwenda katika *artificial technology* ambayo TEHAMA ndio inayotawala ulimwengu sasa tutakapokuwa tunaendelea kupeleka hela za vitabu, lakini tuone pia umuhimu wa kuangalia eneo zima hili la teknolojia kwa sababu sasa hivi umeme vijiji umeendelea kwenda na maeneo mbalimbali sasa umeme upo. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba, tukiweka hivyo tutawasaidia hawa vijana wetu kujifunza kwa vitendo kwenye dunia ambayo wanakuja kuitawala siku za usoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa JaneJelly Ntate ajandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia. Awali ya yote niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Ummy kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa TAMISEMI, naamini kwa kushirikiana na Naibu Mawaziri wachapakazi kazi itafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na eneo la mapato ya halmashauri na katika eneo hili nizungumzie suala la ushuru wa huduma (*service levy*) ambayo ilikuwa ikilipwa na makampuni ya simu makubwa haya ya *Vodacom*, *Airtel* na *tiGO*. Kwa kipindi kirefu kulikuwa na shida kubwa kwamba, hizi kampuni kubwa za simu ushuru wa huduma (*service levy*) ulikuwa unalipwa kwa halmashauri moja tu ya Kinondoni pamoja na kwamba, hizi kampuni za simu zilikuwa zinazalisha mapato kutoka maeneo yote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na tatizo kubwa kwamba, hizi kampuni za simu zilikuwa zinapata mapato kutoka Mbeya, Mwanza, Muleba, nchi nzima, lakini ushuru wa huduma ulikuwa unalipwa kwa halmashauri moja tu ya Kinondoni kwa sababu, eti makao makuu ya kampuni hizi yalikuwa yako Kinondoni na kwamba, sheria ilikuwa inasema hilyo. Ambayo ilikuwa ni *very unfair* kwamba, kampuni *in-generate* mapato kutoka halmashauri zote na halmashauri hizo zinastahili kupata ushuru wa huduma (*service levy*) lakini ilikuwa inalipwa kwa Manispaa moja tu ya Kinondoni kwa sababu, makao makuu yalikuwa pale, hii ilikuwa ni *very unfair*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Waheshimiwa Wabunge tulijenga hoja na tukapitisha sheria kuanzia mwezi uliopita ambao unaendelea mpaka sasa kwamba, sasa hizi kampuni badala ya kuilipa Kinondoni kwa sababu, Kinondoni ilikuwa inanufaika inapata mpaka bilioni sita kwa mwaka wakati halmashauri nytingine hazipati hata shilingi, kwamba, badala ya hizi kampuni kulipa ushuru wa huduma kwenye halmashauri moja basi walipe ushuru wa huduma TAMISEMI, halafu TAMISEMI isimamie kuhakikisha inagawanya huu ushuru wa huduma ili halmashauri zote Tanzania ambazo na zenyewe zina minara ya simu zinazalisha mapato, zipate ushuru huu wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema kwamba, baada ya kampuni hizi kupeleka ushuru wao wa huduma TAMISEMI, TAMISEMI iwasiliane na *TCRA* ili *TCRA* iwave mchanganuo kwa sababu, *TCRA* inajua kwamba, hizi kampuni zimepata kiasi

gani kutoka Mbeya, Mwanza au Nzega, ili kila halmashauri ipate stahiki yake ya ushuru wa huduma kwa mujibu wa mapato ilioyo-*generate* kwenye halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia nimeona kwamba, ni kweli kampuni za simu sasa hivi zinapeleka ushuru wa huduma TAMISEMI, lakini TAMISEMI wanachofanya wanagawanya *equal*, kwamba, kuna Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kwa hiyo, wakipata yale mapato wanagawanya tu *equally* kwa 185 bila kujali mapato yaliyozalishwa katika eneo husika, ambayo haikuwa sheria tuliyopitisha.

Kwa hiyo, niwaombe TAMISEMI sasa kwamba, hizi kampuni kubwa za simu zikishaleta ushuru wao wa huduma pale TAMISEMI, TAMISEMI iwasiliane na *TCRA* ili *TCRA* iwape mchanganuo kwamba, Mbeya wanastahili kiasi gani, Muleba wanastahili kiasi gani, Nzega wanastahili kiasi gani, Handeni wanastahili kiasi gani, Same wanastahili kiasi gani, ili kila halmashauri ipate stahili yake husika sahihi na wala sio kugawa *equally*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu, naona sasa hivi TAMISEMI pengine wanaogopa kazi au vipi wakilipwa hayo mapato kutoka hizi kampuni za simu wao wanagawanya tu *equally*, kwa hiyo, kila hlmashauri inapata milioni 10 au ngapi basi, wakati halikuwa lengo la sheria tuliyopitisha. Naomba TAMISEMI wafanye kazi ili kila halmashauri ipate stahiki yao. Nina uhakika mapato ya kampuni ya simu ya Mbeya hayawezি kuwa sawa na mapato ya kampuni ya simu ya Muleba. Mapato ya kampuni ya simu yanayokuwa *generated* Tanga hayawezی kuwa sawa na mapato ya kampuni ya simu yanayokuwa *generated* Nzega, kwa hiyo, lazima kazi ifanyike TAMISEMI wawasiliane na *TCRA* ili kila halmashauri ipate stahiki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni *TARURA*, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea. Nataka niongezee tu hapo kwamba, kwa nini Wabunge wengi wanataka *TARURA* iwezeshwe ili iweze kuimarisha barabara,

hasa za vijijini ni kwa sababu, barabara za vijijini zina *impact*, zinaathiri sekta nyingine za maisha kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea, nilitaka kiongezee tu hapo kwamba kwanini Wabunge wengi wanataka *TARURA* iwezeshwe ili iweze kuimarisha barabara za vijijini ni kwa sababu barabara za vijijini zina *impact*, zinaathiri sekta nyingine za maisha kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za vijijini wote tunafahamu kwamba watu wetu wengi wanaoishi maeneo ya vijijini shughuli yako kuu ni kilimo, na ili kilimo kibadilishe maisha yako maana yake ni bei ya mazao iwe nzuri, na hauwezi kupata bei nzuri ya mazao ukiwa maeneo ya kijijini kule Mashambani kama barabara ya kuyatoa mazao kule shambani na kuyafikisha sokoni itakuwa mbaya. Kwa hiyo, tunapozungumzia *TARURA* ipewe fedha iimarishe barabara za Vijiijini tunazungumzia bei ya mazao na hali nzuri ya wakulima kule vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za vijijini zina athari kwa huduma nyingine kama Afya na Elimu, sisi maeneo ya kwetu kule maeneo ya kwa mfano Jimboni kwangu kule Bulende, Itumbili Siliaza wakati wa masika barabara hazipitiki kabisa, kwa hiyo hata wanafunzi hawawezi kwenda shule, kwahiyio tunazungumzia barabara lakini maana yake ni kwamba barabara hii *TARURA* wasipowezeshwa wakaifanya ipitike ina-*impact* inaathiri kwenye elimu kwasababu hata watoto hawawezi kwenda shule kwasababu mito inajaa, mabonde yanajaa watoto hawaweze kupita, kwa hiyo ni barabara lakini ni barabara ambayo ina-*impact* kwenye Elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuwa na barabara vijijini kwenye vitongoji hazipitiki maana yake hata huduma ya Afya inaathirika kwa kiwango kikubwa tunasema akinamama wajifungulie zahanati wajifungulie kwenye vituo vya Afya kuna maeneo mengine wakati wa masika huwezi

hata kupita kutoka kwenye kitongoji unachoishi kwenda kwenye zahanati, kwasababu barabara inakatika kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyio ni barabara, ukiitazama unaona barabara lakini maana ni huduma ya Afya ina-*impact* kwasababu mwananchi, huyu mama mjamzito ambaye anatakiwa akajifungulie kwenye kituo cha Afya hawezi kufika ku-access kituo cha Afya au zahanati.

Kwa hiyo, tunaposema barabara za vijiji ni ziwe *improved* maana yake ni maisha bora ya wakulima kwa maana ya bei nzuri ya mazao maana yake watoto waweweze kwenda shule, maana yake ku-*improve* elimu, maana yake hao wananchi waende wa-access wafike kwenye vituo vyaa afya na zahanati maana yake kui-*mprove* afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kwamba huu mwaka wa fedha tunaokwenda kuumalizia ambayo imebaki miezi miwili halmashauri yangu ya Nzega iliidhinishiwa nilioni moja kwa ajili ya kujenga jengo jipya la Halmashauri kwasababu baada ya agizo la kwamba halmashauri za vijiji zilizokuwa mijini zihame sisi Nzega tulihama kutoka Nzega Mjini tukaenda Ndala, sasa kule Ndala tulipo sasa tunakaa kwenye madarasa ya Shule ya Sekondari ya Ndala pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake ni kwamba tunazuia hata ile shule sasa ishindwe kuandikisha wanafunzi kwasababu ndizo ofisi za halmashauri sasa hivi tupo madarasani. Sasa hiyo bilioni moja ambayo iliidhinishiwa Mheshimiwa Waziri nikuomba kama kuna uwezekano lifanyike lolote linalowezekana tupate hiyo, tuanza kujenga ofisi. Ofisi tuliyokuwanayo pale mjini tumewaachia Halmashauri ya Mji, kwa hiyo tunakaa madarasani kwa hiyo kukaa kwetu madarasani tunazuia hata wanafunzi wasiweze kupata elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili kama Mheshimiwa Naibu Waziri ufanya kila linalowezekana hii miezi miwili iliobaki hii bilioni moja tuliyoidhinishiwa iweze kutoka,

Hamashauri ya Nzega tuhame kwenye madarasa, tupate jengo letu tuanze kufanya kazi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia 100, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Mpakate tutamalizia na Mheshimiwa Janejelly Ntate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya TAMISEMI kwanza niwashukuru Serikali kwa yote yaliyofanywa katika Jimbo la Tunduru kusini. Kwasababu ya hotuba illyotolewa na Waziri naomba nichangie katika sehemu tatu, sehemu ya kwanza ni suala la Utawala bora na sehemu ya pili ni Afya na sehemu ya tatu itakuwa ni suala la Elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na suala la Utawala bora kama ulivyoeleza kwenye hotuba yako umeeleza vizuri namna ambavyo Utawala Bora inatakiwa viongozi wetu wa Serikali waweze kuwasikiliza wananchi ili kupata kero zao. Lakini kwenye Wilaya yetu ya Tunduru, halmashauri yetu ina vijiji 157 na ina vitongoji zaidi 1,100 tuna Mkurugenzi mmoja, tuna DC mmoja akitaka kupita maeneo yote kusikiliza kero vijijini maana yake kwa mwaka atabidi atumie zaidi ya siku 157 ili kupita kusikiliza kero katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa kwasababu linasababisha viongozi wetu wa wilaya wasiweze kufika maeneo ya vijijini kusikiliza kero za wananchi. Naomba sana tumewahi na tumepitisha mara nyingi maombi ya kugawa Wilaya ya Tunduru pamoja na kuwa na halmashauri mbili na Wilaya peke yake ziwe mbili, hii itarahisisha kupata Mkurugenzi, kupata Wakuu wa Wilaya wawili ambao watasadidia kuhakikisha kwamba wanasililiza kero za wananchi kwa urahisi zaidi kuliko ilivyokuwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iangalie Wilaya ya Tunduru halmashauri hii ilipata Wilaya tangu mwaka 1905 Mkoloni, walio wengi humu ndani tulikuwa hatujazaliwa, tunaomba sana Wilaya hii muifikirie, halmashauri hii iweze kugawika katika sehemu mbili ili kurahisishia wananchi wapate huduma hizi na kero zao wazieleze kwa urahisi zaidi kwasababu Mkurugenzi, Wakuu wa Wilaya watafanya kazi hii ya kuwasikiliza wananchi kwa wakati mmoja ili waweze kutoa kero zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili suala la Afya ukiangalia kama Halmashauri ya Tunduru ina kata 39, ina zahanati 52 tu kat i ya vijiji 157. Kwa hiyo, kwasababu ya ukubwa wake ulivyo utakuta kituo cha afya kimoja kinahudumia kata tatu mpaka nne, tuchukulie mfano kituo cha Afya Mtina kuna kata tano zinahudumia kituo kimoja, kaini bado kuna matatizo ya miundombinu ya maeneo yale kwasababu hakuna Wodi ya akinamama hakuna *Maternity ward* kama nilivyozungumza hakuna chochote, hakuna chumba cha upasuaji, kwa hiyo watu wanatembea mwendo mrefu sana kwenda kufuata huduma za Afya Mtina. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mara nydingi kutokana na hali mbaya ya barabara zetu zilivyo wananchi wale wanabebwa kwenye matenga, matenga yanabebwa kwenye baiskeli au pikipiki kwenda Hospitali. Akinamama wajawazito wanabebwa kwenye matenga kwenda kwenye kituo cha Afya kwa ajili ya kuwashudumia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kama sera inavyosema kila Kata iwe na kituo cha Afya, naomba tuboreshe kituo cha Afya Mtina ili kiweze kutoa huduma ile ambayo inatakiwa na ikiwezekana tuongeze kituo cha Afya kingine kwenye Kata ya Lukumbure, Nchesi Tuwemacho pamoja na Namasakata. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuna ahadi ya muda mrefu sana ya Rais wa Awamu ya Nne ya kujenga kituo cha Afya Nalasi jambo hili tangu mwaka 2014 nimeuliza Bungeni *term* iliyopita Bunge la Kumi na Moja zaidi ya mara

tatu. Halmashauri imejitahidi imepeleka zaidi ya milioni 80 pale kuanza kujenga, lakini kila mwaka kwenye bajeti yetu tunatenga shilingi 100,000,000 kwa ajili ya kuendeleza kile kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na ukubwa wa Halmashauri yetu na mapato yetu pamoja na kwamba tunapata zaidi ya Bilioni tatu kwa mwaka lakini hazitoshi kwasababu eneo letu ni kubwa kata ni nyingi mgao unakuwa hauotoshelezi kuweza kujenga kituo cha afya maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwasababu nimeuliza mara chungu nzima nimeenda kwa Mheshimiwa Waziri Jafo kipindi kile hadi kwa Katibu mkuu kuhusiana na ahadi hii naomba muangalie namna ambavyo Nalasi inaweza kuingia kwenye bajeti hii kituo kile kiweze kujengwa ili kuondoa hii dhana ambayo Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi ya viongozi wetu wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo suala la Elimu kwa kweli kwa Wilaya ya Tunduru tuna shule ya Msingi 152 kati ya hizo zina upungufu wa walimu zaidi ya 1,000 tunahitaji walimu 220 tunao 991. Shule nyingine zina walimu watatu hadi wanenye, asilimia 60 zina walimu watano, maana walimu wengi wapo mjini hapa vijijini kwangu hakuna walimu. Naomba sana suala la walimu litakapokuja kufanyiwa ufumbuzi wa kuajiri walimu wengine tuone sisi wenye Majimbo ya vijijini kuhakikisha kwamba wanapata walimu wa kutosha ili kuhakikisha kwamba wanatoa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana shule zetu za Serikali ufaulu unakuwa ni mdogo kwasababu walimu hawapo, hawatoshelezi nichukulie mfano shule ambayo ninatoka shule ya Semeni ina zaidi ya wanafunzi 900 walimu wapo saba, madarasa yapo sita wanaelewaje hawa watu, wanafundishaje? Wanafauluje hawa Watoto? Naomba sana kwenye miudombinu ya madarasa tujitahidi kama walivyzungumza wenzangu kwenye mgao huu wa majengo ya zahanati, majengo ya shule za msingi muangalie maeneo

au Majimbo ambayo yana vijiji vingi yapewe kipaumbele ili mgao uwe wa kutosha kuhakikisha kwanza tunapunguza tatizo la madarasa tunapunguza matatizo ya zahanati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ningependa kuongelea suala la *TARURA*, kwa kweli *TARURA* naungana mkono na wenzangu Bunge liliopita tulionba tuongeze shilingi hamsini kutoka kwenye mafuta ili wapewe *TARURA* kuhakikisha kwamba barabara zetu wanatengeneza vizuri, naona wenzangu wamesahau tunaomba sana jambo hili tuliongea kwa uchungu miaka mitano iliyopita, kama mmeshindwa kwenye mafuta basi chukueni hata kwenye simu, ili tupate fungu la kuhakikisha kwamba tunajenga barabara zetu ziwe nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia mfano Tunduru Wilaya nzima ya Halmashauri ina kilometra 1,200 bajeti iliyopita tulipewa bilioni moja na Milioni 250 ambayo kwa hesabu ya kawaida ambayo wanatumia *TARURA* wana uwezo wa kukarabati barabara ambayo ina urefu wa kilometra 103 kwa maana hiyo Kilometra 1,100 zote hazina fedha, kwa maana hazijatengewa fedha, na kwa hali ilivyokuwa mbaya kama tutaendelea na mtindo huu wa *TARURA* kupewa fedha zilizopo bila kutenga fedha nyingine hizi barabara zitakuwa bado zina shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye Jimbo langu kuna barabara ambazo zina zaidi ya miaka 20 hazijawahi kupitiwa na greda, greda yao ni miguu ya watu na baiskeli, kwa hiyo inaonekana hapa kuna barabara kwasababu miguu ya watu inapita pale, baiskeli zinapita pikipiki zinapita unajua kwamba hii barabara inakwenda kijiji fulani. Kuna barabara ya Chemchem kwenda Ligoma mpaka Msinji ina zaidi ya miaka 15 haijawahi kufanyiwa ukarabati, kuna barabara ya Ipanje, Ndishyaje mpaka Marumba ina zaidi ya kilometra 40 haijawahi kufanyiwa chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Marumba - Masugulu nayo haijawahi kufanyiwa chochote

kuna barabara ya Mchima Lashya Chemacho hamna kitu, barabara Amani kiungo mpaka Misechela, nayo haijawahi kutengenezwa kwa muda mrefu sana.

Naomba sana jambo hili mliangalie *TARURA* wapewe fedha za kutosha ili waweze kuhakikisha kwamba barabara zetu zinapitika kwa wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tumalizie na Mheshimiwa Janejelly Ntate.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa Afya na leo na mimi nichangie kwenye bajeti ya TAMISEMI. Lakini nikupongeze Mheshimiwa Ummy kwa kuteuliwa na kuendelea kuaminika kuisaidia Serikali pamoja na wasaidizi wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia walioandaa llani ya Chama cha Mapinduzi, hawa kweli kweli walikuwa na fikra zilizo sahihi, kwa mara ya kwanza llani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa 180 -181 inaongelea maslahi ya watumishi wazi kabisa, na niwashukuru waliochangia kwa kusema maslahi ya watumishi wa Tanzania. Hasa wengi mlilikita kwa walimu lakini niipongeze pia Serikali imefikia uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025, lakini waliofanya hii kazi ni watu gani, ni watumishi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na nilipokuwa naangalia makundi yangu ya watumishi hata Wabunge mpo ni watumishi wangu wa miaka mitano mitano, lakini kuna wale watumishi wanaotoka baada ya miaka 60 kustaafu. Lakini watumishi hawa walikuwa wanafanya hivi vyote kwasababu gani, walikuwa na maagano na Serikali, Serikali kupitia vyama vya wafanyakazi iliwaomba watumishi, kwamba tuvumilie kwa miaka mitano tujenge Uchumi, baada ya kumaliza kujenga uchumi tutakuja na maslahi yenu na ndio maana

Ilani ya Uchaguzi imeyasema tumezungusha hapa tunaongea matatizo ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unjuka wangu mheshimiwa Jenista ulipokuwa unawasilisha bajeti yenu ya Waziri Mkuu niliangalia angalia sikuona suala la nyongeza ya mshahara lakini nikasema ngoja ninyamaze labda ndio *style*, TAMISEMI mmekuja na bajeti bado haioneshi ukiangalia vifungu nya mishahara kama kutakuwa na nyongeza, na jambo hili tusipoliangalia na kulisemea tunasema mtatizo matatizo lakini hatuangalii chanzo cha tatizo. Yawezekana hata kushuka kwa utendaji ni watumishi wamefika mahali wamekufa ganzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ebu tujiulize kwenye miaka mitano ni watumishi wangapi wamestaafu kwa mshahara wa zamani ambapo tunajua sheria kkokotoo hufanyika kwenye mshahara, waheshimiwa Wabunge niwaombe kwenye hili wote mni-*support* tuongelee suala la nyongeza ya mshahara, nyongeza ya mshahara kwa mtumishi inaongeza hata mafao yake, lakini miaka mitano watumishi hawa walivumilia ili tujenge uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeshajenga uchumi umefika uchumi wa kati tena kabla ya muda wake, na ukiangalia mambo ya kufanya watumishi kwenye llani yapo 16 sasa kama tukipita bajeti hii bila kulisema hili, ambalo limeandikwa pale naomba kunukuu; "kwamba Serikali itaboresha mishahara ya watumishi wa umma kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi wa Taifa na tija ya wafanyakazi," tija wameifanya watumishi wamefikisha uchumi wa kati kabla ya muda wake na uchumi umefika uchumi wa kati. Sasa tunasubiri nini kuongeza mishahara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuongeze mishahara watumishi, Waheshimiwa Wabunge na nyie linawahusu, watumishi wakiongezewa na nyie mtaongezewa kwasababu na nyie ni watumishi wa miaka mitano lakini naona tunalifumbia fumbia macho. Sasa kwa sababu nimetumwa kuwakilisha watumishi leo ngoja nilisemee hilo la mishahara

ya watumishi na nimeona Waziri wa Fedha anaondoka na begi lake lakini nadhani atanisikia alipo kama bajeti yake itakuja haina nyongeza ya mshahara... (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngoja ngoja Mheshimiwa Janejelly, waheshimiwa wabunge huwa narudia mara kadhaa, Mbunge unapochangia zungumza na kiti na sio Mawaziri.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Kwasababu ukizungumza na Waziri asipofanya usije ukalidai Bunge, ongea na kiti ndicho kinachotunza kumbukumbu ni nani ambaye ameomba kitu gani. Hata Mheshimiwa Ummy hapa akinyanyuka akaenda usiseme Waziri ametoka namsubiri atayapata tu, kwa hiyo, wewe zungumza na mimi usimwangalie Waziri yupo katoka taarifa zake atazipata.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee na kiti chako, niseme hivi kama Wizara ya Fedha ikija haina nyongeza ya Mishahara ya watumishi kwa kweli kwa bajeti hiyo wabunge mni-support tukamate shilingi watumishi wanaumia kwa nyongeza ya mishahara na yawezekana haya yote tunaona utendaji unashuka, Wakurugenzi wanafanya vibaya, unajua msongo wa akili unaweza ukafanya, ukafanya mengi, yawezekana wengine wanakaa kimya, wengine wanakuwa na hasira lakini wengine wamedumaa utendaji umedumaa. Hapa nina meseji nilikuwa ninazisoma watumishi wanasema miaka mitano tulioyahidiana imekwisha kuja jambo letu ebu liongee jambo letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na jambo la watumishi ni nyongeza ya mshahara, jambo la watumishi ni kupandishwa vyeo, jambo la watumishi ni kuangalia hayo maslahi yao, nguzo yao kubwa ni mshahara maisha yanapanda, kodi za nyumba zinapanda ada za shule zinapanda lakini mshahara upo vile vile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee na suala la walimu hakuna mtumishi anayeumia kama mwalimu na hii haina mwalimu yupo Dar es Salaam haina mwalimu yupo Tabora. Walimu sasa hivi nauli ya likizo imekuwa ni kitendawili, ni neno gumu kwenye kamusi mtu anakwenda likizo tatu nne hajawahi kulipwa nauli ya kwanza ya likizo. Wakistaafu nimeshuhudia Mkurugenzi mmoja anawaambia nitawatafutia roli sasa, na hakunijua kama ni Mbunge wa Wafanyakazi lakini nilimwambia hakuna mwalimu atakayekwenda na roli, alisema nitawapakia kwenye roli sina fedha TAMISEMI hawajaleta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwalimu aliyefanya kazi akafikisha umri wa miaka 60 leo unamwambia utampeleka na roli, utampeleka na roli wapi lakini wanawapiga dana dana akienda Manispaa wanamwambia TAMISEMI ndio wana fedha zako, akienda TAMISEMI wanamrudisha. Jana nilikuwa na walimu ambao ni tatizo wanaongezwa vyeo lakini mishahara haibadilishwi, mpaka amefikia kustaafu wapo watano na ni Manispaa ya llala inabidi niseme. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamenifuata Bungeni hapa wamelipwa pensheni lakini wa mishahara ya zamani lakini Manispaa inawaambia mfuko ndio una tatizo, namshukuru sana Mkurugenzi wa Mifuko, tumeenda pale ametupokea aka-*print* barua zote ambazo alikuwa anaandikiana na Manispaa kwamba ebu lipa mapunjo yao, lipa faini mnazotakiwa hawa wapewe tofauti zao. Lakini ebu fikiria mstaafu amepanda gari kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na unamdanganya tu unamwambia mfuko ndio unashida. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu walipandishwa vyeo miaka sita mtu hakubadilishiwa mshahara na amefikia kustaafu. Naomba Wabunge tuwe wakali Wabunge kazi yetu ni kuishauri Serikali tuwashauri haya wayaangalie na sio kwa walimu yanawapata watumishi wengi, watumishi wengi, wengi mno wapo kwenye tatizo hilo la kulipwa pungufu ya pensheni kwasababu wanapopandishwa madaraja mishahara yao haibadilishwi lipo kabisa hilo. (*Makof*)

Mheshimia Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja lakini tuliangalie la nyongeza ya mshahara naunga hoja mkono. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa uchangiaji wetu kwa Asubuhi nitaje majina ya wabunge wachache ambao watachangia kipindi chetu cha Mchana Mheshimiwa David Kihenzile, Mheshimiwa Rehema Migilla Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, Mheshimiwa Salma Kikwete Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mheshimiwa Tunza Malapo na wengine tunaendelea kuwaita kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge Mpaka saa Kumi Kamilil Jioni.

(*Saa 07.05 Mchana Bunge lillahirishwa hadi Saa Kumi Jioni*)

(*Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, ninayo majina hapa ambayo tutaanza nayo mchana huu. Tutaanza na Mheshimiwa David Kihenzile, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Migilla, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mzungumzaji wa kwanza jioni hii. Kwanza nishukuru Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake na Makatibu Wakuu kwa sababu tunawafahamu *record* yao ya uchapakazi, tunaamini watakwendwa kufanya kazi changamoto zote ambazo ziko pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache. La kwanza iko changamoto kwenye Halmashauri zetu, pesa hazitoshi, ikifika karibu na mwisho wa mwaka tunaambiwa pesa zimerudishwa, shida ni nini wakati mahitaji yapo na

miradi bado haijakamilika? Tunamuomba Mheshimiwa Waziri atusaidie jambo hili lisijitokeze. Kama changamoto ni fedha zinachelewa kupelekwa, basi angalau ziweze kutumwa katika muda muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunayo changamoto ya miradi ambayo haiishi. Akipita huko kwa navyofahamu uchapakazi wa dada yetu atapata nafasi ya kufanya *survey* kutazama miradi gani ilianza lini na kwa nini haijakamilika. Mimi nimefanya ziara kule kwangu kuna miradi mingine ina miaka mpaka 10 haijakamilika, hii si sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni la kupima ardhi, wananchi wanahitaji sana wapimiwe ardhi yao. Kwanza inaondoa migogoro, pili ni chanzo cha mapato cha uhakika cha Serikali yetu. Napenda Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa kwa ajili ya kuhitimisha atuambie mpango wa Wizara suala hili wanalianzaje na pengine watalikamilisha lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ni changamoto ya ofisi zetu za Wakuu wa Wilaya. Katika mwongozo wa kuandaa bajeti tunaambiwa agenda namba moja ni suala la ulinzi na usalama. Hata hivyo, ukitazama Ofisi za Wakuu wa Wilaya kirasilimali zina changamoto kubwa sana. Mimi nashauri kwa kuwa ofisi za Wakuu wa Wilaya ndiyo wasimamizi wa Halmashauri Mheshimiwa Waziri atazame kama inawezekana asilimia sehemu ya mapato ya ndani iwe *allocated* kwa ajili ya kuendesha ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa ajili ya mafuta na vitu vingine vidogo vidogo, tutawasaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, agenda nytingine ambayo imezungumzwa na watu wengi hapa ni *TARURA*, ni changamoto kubwa sana. Suala hili naomba Mheshimiwa Waziri alichukue kwa namna tofauti. Barabara zikiwa mbovu zina uhusiano wa moja kwa moja na mapato hafifu ya Halmashauri. Barabara zikiwa mbovu zinaharibu magari ya Halmashauri, sasa kumbe kwa kuwa *TARURA* imewekwa ndani ya *TAMISEMI*, kama Serikali Kuu haiwezi kuongeza fedha

basi ni vema ikatoka *circular* kwamba asilimia fulani ya mapato ya Halmashauri iende ikasaidie *TARURA*, Wakurugenzi wapewe na CAG anapokagua atazame, je, *to what extent* jambo hili limefanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo maalum kule kwangu, tunazo changamoto kwenye baadhi ya maeneo; mambo kama mawili hivi. Moja, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu au itakavyompendeza, naomba atusaidie vituo nya afya kwenye maeneo ambayo ni yako *very critical*. Mfano, tunayo Kata ya Mtwango ambayo waliojiandikisha kupiga kura ni zaidi ya 17,000, kumbuka Jimbo langu ni la vijijini lakini pale hakuna hata kituo cha afya na pembedi yake kuna kata zingine zaidi ya tatu, ikiwezekana na ikimpendeza atupatie vituo nya afya maeneo ya Mtwango, Idete na Itandula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo kwenye upande wa *ambulance*, tunazo changamoto kubwa sana kuanzia eneo hilo lakini eneo lingine ni ukanda wa Mgololo ambako kuna kata karibia tatu na kuna kituo cha afya kimoja. Eneo lile hata nikikutumia picha hapa barabara ni mbovu, kuna kiwanda kikubwa cha karatasi kule kina wananchi zaidi ya 40,000 kwenye eneo lile, kuwatoa wagonjwa kule mpaka makao makuu ni changamoto kubwa mno, wakipata gari ya wagonjwa tutakuwa tumewasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo naomba kuchangia ni *issue* ya Taasisi zinazo-*operate* katika nchi yetu. Kwanza, nchi nyingi kama ni *International NGO* inakwenda kwenye nchi husika cha kwanza unapewa *condition* lazima ushirikiane na *NGO* au *Institution* iliyopo pale ndani. Kwanza hiyo ina *ensure security* kuwa *monitor* wale watu wakifika hapa wanafanya nini. Hapa kwetu kuna changamoto kidogo, nimuombe Mheshimiwa Waziri aweke mkakati mzuri zaidi, kama ni *USAID* au *whatever* wakifika washirikiane na taasisi za hapa kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutumia mfano mmoja, ni *declare interest* mimi ni Rais wa *Red Cross*, taasisi

ya Kitanzania na inafanya kazi ya Watanzania, imeanzishwa kwa sheria ya Bunge na ikitaka kufutwa itafutwa Bungeni. Hata hivyo, kuna changamoto, kuna programu ambazo ilitakiwa izifanye yenyewe inafanya taasisi za nje matokeo yake wale hawawezi kuwa na uchungu; kama ni kutibu watu hawawezi kuwa na uchungu kama walivyo Watanzania wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine napenda kuzungumzia maafa. Sheria Na.7 ya mwaka 2015, *Disaster Management Act*, imetaja na imefanua Kamati za Maafa kuanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya kijiji. Kwenye ngazi ya Wilaya imemtaja Mkurugenzi kama Mwenyekiti na wajumbe wengine. Leo tuna maafa kwenye kila kona ya nchi hii, ni kwa kiwango gani Halmashauri zina-*respond* kama hazimuachii Waziri Mkuu pamoja na mama Jenista pale? Ni vyema zikatenga fungu na fungu lile lisibadilishwe likafanye kazi ya maafa. Leo kuna mafuriko kila sehemu kwa hiyo, tunajikuta tunakwepa jukumu letu la msingi tunawaachia watu wengine tunashindwa kutimiza jukumu letu ambalo tunatakiwa tulifanye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ambayo napenda kuchangia ni *effective control* ya *Council*, ni vyema Wizara ika *control* vizuri Halmashauri zake. Naomba nitolee mfano na limezungumzwa hapa ndani suala la Makao Makuu, mfano sisi pale kwetu Mufindi kwa lengo la kupeleka huduma kwa wananchi ilikubalika tuanzishe Halmashauri nyiningine lakini Makao Makuu inayojengwa ni kilomita 6 kutoka ilipo Makao Makuu ya Halmashauri ya zamani, hapa ni kwa faida ya nani? Naomba Mheshimiwa Waziri na timu yake ikiwezekana maeneo kama haya wayaundie timu maalum wakayatazame, je, ni kwa maslahi ya wananchi? Hoja siyo wapi ikae lakini inapowekwa Makao Makuu itazame maslahi mapana ya walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho siyo kwa umuhimu napenda pia kuongezea kwenye kifungu ambacho kimezungumzwa na wenzangu tukatazame maslahi ya Madiwani wetu, Wenyevitii wetu wa Vijiji na Wajumbe wa

Serikali ya Vijiji, hawa ndiyo wanafanya kazi kubwa Zaidi. Hili tunaweza kulifanya kwa namna kuu mbili; moja kama kutakuwa na pesa za Serikali Kuu ziende, lakini pili kuzibana Halmashauri zipeleke kama ni posho au nauli ili wale wanaohangaika na wananchi kimsingi waweze kupata posho kama hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Rehema Migilla atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi jioni ya leo niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda kuwapongeza dada yangu Ummy na timu yake wanafanya kazi nzuri na tuna imani nao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja, nitaanza kujikita kwenye suala la afya. Afya ndiyo mtaji wa mwanadamu wa aina yoyote lakini suala hili kwa baadhi ya maeneo linaonekana kama halipewi kipaumbele cha hali ya juu. Mfano nikiangalia katika Jimbo langu huwa naliita Burundi kwa sababu linahudumia asilimia kubwa ya wananchi waliotoka Burundi lakini lina jumla ya Kata 15 lakini ndani ya hizo kituo cha afya ni kimoja tu. Hali hii inasababisha msongamano mkubwa sana wa wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali kwenda kutibiwa kwenye kituo hicho hali inayowafanya mpaka wahudumu kuzingirwa na wagonjwa. Pia wagonjwa wanaweza wakafa pale pale kwa sababu wanasubiri huduma kwa muda mrefu na wengine kujifungulia njiani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali kwa maeneo ya pembezoni hebu tuyape kipaumbele na kuona na yenyewe yanafaa kupatiwa huduma za afya kama zahanati na vituo vya afya. Jimboni kwangu kuna kituo kimoja tu lakini kuna vituo viwili vya afya mfano Kituo cha

Uyoo na Mwongozo tayari vimeshaanza kujengwa na vimefikia hatua za mwisho. Niiombe Serikali iweze kupeleka fedha kwenye vituo hivyo viweze kumalizika na vianze kufanya kazi kuwashudumia hawa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine kwenye afya hapo hapo ni bima iliyoboreshwa. Suala la bima iliyoboreshwa naona kama haiwasaidii wananchi wetu kwa sababu walivyokuwa wanakata waliona kwamba itakuwa ni suluhisho na mbadala pindi wanapokuwa hawana pesa lakini wanapokwenda kwenye hivi vituo vyetu nya afya wakifika pale, mfano kama vituo nya afya na zahanati nyingi hazina hata maabara, kwa hiyo akifika pale inamlazimu aende kwenye zahanati zingine au mahali pengine kwenda kupima ambapo inamuongeza gharama, kwa hiyo, hii bima inakuwa kama vile haina faida. Vilevile ana bima anakwenda kwenye zahanati hakuna dawa anatakiwa anunue. Tunakwenda kuanzisha bima ya afya kwa wote hivyo kabla hatujaanzisha niombe Serikali ifanye tathmini, je, hii bima ya afya iliyoboreshwa imesaidia kwa kiasi gani kabla ya kuingia kwenye hii bima ya afya mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye sekta ya elimu. Kiukweli elimu bado kwenye maeneo yetu ni changamoto kubwa sana. Miundombinu ya elimu kama madawati, madarasa, matundu ya vyoo bado hayatoshelezi. Cha ajabu tunapongeza Serikali imeanzisha mifumo mingi sana ya kupata taarifa lakini hazitumiki. Leo ikifika mwisho wa mwaka Waziri Mkuu anaanza kupiga kelele madarasa; hivi haya maoteo na hizi takwimu ambazo mnazikusanya kila mahali mnazitumia kwa shughuli gani kiasi kwamba tunafanya haya mambo ni kama vile dharura. Niiombe Serikali mifumo ilioianzisha basi itumike kusaidia mambo yasifanyike kwa ghafla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni masharti ya uhamisho. Mtumishi kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ni suala la kawaida na lipo kisheria na anapokwenda kuhamia sehemu nyingine ana sababu ambazo yeye zinamfanya mpaka ahamie kule lakini masharti

ya uhamisho sasa hivi yamekuwa magumu mno. Leo mtu anaambiwa kuhama kituo kimoja kwenda kituo kingine mpaka apate mtu wa kubadilishana naye, anamtoa wapi? Unakuta watu wengine mfano wa vijijini; shule nydingi za vijijini kule watumishi wengi ni wanaume wanataka wafuate wake zao au wanawake wafuate waume zao, inafikia wakati kama walimu wanaamua kutumia watoto wetu kujipoza. Hali hii kweli ni mbaya, inawaingiza watu kwenye majaribu makubwa, wanaume wanajiingiza kwenye mambo ambayo hayafai, ndoa zinavunjika na wanafunzi wetu tunawaingiza katika mtego mkubwa wa kufanya mapenzi na walimu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni *TARURA*. Kiukweli *TARURA* bado ni changamoto, barabara zetu huko vijijini hazipitiki. Niombe *TARURA* basi iongezewe bajeti lakini tofauti na hapo *TARURA* izilazimishe Halmashauri kama nilivyoongea Bunge liliopita ziweze kuanzisha miradi ambayo itasaidia kuongeza bajeti ya *TARURA* ili iweze kuhudumia barabara kwa kiwango kinachotakiwa. Unakuta sasa hivi *TARURA* kwanza hawashirikishi hata Madiwani au Wabunge, unaambiwa barabara yako hii itatengenezwa bila hata wewe Mbunge au Diwani kushirikishwa wakati wewe Diwani au Mbunge ndiyo unajua barabara zifi zina changamoto na barabara zifi zina manufaa kwa ajili wananchi wetu. Nimucombe Waziri awaambie *TARURA* waweze kushirikisha Madiwani na Wabunge kwenye upangaji wa ujenzi wa hizi barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni kwenye mgawanyo hizi asilimia 10 za vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Hizi pesa kwa kiasi kikubwa sana zinakwenda kwa vikundi ambavyo vinakuwa vinarejesha lakini vile ambavyo vinaonekana vinasuasua bado havipewi kipaumbele. Nina maana kwamba tunakwenda kwa kuangalia vile vinavyorejesha lakini hatujui ni changamoto gani zinasababisha hao wengine wasirejeshe ili watu wengine wapate. Hivyo niombe sasa kwenye vikundi ambavyo vinakuwa labda havirejeshi ile pesa ambayo inapangwa kwa ajili ya kwenda kufanya ufuatiliaji ifanye kazi ikiwa ni pamoja

na kujua changamoto ambazo wanapitia hivi vikundi ambavyo vinashindwa kurejesha ili waweze kuwasaidia kwa sababu lengo ni kuwafanya hawa wananchi waweze kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni nyongeza ya mishahara. Watumishi wetu ndani ya miaka mitano hawajapata nyongeza yoyote ya mishahara. Ndugu zangu hata sisi humu ni watumishi wa Serikali lakini ndani ya miaka mitano kweli hata kanyongeza kidogo! Jamani maisha sasa hivi yamekuwa magumu na vitu vimepanda bei. Nyongeza ya mshahara inamfanya huyu mtumishi apate *morale* ya kufanya kazi lakini kama hawa watu wanunung'unika wanakwenda kutafuta vyanzo vingine mpaka walimu wanakuwa bodaboda, hebu mwaka huu tuwaongeze za mshahara. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rehema Migilla. Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami kupata nafasi ya kuchangia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza kabisa, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuaminiwa na kupewa dhamana hii kubwa pamoja na Naibu Mawaziri wa Wizara hiyo, watendaji bila kusahau Kamati ya Bunge iliyohusika na Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado imeendelea kuwa na vipaumbele vyake katika kuwashudumia Watanzania. Moja ya kipaumbele cha Serikali katika kuwashudumia Watanzania ni kuhakikisha Watanzania wote ikiwezekana wanapata matibabu kwa kutumia mifuko ya bima ya afya hasa wale ambao wako katika sekta ambazo siyo rasmi, kwa maana ya wakulima, wafugaji, wavuvi,

wafanyabiashara, wajasiriamali wadogo wadogo, bodaboda, mama ntilie na kadhalika, watu hawa ndiyo wako wengi kwenye jamii yetu, makundi haya ni zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ikaja na wazo zuri sana katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuanzisha huu Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii ulioboreshwa. Mfuko huu umekuja kwa nia njema sana, una muundo mzuri, una watendaji na wasimamizi kuanzia ngazi ya mkoa mpaka ngazi ya kijiji na mtaa. Nia ya mfuko huu ilikuwa kuhakikisha wanachama wote hawa wanapatiwa huduma za msingi za jamii kwa maana ya kupata ushauri wa daktari, kupima vipimo maabara, kupata dawa zile za msingi kwenye ngazi husika kama ni zahanati, kituo cha afya, hospitali ya wilaya na mkoa tunaita *essential drugs* katika kituo husika, pia huduma ya mama na mtoto. Pia kutokana na kituo cha huduma ya afya kwa mfano kwenye zahanati atapata mapumziko, kwenye kituo cha afya atalazwa na upasuaji mdogo, kwenye hospitali ya wilaya atapata upasuaji mkubwa na mdogo pia ila kwenye hospitali ya mkoa atapata vyote pamoja na huduma zote za rufaa ambazo zimethibitishwa katika huduma za mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto katika kupita kwetu, watanisaidia Waheshimiwa Wabunge; kwenye kampeni zetu kule vijijini akitokea mtu kuchangia suala la afya, kama hajachangia changamoto za mfuko huu; na akichangia changamoto za mfuko huu anapokewa na wanachama wote au Wajumbe wote kwenye Mkutano husika, kuona jinsi ambavyo changamoto ni kubwa. Wanasema, Mheshimiwa uliyesimama hapo tunakuheshimu, kama wanakuheshimu watakwambia hivyo. Mimi nakwenda hospitali nakosa hata *Paracetamol*japo ya kunishusha homa nikajipange kutafuta fedha kununua hiyo dawa ambayo haipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, changamoto ni kwamba wale wale wanachama wetu wa mfuko huu ndio wamekuwa wahamasishaji wakubwa wa kuwatangazia

wenzao wasijiunge na mfuko huu, lakini siyo kosa lao ni kwa sababu ya upungufu uliopo kwenye huduma zinazopatikana kwenye mfuko huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine, unapokwenda kwenye kituo cha afya, unajaziwa *Form C2*, inaitwa kwenda kutafuta dawa kwenye *pharmacynyingine*, pale imekosekana. Kuna tatizo; ukiangalia ile *form* yao, ile dawa inaweza ikawa labda ni ya shilingi 5,000, lakini ukienda kwenye *pharmacynyingine* ambayo zimesajiliwa anakujazia *form*, lakini ile dawa anaandika shilingi 15,000.

Kwa hiyo, mfuko utaendelea kupwaya kwa sababu utawanufaidisha watu wengine. Kwa hiyo, iundwe mamlaka ya kudhibiti na kusimamia suala la madawa kwenye mfuko huu, tunapigwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine, uhamasishaji wa wananchi kujejunga na mfuko huu, sasa uendane na upatikanaji wa huduma ambazo nimezitaja, kwa sababu hatuwezi kupata nguvu sisi wanasiasa na vyombo husika kwenye ngazi husika kuwashauri watu wajijunge, wakati tukisema kiukweli, hizi huduma hazipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunajua Serikali inaendelea kuchangia sawa sawa na wanachama wanaochangia pamoja na wadau, wanaita tele kwa tele. Kwa hiyo, ina maana fedha ipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niieleze Serikali, katika muundo uliowekwa ambao ni mzuri tu, kutoka ngazi ya mkoa mpaka Kijiji, wajijekee malengo angalu ya miezi miezi mitatu mitatu tu, halafu wajifanyie tathmini. Hii itaongeza uwajibikaji na *commitment*. Kwa hiyo, huu mfuko badala ya kuwa wa hasara na watu kuvunjika moyo, utawasaidia kama ilivyokuwa lengo la kwanza la Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri hivyo, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jumanne Sagini, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, ajlandae.

MHE. JUMANNE A. SAGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, dada yangu Ummy na wadogo zangu Manaibu Waziri, nawafahamu ni wachapakazi kweli kweli, tuna imani na ninyi, mtafanya mambo makubwa. Imempendekeza Rais aweke Waziri na Manaibu wawili; ameweeka Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wawili. Nadhani nia ni kuhakikisha kwamba TAMISEMI inachemka kweli kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nawashukuru kabla sijaanza kuchangia moja kwa moja kwa namna mlivyo wasikivu na wasaidizi; miezi miwili iliyopita shule zangu mbili kule Butiama ziliungua moto; Shule ya *Chief Ihunyo* na Shule ya Bumangi Sekondari zote za *A' level*, kwa kweli wepesi wenu wa kutatua tatizo lile umewatia moyo sana wananchi wa Butiama, walimu na wanafunzi wa shule zile. Endeleeni kufanya hivyo kwa Watanzania wengine. Mbali tu na kutimiza wajibu wenu, pia mnapata baraka za Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uksoma hotuba hii ya TAMISEMI, jukumu lao la kwanza walilolitaja ukurasa wa tisa inaendelea mpaka ukurasa wa 10, ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuwaji wa Madaraka *D by D* kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa. Sera hii *D by D* wakati mwingine inazungumzwa, pengine nifafanue kidogo. Bahati nzuri ni-*declare interest* kwamba nimekaa kwenye sekta hiyo kwa miaka kadhaa, *D by D* inayotajwa inaweza ikatafsiriwa kama *Decentralization by Delegation, Decentralization by Deconcentration and Decentralization by Devolution*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuliamua kuchukua mwelekeo wa *Decentralization by Devolution* ambapo unapeleka madaraka kikamilifu kwenye ngazi za chini kwa maana ya watumishi, fedha, ujenzi wa uwezo, lakini na

kurekebisha mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Hizo nyingine tulizijaribu Tanzania kwa nyakati tofauti na hazikufanya vizuri sana, ndiyo maana Serikali ikaamua kwenda kwenye *D* by *devolution. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye usimamizi wa rasilimali watu, inatakiwa tupeleke wa kutosha na wenyewe weledi. Ukiangalia Halmshauri zetu, karibu kila Mbunge aliyezungumza ameongea kuhusu changamoto ya upungufu wa watumishi. Ukienda kwangu Butiama, nilishaiieleza pale TAMISEMI; Idara ya Mipango, Idara ya Utumishi, Maendeleo ya Jamii, Ujenzi, Usafi wa Mazingira, vitengo vya ukaguzi wa ndani, TEHAMA, Ugavi, Uchaguzi, Sheria na Nyuki vyote vina makaimu; na bahati mbaya wengine wanaokaimu hawana hata sifa za kuja kudhibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali iko hivyo kwenye upande wa Utumishi. watumishi wanatakiwa wawe wanne, yuko mmoja; Katibu Muhtasi wanatakiwa sita, yuko mmoja Halmashauri nzima; Idara ya Fedha wanatakiwa 11, wapo sita na kadhalika. Unaweza ukatoa mifano mingi, ukishuka kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ukaenda ngazi ya chini. Sasa kama kweli tunataka *Local Government* ziweze kutoa huduma stahiki kwa wananchi, ukishakuwa na upungufu wa rasilimali watu wa kiasi hiki, itaathiri tu. Ndiyo maana sikushangaa Butiama kupata hati yenye shaka, kwa sababu ina watumishi wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi, 2018 TAMISEMI na Serikali kwa ujumla ilikubali walimu wapandishwe madaraja. Kwa sababu ya kuwa na Afisa Utumishi mmoja tu na mdogo, hana hata uzoefu, hakuna kilichofanyika. Walipandishwa watumishi 50, watumishi zaidi ya 348 walibaki bila kupandishwa madaraja. Hii yote ni udhaifu unaotokana na upungufu mkubwa wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la fedha. Ukiangalia duniani kote, *property tax* ni jukumu la msingi la *local authorities*, yaani wanakusanya mapato yale na wanatumia huko huko. Sisi hapa tumebadilisha *equation*,

mapato ambayo ni ya msingi duniani kote ya *local authorities* yamepelekwa Serikali kuu halafu TAMISEMI na *Local Government* wanaanza tena kuomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia Idara ya Bajeti inajadili labda *one third* irudi, wakishakusanya irejeshwe. *But what is justification?* Hawa ndio wanaohudumia hiyo mitaa, ndio wanasaafisha mazingira yale, lakini fedha zile za *property* zinakwenda juu halafu kurudi kwake ndiyo kama hivyo mnavyosema kwambahazienei. Hatueleweki kwa wananchi. Nadhani ifike hatua tusaidie TAMISEMI ipate fedha stahiki iweze kutimiza majukumu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia bajeti ya Serikali, *vis-à-vis* bajeti ya TAMISEMI. Bajeti Kuu ya Serikali ni shilingi trilioni 36.258 na bajeti ya TAMISEMI ni shilingi trilioni 7.683. Maana yake shilingi trilioni 28.575 inabaki Serikali Kuu wakati TAMISEMI inahangaika na mikoa 26, *Local Government* 185. Hivi katika mazingira haya TAMISEMI inawezaje ikatoa huduma fanisi kwa wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninajua tuna deni la Taifa ambalo ni shilingi trilioni 10.663 ukizitoa pale, bado Serikali Kuu inabaki na shilingi trilioni 17.912. Hawa ni Wizara ambaao ni *occasionally* kugusa wananchi ni kwa nadra, labda miradi mikubwa ya Kitaifa. Wanaohangaika na mazingira ya wananchi, usalama wao, barabara zao, maji yao ni *local authorities*, lakini bajeti walionayo inahuzunisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, athari zake ni nini? Ndiyo hapo tunajadili TARURA kupata kupata fedha kidogo, barabara hawezi kuzitengeneza. Ukrejea kwa mfano kule Butiama, ukienda Kata ya Buswahili, barabara ya Kiagata - Wegero - Kongoto, ukienda Bwiregi - Masuhura - Lyamisanga mpaka Kirumi kuititia Mang'ora, ukienda Kukirango - Kyabakari - Kamgegi mpaka Mugango, ukienda Butiama - Muriaza - Kibubwa - Mwikoko - Masurura ni maeneo yasiyopitika kabisa. Sasa watawezaje hao TARURA kufanya kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati inaanzishwa hii Taasisi ya *Road Board*, kilometra za barabara zilikuwa 58,000, leo wana zaidi ya 100,000 lakini *equation* ya *location* ya *resource* ya *Road Board Fund ni thirt by seventy, justification* iko wapi? Tutamlaumu TARURA, tutamgawana, lakini kwa uwezo alionao hawezi akarekebisha hizi barabara zetu, labda kutokee miujiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kuna maboma mengi ya madarasa, zahanati, ofisi kutokamilishwa, ni kwa sababu ya *under financing*. Ukienda *head quarter* za *local authorities*, kwa mfano Butiama, Makao Makuu hayajakamilika, *certificate wanaleta*, inachukua muda kuleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu. Nyumba za viongozi angalau ya *DC* imekamilika pale Butiama, lakini hana ofisi, Halmashauri jengo halijakamilika na viongozi hawana hata nyumba na ni wilaya mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya posho za Madiwani ni *rampant everywhere*, posho zenyewe ni kidogo. Tungekuwa tunajenga hoja kwenye posho za Madiwani, Wenyeviti vya Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji zifikiriwe kuwekwa. Kwa kiwango hiki, ni shida kabisa! Ushauri wangu kwenye hili, Serikali iangalie vigezo vya kugawa *financial resources* kwa ngazi zake zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni yale mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Naomba kushauri, TAMISEMI ikubali kujenga uwezo wa Wizara nyingine wajue dhana ya *D by Dili* waweze kuwa-*support* kwenye utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, ajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa siku hii ya leo kuweza kuchangia bajeti yetu ya TAMISEMI. Naomba nimshukuru sana Mungu ambaye ametupa uzima na uhai hatimaye tuko leo hapa tukiendelea kutetea wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy kwa kazi kubwa, tunamjua, tunamfahamu alifanya kazi kubwa akiwa Wizara ya Afya, ni mwanamke ambaye ni shujaa, ni Hodari; tunajua kabisa kutokana na jitihada zake, hii wizara ataiweza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu suala la *TARURA*. Kwangu kuna maeneo, kata nyingine sasa hivi wako kisiwani kabisa. Madaraja yote yamechukuliwa na maji, barabara zote zimehama, maana sijui niseme nini? Sina hata la kusema, maana tunaonekana kama vile hatufanyi kazi kabisa. Hii ni kutokana na uwezo wa *TARURA*. Maana yake hata *TARURA* wa wilaya na wa mkoa wanashindwa hata kujitokeza kwa sababu hawana fedha ya kwenda kurekebisha mambo mbalimbali ambayo yanatokea katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa sababu Wabunge wengi wamezungumzia *TARURA* tunaomba kwa unyenyekevu mkubwa sana, Serikali iongeze fedha kwa *TARURA* kwa sababu maendeleo yote yanatokea ndani ya vijiji vyetu. Vijiji vyetu sasa hivi wamelima, lakini maeneo ya kupitishia mazao yao hakuna, siyo barabara wala madaraja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nikikwambia, madaraja sijui mangapi huko yamekatika, wananchi Kata hii na hii hawaonani, kijiji hiki na hiki hawawasiliani, ni shida. Naomba kwa unyenyekevu mkubwa sana, *TARURA* iongezewe fedha ili waweze kutekeleza hii miradi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara miaka miwili sasa hazijatengenezwa. Sasa mvua ya mwaka juzi, 2019, mvua ya mwaka jana, 2020 na inayoendelea, basi mambo

yamezidi kuharibika zaidi. Serikali tunajua ni sikuvi, lakini kwa TARURA safari hii tunaomba muipe kipaumbele cha kwanza. Kipaumbele cha kwanza ni TARURA ili njia zetu ziweze kupitika. Kata yangu ya Itenka ambayo ni kata ya uchumi sasa hivi wako kisiwani. Ninaomba sana tusaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie kwenye upande wa Watendaji. Tuna vijiji na kuna maendeleo mbalimbali ambayo tunapeleka ndani ya vijiji vyetu, lakini hatuna watendaji. Utamkuta Mtendaji Kata ndani ya vijiji sita au saba ana Watendaji wa Vijiji wawili au watatu. Unakuta vijiji vine au vitano hakuna watendaji, wanachukuliwa walimu ndio wanakuwa mbadala wa watendaji. Wabunge wengi wamesema kuhusu watendaji, tunaomba mtuongezee Watendaji wa Vijiji, hatuna kabisa katika maeneo yetu ambapo ndiko kunapelekwa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta wakati mwengine Mwenyekiti wa Kijiji hana msaidizi, inabidi aombe msaada kwa mwalimu akaenaye kwa ajili ya miradi mbalimbali ambayo inayofanyika katika eneo la kijiji husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile utamkuta huyo Mwenyekiti wa Kijiji hana posho, hana mshahara, wanapewa fedha nyingi za miradi, lakini yeye mwenyewe; Mwenyekiti wa Kijiji au Kitongoji hana mshahara. Nilikuwa naiomba sana Serikali, kwa sababu miradi mingi inakwenda vijijini na hao Wenyeviti wa Vijiji ndio utakuta wakati mwengine yeye mwenyewe ndio Mwenyekiti wa Kijiji, yeye ndio mtendaji, hana posho wala kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, tuwaangalie Wenyeviti wa Vijiji ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi wapatiwe posho. Wengi wamezungumza kwamba wengine wanachukua rushwa kwa sababu hawana posho. Tukiwatazama kwa umakini zaidi na tukawapelekea posho, wanaweza kufanya kazi kwa umakini Zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niungane na Wabunge wenzangu kuhusu Madiwani. Madiwani

wanafanya kazi nzuri sana na utamkuta Diwani ana vijiji 16 au vijiji 10, lakini umbali wa kutoka kijiji kwenda kijiji posho yake ni ndogo. Tunaomba Madiwani waongezewe posho ili ufanisi uweze kuwa mzuri, waweze kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Halmashauri zetu magari hakuna. Miradi mingi inaenda katika Halmashauri zetu, lakini kutokana na uhaba wa magari kwa ajili ya kuzungukia kukagua miradi, Mkurugenzi pamoja na watendaji hawana usafiri. Tunaiomba Wizara iangalie upya kuwapa Halmashauri zetu vitendea kazi kwa ajili ya kukagua miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri mnaona sasa hivi fedha nyingi tunapeleka kwa kutumia *force account*. Sasa *force account*, tunapeleka fedha huko, lakini kama mtendaji mkuu hana usafiri kwenda kuangalia kwa umakini ujenzi wa shule na madarasa itakuwa ni shida. Fedha nyingi zinapotea na miradi mingi inajengwa chini ya kiwango. Naomba sana magari kwenye Halmashauri zetu yapelekwe ili ufanisi wa kazi uweze kuwa mzuri na miradi mbalimbali ifanyike kwa ufanisi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameongea kuhusu uboreshaji wa bima. Mfuko wa Afya wa Jamii ni shida. Kwenye zahanati zetu, vituo vyta afya hakuna vifaa tiba, hakuna dawa, mgonjwa akienda pale anaambiwa kipimo hakuna, hakuna dawa, sasa ni shida. Jamani tunaomba tujitahidi kwa hili. Kwa sababu tunaenda kuwaambia watoe shilingi 30,000; tulianzia shilingi 10,000 tukawaambia mtoe shilingi 30,000 kwa sababu bima hii imeboreshwa; utatoka ndani ya zahanati, utaenda kwenye kituo cha afya, utaenda wilayani, utaenda mkoani, lakini matokeo yake anakwenda kote kule, hapewi huduma ambayo inastahiki. Naiomba Serikali iangalie upya uboreshaji wa hii Bima upya kwa sababu nayo inaleta shida kwa ajili ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo langu la Nsimbo, naomba niishukuru Serikali imenijengea Hospitali ya Wilaya ingawa hajakamilika. Ila kuna kata ziko mbali kama

Kata ya Ugala. Kutoka Kata ya Ugala mpaka ufile kwenye Makao Makuu ya Wilaya au kwenye Makao Makuu ya Kituo cha Afya, wanatembea kilometra 80. Mtu anatoka kwenye zahanati kwenda kwenye kituo cha afya, anatembea porini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kata ya Ugala nijengewe kituo cha afya kwa sababu watu wanatembea umbali mrefu, watu wanakuwa. Acha Kata ya Ugala, kuna Kata nyiningine ya Stalike. Kutoka Stalike mpaka uikute Hospitali ya Makao Makuu ya Wilaya ni kilometra 50. Naiomba Serikali iangalie haya maeneo yenyne mazingira magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Itenka kama sasa hivi wako kisiwani, wana zahanati ndogo ambayo haina huduma nzuri. Naomba Kata ya Itenka nayo ijengewe kituo cha afya ili sasa kuweza kupunguza yale matatizo. Hata kama watu wako kisiwani, basi wawe na huduma bora, safi na salama katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Aleksia Kamguna na Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pili kwa sababu leo nimesimama naomba nitoe pole zangu kwa Watanzania wote kwa kumpoteza Rais wetu mpandwa, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpe pongezi mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kushika kijiti cha kiliongoza Taifa letu la Tanzania. Sisi kama Watanzania, kama wanawake kwa ujumla tuko naye bega kwa bega kumuunga mkono Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo niwape pole wananchi wangu wa Mchinga, hasa wale wa Kata ya Milola ambao wamekumbwa na kadhia ya tembo na mtu mmoja amefariki kwa kukanyagwa na tembo usiku wa jana kuamkia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze kwa kuzungumzia suala la *TARURA*. Karibu Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu waliosimama hapa walikuwa wanazungumzia suala la *TARURA*, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri wetu na watendaji wake wameeleza vizuri sana na wao wameshika hiki kijiti vizuri sana na wao wameshika hiki kijiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Mheshimiwa wetu wa Awamu ya Sita kumuona dada yetu, mama yetu, mwanetu wetu, kwamba hapa anayefaa si mwingine bali ni Ummy Mwalimu. Naamini na najua Ummy ni mchapakazi mzuri, ni hodari na ni mfuatiliaji, ukimwomba jambo hakuna anapokuachia. Ninachopenda kusema tu *TARURA* inabidi iongezewe pesa. *TARURA* ndio kila kitu, asilimia kubwa ya wananchi wanaishi huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lazima tutengeneze aidha azimio kama tulivyotengeneza wakati ule kwenye eneo la maji ili tumtue mama ndoo kichwani. Tukachukua pesa kutoka eneo fulani tukasema hizi zingizwe kwenye eneo hili ili wananchi tuwatue ndoo kichwani. Kwa hiyo ushauri wangu ili tufanikiwe kwenye hili, tunabidi tuweke hilo azimio kwamba tunataka *TARURA* iongezewe pesa kwa uchache hata iwe asilimia arobaini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye Jimbo langu la Mchinga; Ukitunguka jimbo zima hakuna hata kipande cha sentimita moja chenye barabara ya lami. Sasa kwa misingi hii sio rahisi, halafu Jimbo lile yaani ukitoka kata moja kuelekea kata nyingine lazima upitie jimbo lingine ndipo uweze kufika. Sasa ushauri wangu na ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri, tuunganishiwe zile barabara zetu na *TARURA*, lakini kama *TARURA* hawajaongezewa pesa sio rahisi,

siku zote zitakuwa ni barabara ambazo hazipitiki na haziunganishi hilo Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kutoka Nangalu kwenda Milola huwezi kufika kutoka Mipingo kwenda Namapwiha huwezi kufika kutoka Moka kwenda Mtumbukile ni tatizo. Naona yanakufurahisha, hayo ndio majina ya Mchinga. Kwa hiyo kule kuna changamoto kubwa zisizomithirika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nataka nizungumze mradi wa *EP4R*. Tunaishukuru sana Serikali waliweza kutupatia hizo pesa na hata 2017/2018 walitupatia hizo pesa na walijenga mabweni mawili pamoja na vyoo, lakini mabweni yale hayajakamilika. Kuna bweni la wasichana na bweni la wavulana kwenye Shule ya Kitomanga hayajakamilika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi kama Mheshimiwa Waziri anavyojua matatizo ndani ya Mkoa wetu wa Lindi na Jimbo letu la Mchinga, wanafunzi wanasoma pale wanatoka maeneo zaidi ya kilomita 10. Hivi juzi wanafunzi wameambiwa wabaki nyumbani kwa sababu walihamia kwenye majengo ambayo yaliachwa na Wachina wakati wanajenga. Kikubwa zaidi hata Mwalimu Mkuu wa Shule ile anakaa kwenye nyumba hizo hizo ambazo zimeachwa na hao Wachina.

Mheshimwa Naibu Spika, sasa wakaguzi walipokuja wakasema nyinyi hamjajisajili kama bweni, kwa hiyo rudini nyumbani. Sasa naomba hilo nalo walitazame kwa jicho la huruma ili watoto wale waje wasome pale kwa muda, hatimaye wakitumalizia hayo mabweni, tutafanya jitihada nyingine na zilizokuwa bora zaidi sio kwamba walikaa pale kwa kupenda bali ni kwa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nataka nizungumzie suala la vyombo mbalimbali ambavyo Mwalimu anaitika; vyombo hivi ni vingi kuna TAMISEMI, Wizara ya Elimu,

TSC - Tume ya Utumishi wa Walimu na sasa kuna chombo kingine kinachokuja kinaitwa Bodi ya Kitaalam ya Mwalimu. Sasa hivi vyombo ni vingi, Walimu wenzangu wameniagiza kwa sababu mimi kwa taaluma ni Mwalimu, wanachohitaji hapa wabaki na chombo hiki kimoja wabaki ambacho ni *TSC* na sio Bodi ya Kitaalam ya Mwalimu. Wanahitaji hivyo kwa sababu *TSC* inahudumiwa na Serikali, lakini hiki chombo kikishaundwa na Serikali anatakiwa Mwalimu huyu mwenyewe akiendeshe na ni ngumu sana ukizingatia hata hali yenye we ya Mwalimu nayo ni mtihani kwake. Tunaomba waliangalie hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nataka nizungumzie Walimu kutopandishwa madaraja kwa wakati na kutorekebishiwa mishahara yao kwa wakati. Naomba hili jambo waliangalie kwa utete wake ili Walimu wapandishwe madaraja yao kwa wakati na warekebeshiwe. Kwa mfano, kuna Walimu wa 2014/2015, hawa hawa hawajapanda kabisa madaraja na hata wale wa mwisho kupanda madaraja 2014 imekuwa mwisho. Naomba Serikali waliangalie hilo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kwa unyenyekevu wake mkubwa utupe jibu sahihi kuhusu *TSC* na atupe jibu sahihi kuhusu hiyo Bodi kwani hawaitaki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nikushukuru sana kwa kunipa fursa, nitasubiri Wizara nyingine ili niweze kuchangia hoja zangu Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aleksia Kamguna, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro na Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa heshima na taadhima, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sisi sote kutuwezesha kuwa salama. Pia nawashukuru Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kuwasilisha bajeti yao ambayo ni nzuri, inaleta mwelekeo pamoja na changamoto zake, lakini inaleta matumaini katika Taifa letu. Tunasema ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli kwetu tuna matatizo, Mkoa wa Morogoro ni mkoa wenyе bahati, tumepata miundombinu ya kimkakati, lakini kuna matatizo mengi katika mkoa huu. Naomba kwa heshima na taadhima nizungumzie huo mkoa. Mkoa wa Morogoro ni mkubwa sana na wote wanakiri ni mkoa wa pili katika nchi yetu, lakini tumepata neema, tuna ardhi nzuri, kadhalika na kadhalika, lakini pamoja na hiyo ardhi nzuri imeguka sasa imekuwa shubiri inatutesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Nichukue mfano wa Wilaya ya Malinyi; wilaya hii iko bondeni, yaani mvua ikinyesha Iringa sisi kwetu ni maji. Ninavyoongea leo hii, siwezi nikatoka hapa Dodoma kwenda kwetu sina kwa kupita, kwa maana wilaya nzima imejaa maji. Kwa kuwa imejaa maji hatuna miundombinu ya barabara, hali ni mbaya, yaani Malinyi waiangalie kwa jicho la huruma, wengine wote wanalilia lami lakini sisi tunalilia kufika kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Malinyi ni wilaya mpya, ni wilaya ambayo imetokana na Wilaya mama ya Ulanga imeanzishwa mwaka 2015, lakini kama nilivyotangulia kusema barabara hatuna, yaani TARURA kama inawezekana, wote wanasema asilimia 40, basi kwetu sisi iwe asilimia 60 kwa ili iweze kuisimamisha Malinyi. Malinyi hatuna madaraja na hatuna hata barabara ya changarawe. Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, angekuwa amefika Malinyi angenielewa ni nini nazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuna njia ya kuingia Malinyi; tukifika sehemu moja ambayo inaitwa Misegesi kwenda Malinyi huwezi kufika, kuna hitaji daraja na halipo. Kuna sehemu nyngine ya Malinyi kuelekeea Lugala ambako ndiko kuna Hospitali ya Misheni ambayo tunaitegemea, huwezi kufika kwa sababu barabara hakuna. Pia kuna sehemu nyngine ambayo inaitwa Malinyi Lugala ndio huko kwenye Hospitali karibu, lakini huwezi kufika. Sasa huyo mtu wa Malinyi anaishije. Naomba Mheshimiwa Waziri avae viatu vya watu wa Malinyi, kwa kweli Malinyi tuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wanasema kwamba wanahitaji *TARURA* kwa ajili ya barabara na sisi watu wa Malinyi tunasema *TARURA* ni uhai, kwa maana bila ya *TARURA* sisi hatuwezi kuishi na kweli maisha yetu ni magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Malinyi tuna matatizo kwa upande wa afya. Hatuna barabara, hatuna *dispensary*, hatuna Hospitali ya Wilaya, Hospitali ya Wilaya imejengwa, kuna kipindi walitoa mwongozo kwamba, lazima hospitali zote waanze kutibia wagonjwa wa *OPD*, ndio hicho kimeanzishwa, lakini kwa ujumla hospitali ya Serikali hakuna. Sasa kama hospitali ya Serikali hakuna, miundombinu ya barabara hakuna, huyu mwanamke ambaye amepewa kazi na Mungu ya uzazi, anawezaje kutoka kwake afike kwenye hospitali na kama atafika kwenye hospitali, kwanza hospitali yenyewe halpo, anaenda wapi? Tunaomba pia Mheshimiwa Waziri kwa upande wa afya atuangalie, hatuna barabara, hatuna hospitali, kama mama inaumiza. Naomba watuangalie Malinyi. Leo sina mengi ya kusema zaidi ya kuomba yaani nimesimama kwa ajili ya kuomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine ya Wilaya ya Ifakara kuna hospitali moja inatiwa Man'gula B. Hapa limejengwa jengo zuri kabisa la Kituo cha Afya katika Mkoa wa Morogoro, lakini hakuna sehemu ya *operation*. Ni kituo cha afya kikubwa na kizuri na Serikali imetumia pesa nyingi. Sasa tunaweka kile kituo bila sehemu ya wazazi na wazazi wanafariki, tunaomba nalo liangaliwe, bado Morogoro ina changamoto. Morogoro ni kubwa na lazima TAMISEMI waiangalie kwa jicho la pekee wakilinganisha na mikoa mingine, kwa sababu kama ni kubwa ina maana na mahitaji yake yatakuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande mwingine wa utawala; hili naomba niwaeleze, sasa hivi naona kuna mikoa mingi au Wilaya nyingi kuna matatizo au ina changamoto, unakuta Mkuu wa Wilaya anagombana na Mkurugenzi, anagombana na Mbunge, sasa kunakuwa tafrani, nafikiri viongozi wenzangu watakubaliana nami

kwamba katika wilaya nyingi au halmashauri nyingi hazina amani, kuna vurugu. Kwa nini kuna vurugu? Yawezekana kwa mawazo yangu uteuzi tunaoufanya sasa hivi wa Wakuu wa Wilaya labda turudi nyuma, mwanzo tulikuwa tunawachukua hawa Maafisa Tarafa, wanakuwa na uzoefu, wanakuwa karibu na Wakuu wa Wilaya, ukimteua kuwa Mkuu wa Wilaya anajua zile *ethics* za uongozi, lakini hawa wa sasa hivi kama wanawatoa tu shulenii, wanawapeleka wanakuwa Wakuu wa Wilaya, matokeo yake kunakuwa *conflict of interest*, matokeo yake wilaya zinakuwa na vurugu. Hilo nimeliona, naomba tuliangalie kwa umakini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Niwakumbushe tena Waheshimimiwa tunapochangia humu ndani na mimi nakumbushwa hapa mbele, usizungumze Serikali inakusikiliza usiwe na wasiwasi, zungumza na Kiti, Serikali inapata ujumbe. Kwa sababu ukimwambia moja kwa moja asipokuwa kwenye kitu chake unaanza Waziri umetoka, anaweza akapigisha simu na Rais, sasa si lazima atoke, maana Rais naye ni sehemu ya Bunge. Kwa hiyo tuwe tunatilia maanani hilo jambo.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Condester Sichalwe ajiandae.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara napenda kuanza kuwashukuru viongozi wa TAMISEMI kwa kuweza kuidhinisha mafungu mbalimbali ya fedha ambayo tayari yameshafika kwenye Jimbo langu la Ngara. Mathalani naomba niwashukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Dugange na Dkt. Riziki Shemdoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miezi michache iliyopita, Jimbo langu la Ngara limepokea mafungu mbalimbali ya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu

ya aina mbalimbali kwenye vituo vya afya, shule za sekondari, na kwenye shule za misingi. Nawashukuru sana kwa kuweza kutapatia fedha sisi wananchi wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwa watumishi. Watumishi hasa Walimu pamoja na wale wa kada ya afya wana changamoto nyingi sana mtambuka ambazo wamekuwa wakiishi nazo kwa muda mrefu. Kuna malipo *call allowance* wanayotakiwa kulipwa watumishi wa kada ya afya, kwenye Jimbo langu la Ngara, kuna watumishi wana miaka nane mpaka kumi na zaidi hawajalipwa hii fedha inayoitwa *call allowance*, wanaishi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Walimu, kama ambavyo wenzangu wamechangia, kwenye Jimbo langu la Ngara, Walimu wana changamoto nyingi sana, Walimu wanadai kupandishwa madaraja, wanadai malimbikizo ya uhamisho pamoja na *allowances* za matibabu, hawajalipwa kwa muda mrefu. Kama kuna watu wako hoi, basi ni hawa watumishi na uhoi wenyewe unatofautiana. Kuna mtu yuko hoi anaumwa anameza *Panadol*, mwagine ni hoi yuko *ICU*na mwagine yuko kabisa kwenye vitu vingine. Hawa wako hoi, naombeni sana TAMISEMI wa-*coordinate* na watu wa utumishi ili Ngara tupate kibali cha kupandisha vyeo. Toka mwaka 2008 hatujapata kibali ambacho tumeshakiomba mpaka sasa. Kwa hiyo hawajapandishwa madaraja toka mwaka 2008, 2009, 2020 na sasa ni 2021. Napenda kuionomba TAMISEMI wa-*coordinate* na watu wa utumishi ili tuweze kupata vibali angalau kwa kuanzia kibali cha mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa Bodi ya Walimu kama kuna kitu kinaenda kutuvuruga Tanzania ni hii inaitwa Bodi ya Walimu. Walimu wana makato ya aina mbalimbali mpaka sasa kwenye mishahara yao. Sasa tupo hapa kuna kitu kinaendelea huko TAMISEMI, wanatengeneza Bodi ya Walimu na inakuja na sheria inayotaka walimu wawe wanakatwa fedha kila mwezi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna jambo walimu hawataki kusikia ni hili hapa la kuja na sheria inayotaka walimu wakatwe fedha na kila mwezi hela yao iondolewe. Kwanza mishahara yenyewe ni midogo, halafu tunataka tena kuwakata hela. Hilo jambo litaleta vurugu, halikubaliki walimu kwenye jimbo langu wamesema hawataki kusikia kitu kingine kipyä kitakachokuwa na madhara ya kukata fedha zao kwenye mishahara yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu, hasa ya shule za sekondari na msingi; Jimbo langu la Ngara lina changamoto kubwa hasa katika upande wa matundu ya vyoo. Mathalani, shule za sekondari zina upungufu wa matundu 132, ukiangalia hapa maana yake wanafunzi 2,640 hawana mahali pakujisaidia. Ninaomba sana TAMISEMI watakapokuja wana-*consolidate* mlchang'o yetu basi Ngara watuungezee matundu ya vyoo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa nyumba za walimu, tuna upungufu wa nyumba za walimu 344. Maana yake ni kwamba walimu wenye familia ya watu watano, zaidi ya watu 1,720 wanaishi katika mazingira yasiyoeleweka eleweka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa upungufu wa walimu, tuna upungufu wa walimu 197; maana yake ni kwamba inapotokea fursa ya kuajiri walimu wapya kwa upande wa Jimbo la Ngara, wachukue walimu wawaambie waingie kwenye vyumba vyaa madarasa. Vyumba vyaa madarasa viwili vikijaa wafunge mlango halafu hao wote watuletee kwenye Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu 197 ni sawasawa na madarasa mawili yaliyojaa wlaimu. Ninaomba sana, ninawaomba TAMISEMI itakapotokea fursa ya kuajiri walimu wapya basi Ngara watuletee idadi ya walimu wanaolingana na madarasa mawili yaliyojaa watu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya sera ya afya inasema kila kijiji kiwe na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya. Nina upungufu wa vituo vya afya 17, nina upungufu wa zahanati 29; maana yake ni kwamba upungufu wa zahanati 29 unasababisha watu 72,000 wakose mahali pakwenda kupata huduma za afya. Ninaomba sana TAMISEMI watakapokuja ku-*consolidate* angalau Ngara waniongezee vituo vitatu vipyta vya afya. Hizo ni zahanati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vituo vya afya, ninaomba sana kwasababu tuna upungufu wa vituo vya afya 17 ambapo watu 340,000 hawana mahali pauhakika pakwenda kupata huduma za afya kutokana na ukosefu wa vituo vya afya. Ninaomba angalau TAMISEMI watuongezee vituo vya afya angalau vitatu katika mwaka huu wa fedha ili kuweza kuondokana na changamoto za eneo hili la miundombinu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TARURA*; kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwenye michango ya nyuma, *TARURA* inahitaji ongezeko la bajeti, hili halina mjadala. Kwa upande wa Jimbo langu la Ngara, *TARURA* wamekuwa wakipewa ukomo wa bajeti unaolingana kwa miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba kwa Jimbo langu la Ngara tuna madaraja, tuna makalavati 652 na fedha tunayopewa ni ya kutengeneza kalavati 15 kwa mwaka; maana yake ni kwamba tunahitaji miaka 43 kuweza kujenga makalavati ya Jimbo la Ngara, *a good 43 years!* Ina maana kwamba hili jambo halikubaliki, ninawaomba sana waweze kutu-*consider*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja; ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa kunipa nafasi, niishukuru Wizara kupidia kwa Waziri kwa kazi nzuri sana ambayo imefanyika ndani ya kipindi cha miaka mitano. Tumeshuhudia ongezeko la vituo vya afya, shule nydingi zimejengwa na fedha zilikuwa zikienda, na mimi jimboni kwangu nilipata hizo sehemu ya huduma za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi kwenye eneo ambalo Wabunge wengi wamezungumzia, suala la *TARURA*. *TARURA* kwa bajeti ambayo ipo haitakuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote kile, na Waziri nikuhakikishie dada yangu, kama utakuwa na bajeti uliyonayo ni ngumu sana kutekeleza miradi ya maendeleo. Tuna kilometa zaidi ya 100,000 za barabara za mijini na vijijini. Pamoja na ongezeko uliloleta la shilingi bilioni 124 kwenye bajeti hiyo, haiwezi kufanya kitu chochote kile kwani mahitaji ni makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, sasa ninawaomba tutoke na maazimio ya kuishauri Serikali na maamuzi magumu ambayo tukiyafaya tutapata suluhisho la kudumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia kwenye Bunge hili, Bunge hilo ndilo lilitotoa maamuzi tukapata fedha za kujenga barabara Mfuko wa *TANROADS*, zilipatikana kupidia Bunge. Mfuko wa *REA*, Wabunge hapahapa ndio tulioipitisha tukapata fedha za kuendeleza miradi ya umeme vijijini. Bado tumekuwa na mawazo ya kujenga uwezo juu ya Mfuko wa Maji. Ni sisi hawahawa Wabunge ambao ndio tunahitaji kutoa mawazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo ambayo yataisaidia Serikali kutoka mahali tulipo. Naomba Waheshimiwa Wabunge turidhie, tutenge shilingi 100 – haya ni mawazo ambayo atawea kuangalia sasa Waziri wapi watakwenda – tuna maeneo matatu ya mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la kwanza alilitoa Mheshimiwa Zungu; shilingi 50 tuitenge kwa ajili ya sekta ya mawasiliano, kila mtu anapopiga simu kwa siku tuwe tunachangia shilingi 50, na tuweke wazi kwamba shilingi 50 tunatenga kwa ajili ya kujenga barabara za mijini na vijijini. Itatusababisha kupata shilingi bilioni 540.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaona shilingi 50 haitoshi, tukitenga shilingi 100 kwa siku, kila mtumiaji wa simu akitumia shilingi 100, tutapata shilingi trillioni moja na bilioni 80 ambayo ni fedha zitakazoweza kwenda kujenga miundombinu ya barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda mbali zaidi kama tunaweza tukatenga shilingi 200, kila siku mtumiaji wa simu akawa anatenga shilingi 200 Watanzania tukawaambia ukweli, na sisi Wabunge twende tukawaeleze ukweli wananchi wananchi kwamba shilingi 200 tunaitenga kwa ajili ya kuhudumia barabara za mijini na vijijini; tutapata trillioni mbili na bilioni 160. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitano tutakuwa na miundombinu bora sana kwenye nchi yetu. Na zile fedha ambazo zimetengwa kwa sasa tulizonazo zitasaidia kwenda kuimarisha miundombinu ya zahanati, vituo vyaya afya na hospitali, mtajenga na majengo mengine kwa hii bajeti uliyonayo. Kwasababu tutakuwa tumepata chanzo kikubwa ambacho kitatoa fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinivinevyo tutakuwa tunasema maneno ambayo yatajirudia. Kila mtu atakuja atasemea juu ya TARURA, TARURA haina fedha ya kutosha. Naomba hili Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja, tuwe na maamuzi ambayo yatatusaidia kupata mahali pa kutoka kupata fedha za kutosha za kuhudumia maeneo ya huduma za simu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie fedha za Mfuko wa Jimbo; kumekuwa na uwiano usiokuwa sawa kwenye

majimbo mbalimbali ambayo yanatofautiana. Bado Mfuko wa Jimbo ni uleule, tena ambao haujapitia tathmini ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnakuta mtu ambaye ana kata tatu, tano au sita mnapewa sawa na wale ambao wana kata zaidi ya kumi mpaka ishirini, naomba hili mkalifanyie kazi, mfanyie *review* ya majimbo yote, muangalie ukubwa wa majimbo ili tuweze kupata uhalisia mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninapenda kuiomba Serikali; zipo halmashauri kama ya kwanga ambayo mimi nimetoka, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, ndiyo iliyozaa halmashauri zote ambazo zipo Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kila halmashauri illyokuwa inazaliwa walikuwa wanatoa magari kwenye halmashauri mama, matokeo yake halmashauri mama ilikosa vyombo vyya usafiri. Tumetoa kupeleka manispaa, tumepeleka Mlele, Mpimbwe na Nsimbo, matokeo yake hii halmashauri haina vyombo. Ninaomba kupitia kwa Waziri, aiangalie halmashauri hii aipatie vyombo vyya usafiri ili viweze kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tunayo majengo yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, ni karibu sehemu zote. Naamini kama mapendekezo tuliyotoa yakifanyiwa kazi zile fedha zitakazobaki hapo tuzipeleke ziende zikaimarishe kujenga majengo ambayo wananchi wamejitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni karibu nchi nzima kila sehemu wanajitolea, wanajenga kwa nguvu zao, bahati mbaya yale majengo yanachukua muda mrefu na wakati fulani yanaanguka kuwavunja nguvu wananchi. Tunaomba sehemu ambako wamejenga majengo ya zahanati, vituo vyaa afya, shule za msingi na sekondari, Serikali muwaunge mkono mpeleke fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ni kauli ya kwenu ninyi Serikali ambayo mnaitoa kwamba asilimia 20 ikifanywa na

wananchi na asilimia 80 Serikali itakuja kuwa-support sasa matokeo yake wananchi wako fasta kuliko Serikali inavyopeleka huduma hiyo ya msingi. Naomba hili mlifanyile kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba muangalie sana posho za wenyeviti wa Serikali za vijiji, posho za Waheshimiwa Madiwani, ambao wanafanya kazi kubwa sana. Kila jambo linalotekelawa na Serikali linashuka huku chini. Wanaofanya hiyo kazi ya hamasa ni hawa wenyeviti wa Serikali, wenyeviti wa vitongoji na Madiwani ndio wasimamizi wakubwa. Kwa hiyo tunaomba eneo hili mliangalie ili waweze kufanya kazi kwa tija na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mheshimiwa Boniphace Butondo ajiandae.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru na kipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa mambo ambayo waliweza kutufanya katika Jimbo la Mombasa katika Awamu ya Tano, na mambo ambayo wanaendelea kutufanya katika Awamu hii ya Sita; tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kwamba tuna imani sana na wewe kwenye Wizara husika ambayo umepewa kuisimamia, lakini pia kuendelea kuwapongeza kaka zangu, Manaibu hodari sana ambao wanamsaidia dada yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba niwasilishe baadhi ya changamoto za wananchi wa Jimbo la Mombasa kama ifuatavyo. Nitaongelea kwenye miundombinu ya barabara pamoja na madaraja;

miundombinu ya elimu; miundombinu ya vituo vya afya pamoja na zahanati na muda ukiwa Rafiki nitamalizia na namna gani kuendelea kuwawezesha akinamama wa vijiji ni katika ubunifu wao mbalimbali walionao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Momba ndilo jimbo ambalo tuseme kwa Mkao wetu wa Songwe linaongoza kwa kiasi kikubwa sana kulima mpunga, maharage pamoja na mahindi. Na tunaweza kusema ndilo jimbo ambalo linalisha Mkao mzima wa Songwe kwa mbegu, au tuseme kwa zao la mchele. Lakini pamoja na nchi ambazo ni Jirani kama Kongo na Zambia, wanategemea sana mchele pamoja na maharage kutoka kwetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, kutokana na mambo ambayo Waheshimiwa wenzangu ambao wametangulia kueleza hapa. Ufinyu mkubwa uliopo kwenye bajeti ya *TARURA* ni wazi kwamba hata nitakapoeleza changamoto nyingi ambazo zinalipata Jimbo la Momba sitaweza kumaliza. Kiukweli Jimbo la Momba ni miongoni mwa majimbo ambayo yana changamoto kubwa sana ya miundombinu ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sasa ambavyo ninaongea hapa ni kweli ziko kata ambazo ziko pia visiwani, zimebaki kwasababu hakuna madaraja, barabara siyo rafiki, hawawezi wakatoka kwenda kijiji kingine, hawaweze wakatoka kwenda kata nyingine, wanaendelea kusubiri mpaka mvua zitakapokauka ndipo waendelee kupitia kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Hali hiyo imeendelea kusababisha kudorora sana kwa mapato ya halmashauri yetu, pamoja na kwamba jimbo linaendelea kuhudumia na nchi nyingine ambazo zipo mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali; kwa kuwa *network* ya barabara ambazo ziko ndani ya Jimbo la Momba ni barabara 57 zenye urefu wa kilometra 647.21, ninajua kwa ufinyu wa *TARURA* barabara hizi haziwezi kutekelezeka. Niende kwenye uhalisia; tunaomba tuombe barabara chache za kimkakati ambazo kuwepo kwa

barabara hizi Serikali itakapotuwezesha, kunaweza kukachangia kwamba halmashauri ikaongeza mapato yake, lakini pia ikavutia maana zitakuwa ni barabara za kimkakati. Lakini pia inaweza ikafanya hata wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika maeneo hayo, yakawavutia kuendelea kubaki hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kwanza ambayo nianze kuiombea ni barabara ya Makamba – Ikana. Na barabara hii sababu ya kuiombea barabara hii ni kwamba ndiyo barabara ambayo inaunganisha Jimbo la Mombasa kwa ukanda wa juu na wa chini na soko la kimataifa la mifugo na mazao limejengwa katika Tarafa ya Ndalambo ambalo tunalitegemea sana katika kupandisha mapato ya halmashauri na kuliongezea Taifa mapato yake kwa kuwa tutaendelea kusambaza kwa wingi na kwa ubora kwenye nchi zetu ambazo ziko Jirani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tutakapokuwa tumeipata barabara hii, itakuwa imerahisisha Tarafa za Msangano na Kamsamba ambazo zina jumla ya kata nane, kwa hiyo watapandisha mazao yao kwa urahisi kwa ajili ya kwenda kufika kwenye soko la mifugo na mazao ambalo lipo Kakozi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ninayoiomba ni barabara ya Chindi – Msangano ambapo kuwepo hapo kuna daraja kubwa ambalo limetenganisha Halmashauri ya Wilaya ya Mombasa pamoja na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Kwa hiyo kama barabara hii itafunguka, na tutakapopata daraja katika eneo hilo, itatusaidia sana wananchi kuendelea kuwa na *options* mbalimbali kwa ajili ya kupeleka mazao mengine au na shughuli nyingine za kiuchumi kwenye Mji wa Tunduma ambao tunautegemea kama mji ambao uko mjini kwa ajili ya kuendelea kupata mahitaji mbalimbali, ikiwa na hospitali ya wilaya iko kwenye Mji wa Tunduma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ninayoiombea ni barabara ya Ivuna – Chole. Barabara hii

inaunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Momba pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Songwe. Na wananchi ambao wapo katika Kata ya Mkomba wanatenganishwa na daraja kubwa. Mwenyewe kipindi cha mvua nikienda kufanya ziara ni lazima nibebwe mgongoni kwasababu baiskeli haiwezi kupita, pikipiki haiwezi kupita, gari haliwezi kupita. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara nyingine ambayo naomba ushughuliki ni barabara ya Kakozi - llonga. Barabara hii ndiyo ambayo inaunganisha Mkoa wa Songwe pamoja na Mkoa wa Rukwa. Barabara hii pia Mheshimiwa baba yangu Mheshimiwa Kandege naye ninajua itamsaidia sana kuja kutumia lile soko la mifugo na mazao kwa sababu ataleta mazao yake pale. Vilevile barabara hiyo ndiyo ambayo inapita mpaka kufika kwenye Bandari ya Kalemii.

Kwa hiyo, itasaidia wananchi wa Jimbo la Momba na Majimbo mengine ambayo yapo kwenye Mkoa wa Songwe na kwenye Halmashauri zingine wanaweza wakaitumia kwa ajili ya kufikisha mazao yao au vitu vyovyote kwenye bandari hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri kidogo kwa Serikali namna gani inaweza ikatusaidia kuongeza pato kidogo kwa TARURA. Nitolee mfano wa wananchi wangu wa Jimbo la Momba. Wananchi wa Jimbo la Momba kwa asilimia ni wachache sana ambao wana simu za *smartphone*, kwa hiyo, mtu anaponunua kifurushi anapewa dakika za maongezi, *SMS* za ku-chat pamoja na *MB* lakini kwa sababu ni watu wa kupiga tu hata ku-chat kwa *SMS* za kawaida hawa-chat, inapofikia kile kifurushi kina-expire anakuwa ametumia dakika lakini *MB* pamoja na *SMS* zinakuwa zimebaki lakini mtu yule anakuwa ameshalipia na kodi ya Serikali amekatwa kwenye ule muda wa maongezi. Mnaonaje kama TAMISEMI wataamua kwamba kile ambacho kinakuwa kimebaki kwa sababu ni cha mwananchi na alikilipia kwa pesa yake halali akatolea na kodi kwa nini isirudi ili ije kwa ajili ya kusaidia vitu kama hivi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa Waheshimiwa Wabunge tuna *experience* kitu hiki, umenunua dakika, *SMS* na *MB* unatumia kidogo vinabaki vinaenda wapi? Kwa hiyo, tunayaafaidisha makampuni ya simu ambayo yameshatuchaji na tunawaachia bure, hivi *wiki-expire* tuwekeane mwongozo vinarudi kwa Serikali kwa sababu itakuwa ni changizo halali la mwananchi huyu. Kwa hiyo, mimi naona inaweza kutusaidia kukusanya na kuboresha barabara na katika hilo dada yangu Mheshimiwa Ummy mtukumbuke huko Mombasa, ahsante sana. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwenye miundombinu ya elimu, kutokana na Jimbo la Mombasa kuwa na changamoto nyingi za barabara imepelekea mazingira ya walimu wengi ambao wanafanya kazi ndani ya Jimbo la Mombasa yanakuwa si Rafiki. Walimu hawa kuna wakati wanakuwa wanbung'unka, hawana motisha ya kufanya kazi vizuri. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pilii imeshagonga. Tunaendelea na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mungu ambaye ametupa afya na uzima. Pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Hai, naomba niishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo wanatujali, sasa hivi tunaona raha ya kuchagua Chama cha Mapinduzi. Raha hiyo tunaiona kwa sababu tayari tumekwisha kutengewa fedha kwa ajili ya mradi wa maji pale Kikafu, naishukuru sana Serikali.

Pia tumefanyiwa ukarabati wa shule zetu mbili; Lyamungo na Machame *Girls*. Vilevile tumeonja angalau lami japo kwa mita chache lakini ndiyo zimeingia kwa sababu tulichagua Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa sana hili ambalo tumelipata tumetengewa shilingi bilioni 1.6 kwa sababu ya kufufua Kiwanda cha *Machine Tools*. Hii ndiyo raha ya kuchagua Chama cha Mapinduzi, nawashukuru sana. Si hivyo tu, kwenye Wizara hii ambayo naenda kuchangia muda si mrefu tumepelekewa shilingi milioni 280 kwa ajili ya ukarabati wa Shule za Narumu, mabaara lakini na ujenzi wa nyumba za walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa njielekeze kwenye kuchangia hoja iliyopo mezani. Nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu nina imani kabisa na Mheshimiwa Waziri dada yangu Ummy pamoja na wasaidizi wake wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi si mahiri sana wa kusifia lakini ninazo sababu za kumsifia Mheshimiwa Waziri huyu kwa kazi nzuri anayoifanya. Majuzi wakati wa Pasaka nilitembelea Kituo cha Afya pale Kisiki, aliona kwenye taarifa ya habari ye ye mwenyewe akanitafuta na akaniambia kituo hiki tunaenda kikitengeneza kiwe cha kisasa ndiyo maana namsifia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa Naibu Waziri Silinde majuzi tukiwa humu Bungeni alitoka akaenda kufanya ziara kule Hai. Ndiyo maana nasema hakika tuna timu nzuri ambayo inatusaidia hapo TAMISEMI. Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo naye leo asubuhi ameniambia tukimaliza Bunge hili tunaenda naye Hai. Kwa hiyo, ninayo sababu ya kupongeza timu hii nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu, pamoja na mazuri hayo machache ambayo tumefanyiwa kwa kipindi cha miaka 15 tuliyakosa sasa tumeyaanza kuyapata, naomba niseme kwenye elimu bado tunashida. Shule zetu za msingi pale Jimbo la Hai zimejengwa kuanzia mwaka 1950 na kurudi nyuma na sasa hivi zimechakaa sana, tuna shule 106 ni chakavu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pasaka nilitembelea Shule ya Mafeto ukienda pale Mheshimiwa Waziri ni aibu na wewe nilikutumia *clip* ile uone shule ile imechakaa kabisa si rafiki. Shule zote hizi 106 zimechakaa kweli kweli. Niombe Serikali ielekeze nguvu hapo ili pamoja na nguvu za wananchi na mimi mwenyewe tunazozitumia kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii lakini Serikali itusaidie kupeleka fedha pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni pamoja na shule za sekondari. Tunayo Shule yetu ya Lemila pale na yenyewe imechakaa. Shule hii kimkakati kwa sababu inazungukwa na Kata nne tunaomba sana Serikali itutazame tuwe na shule ya kidato cha tano na kidato cha sita kwa sababu shule ile mazingira ni rafiki lakini tunalo eneo la kutosha; tuna hekta ishirini kwa ajili ya ujenzi wa kidato cha sita pale. Naomba pia nikumbushe pamoja na shule hizo nilizozitaja tuna Shule ya Uduru imechakaa san ana Shule ya Mkwasangile imechakaa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna eneo lingine ambalo niombe Serikali ilitazame sana. Pale Jimbo la Hai tulikuwa na shule tano, hizi shule tano zinaitwa shule za msingi za ufundi. Shule hizi zilikuwa zimejengwa mahsus kwa ajili ya kuandaa vijana wetu kupata ufundi wa aina mbalimbali. Shule ya pale Mshara inaitwa Shule ya Msingi ya Ufundu Mshara, mle ndani kuna vifaa kwa ajili ya kufundisha watoto wetu kushona cherehani, kufuma lakini pia mafundi seremala. Ile shule imesimama, vifaa viro mle ndani, watoto walianza kusoma lakini tangu mwaka 2019 walisitishiwa kufanya mitihani, hili linahusisha Wizara ya Elimu lakini pia TAMISEMI. Shule ya Mshara, Mkwasangira, Sare, Mroma lakini pia tuna shule moja ilijengwa kwa kusudio hilo na mradi wa TASAF na yenyewe imelala naomba ziangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi zitatusaidia kuwaibua vijana wetu kwenye eneo la ufundi lakini wakati huo huo Wizara ya Elimu *ijiandae* kufungua shule hizo ili watoto hawa waweze kufanya mitihani ya ufundi lakini pia waweze kupewa vyeti. Hii itaendana sambamba na fedha nydingi ambazo Serikali imepeleka kufufua Kiwanda cha *Machine*

Tools, tutapata watoto wa kwenda kufanya kazi kwenye kiwanda hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nililotaka kuchangia, nafahamu tumetengewa fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya pale Lundugai. Niombe sana Wilaya ya Hai tunayo changamoto kubwa, tuna mahitaji ya vituo vya afya 12. Bahati nzuri tumeshatenga maeneo, haya maeneo naihakikishia Serikali yapo, hayana mgogoro na sisi tupo tayari kuchangia pale ambapo itakuwa tayari na wao kutuletea fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa niombe sana pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ameshanikubalia hiki Kituo cha Kisiki hatuna gari la wagonjwa, watumishi hawatoshi lakini pia hatuna jengo la mama na mtoto. Hii ni sambamba na Hospitali yetu ya Wilaya na yenyewe gari la wagonjwa hakuna, hakuna Jengo la Maabara wala Jengo la Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo kuhusu *TARURA*, wenzangu wamesema sana lakini kwa Jimbo la Hai kwa kweli mtutazame kwa jicho la huruma. Pale tuna mtandao wa kilometra 600 na mita 200 lakini bajeti ambayo tumewekewa makadirio ni shilingi bilioni 1.7 haiwezi kutusaidia. Wenzangu wameshashauri namna ya kufanya, niombe kwa mahsus i wake mtusaidie. Tuna barabara inayotesa wananchi kutoka pale Kwa Sadala - Uswaa, Kivuko cha Mkalama – Kikavu Chini lakini Boma Ng'ombe - *TPC* na barabara zingine ambazo nimekwisha kuzisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kwa haraka haraka, niombe sana Serikali tuna soko la kimkakati pale Kwa Sadala. Soko hili sipumui, simu yangu inajaa picha kwa sababu ya soko hili. Kila siku wananchi wanapiga picha wananiambia limechakaa halifai lakini tunalo eneo ambalo tumeshatenga kwa ajili ya soko hili. Ikumbukwe Wilaya hii kwa asilimia 78 tunategemea kilimo, wananchi wako tayari kulima soko lile liwe la kimataifa ili tuweze kukaribisha wawekezaji

waje wanunue lakini pamoja na kuwa na viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga Kituo cha Afya Longoi na Naibu Waziri amekitembelea. Sasa tunaomba vifaa tiba na watumishi ili tuweze kufungua kituo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumze jambo ambalo wenzangu wamesema pia. Haya yote tunayoyapanga na hizi bajeti tunazozipitisha wanaoenda kusimamia ni watumishi wa umma. Naomba sana Serikali ione haja ya kuongeza mishahara ya watumishi. Pia watumishi wale ambao wamepandishwa vyeo na wana barua zao mishahara yao irekebishwe. Changamoto kubwa tunayoiona hapa wakati mwingine tunalaamu sana Maafisa Utumishi lakini tujue sisi Wabunge hapa ndiyo tunaopitisha bajeti. Pale Wizarani naomba TAMISEMI mtashirikiana na Utumishi kuona namna ya kuongeza *ma-approverwengi* ili kazi inapofanyika huku kwenye *level* ya Halmashauri watumishi hawa mishahara yao iweze kuruhusiwa mapema na kuondoa kuwa na malimbikizo mengi ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize barabara moja muhimu sana. Tuna barabara ya kutoka pale Mferejini – Narumu - Makoa ni kilometra 13 tu. Hii barabara inatupasua kichwa. Barabara hii ililitwa ya ng'ombe nimekuwa nikiisema sana na ni ahadi ya Rais, niombe sana mnifungue kwa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kwa kuhitimisha, nimeona kwenye hotuba imeleeza kuwa na maeneo ya uwekezaji. Jimbo la Hai tunayo maeneo ya uwekezaji lakini changamoto yapo kwenye Vyama vya Ushirika 17. Jambo hili nimekuwa nikisema sana na hapa nasema mapema kabisa kwa Wizara ya Kilimo tutakapofika kwenye Wizara ya Kilimo ile shilingi nitaitazama mno namna ya kuifanya. Juzi hapa tumekuwa na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Waziri wa Utalii na Maliasili tumetembelea kule amejionea mwenyewe namna ambavyo kuna mikataba ya hovyo kwenye ushirika.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele imegonga Mheshimiwa.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, pia niwakumbushe tena kuzingatia Kanuni zetu, mambo yale yatakayokuja baadaye unayaacha kwa ajili ya baadaye kwa sababu Kanuni zetu zinaita kitendo kama hicho kuwashisha shughuli. Kwa hiyo, unatakiwa kuchangia hoja iliyopo Mezani. (*Makofi*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Boniphace Butondo atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ajiandae.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ameendelea kutujalia afya. Pia naomba niendelee kukushukuru wewe sana kwa sababu nimepata nafasi ya kuchangia jioni hii katika bajeti hii muhimu ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu hasa nitajielekeza katika eneo la *TARURA* pamoja na elimu na kidogo nitagusia upande wa afya. Kwanza, naungana mkono kabisa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba ipo haja ya kuitizama *TARURA* kwa macho mawili na hasa katika eneo zima hili la kuongeza hii *percentage* ya kiasi ambacho *TARURA* wamekuwa wakipewa fedha kwa ajili ya kushughulikia barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo kubwa lenye mtandao mkubwa unaohitaji kutengenezwa ama kulipa kipaumbele ni eneo la barabara zilizopo vijijini. Eneo la

Kishapu tuna jumla ya kilometra 1,030 ambazo zinahitaji kutengenezwa lakini zikiwa katika mazingira magumu kweli kweli. Yapo maeneo mengine yapo katika mbuga hasa lakini vile ni vijiji na kuna maeneo ya kiutawala ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa vyovyyote vile huduma ya barabara ni ya msingi sana kwa sababu bila huduma ya barabara huduma hizi zingine; kwa mfano huduma ya afya wananchi hawawezi wakayafikia maeneo kwa ajili ya kwenda kupata huduma iwe katika *health centre* au *dispensaries* lakini hata katika sekta ya elimu kuna wakati watoto wanashindwa kufika maeneo ya shule kutohana na matatizo ya maji na hasa panapokuwepo na matatizo ya vivuko kadhaa kuharibika Zaidi, kwa hiyo, lipo tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia usafirishaji wa mazao kila mmoja hapa anafahamu Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa ambao unalima sana pamba. Tunapozungumza zao la pamba ni Wilaya ya Kishapu ndiyo inayoongoza kwa kulima pamba. Tafsiri yake Wilaya ya Kishapu ni moja kati ya wilaya na inawezekana ikawa ya kwanza ama ya pili nchini kwa uzalishaji wa pamba. Sifa ya zao la pamba katika kuchangia uchumi wa nchi hii unaweza ukawaona hawa wana Kishapu ndiyo wanaongoza kwa adha ya barabara, hapa hakuna haki kabisa.

Nataka niishauri sana Serikali na hasa Wizara yetu ione umuhimu wa Wilaya ya Kishapu kuhakikisha kwamba barababara zinatengenezwa na inaongezewa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niyataje baadhi ya maeneo ambayo yana hali mbaya kabisa, zikianza tu kunyesha mvua safari za kuelekea Kata za Itilima, Kiloleli, Mwaweja na Mwamalasa inakuwa ni shida, hizi ni kata ambazo hazipitiki kabisa. Hili ni tatizo ambalo kwa kweli tusipoliangalia tunaweza tukawakatisha tamaa sana wananchi. Zipo Kata za Uchunga, Mwataga na Somagegi, hizi ni kata ambazo na zenyewe zinakuwa kisiwani pale mvua zinapoanza kunyesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Serikali kulitazama eneo hili na kuona haja ya kupeleka fedha za kutosha. Wenzangu wameshauri sana katika masuala ya simu, hili jambo tunaweza tukaliangalia na Serikali ifike mahala iwe *serious*, tuwahurumie wananchi. Bunge limekuwa likitoa mawazo hata katika eneo la mafuta, kwa nini tusifike mahali tukajifunga mkanda lakini lengo tuwafungulie njia wananchi? Nasema hivi kwa sababu Watanzania kwa ujumla wanahangaika na masuala ya barabara. Kwa hiyo, mimi naamini kwa sababu Serikali ya CCM ni sikiu kupitia mMwaziri wetu na hususani Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na wasaidizi wake ndugu yangu Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Dkt. Dugange mfanye hili jambo ili mradi tuwapunguzie adha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata habari kwamba kuna kama shilingi bilioni 100 zimeongezeka kidogo na wengine wameshaanza kupata taarifa, zimeshaanza kutumwatumwa kule, mimi naomba Kishapu tuikumbuke. Tuikumbuke Kishapu kwa jicho la huruma kwa sababu wananchi hawa wanateseka sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nizungumzie ahadi za viongozi wetu wakuu. Kipindi cha Uchaguzi aliyekuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alifika Kishapu na bahati nzuri aliweza kuahidi kilometra nne. Ahadi hii alikuja kusisitiza kwa sababu alishaiahidi awamu ile ya kwanza, maana yake miaka mitano barabara hiyo ilikuwa hajatekelezwa lakini imeanza kutekelezwa kwa mwaka fedha uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kilometra nne tumepata jumla ya shilingi milioni kama 114, shilingi milioni karibu 380 zilikuwa hazijafika. Naomba sana fedha hizi ziweze kufika na kusaidia wananchi hawa ili mradi Mji wa Kishapu na wenyewe uweze kufanana. Kwa sasa hivi kazi iliyopo kwenye ile kilometra moja kuna asilimia kama 94, lakini nachoomba Wizara iweke msukumo na kuhakikisha fedha zile zinafika Kishapu na kuhakikisha kwamba mradi huo tunaukamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu wa walimu 1,611 katika shule za msingi, hapa kuna tatizo kubwa sana. Kwenye nyumba za walimu na penyewe pana shida kubwa. Kuna tatizo kubwa sana upande wa madarasa, wananchi wamejitahidi sana kutoa nguvu zao kuhakikisha kwamba wanasukuma mbele na kutoa mchango upande wa madarasa. Hata hivyo, kuna haja Serikali kuweka mpango maalum kuhakikisha kwamba ina-support nguvu za wananchi, yako magofu mengi ambayo yanahitaji support na hii ni katika shule za msingi na sekondari. Naomba sana Wizara hii iweze kutazama maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna Kata mpya za Shagihilu, Mwaweja, Bupigi, Mwasubi, Mwadui, Luhumbo na Mwamala tumeshaanzisha sekondari mpya na bahati nzuri Serikali imekuja na mpango wa kuhakikisha inapeleka fedha kwa ajili ya sekondari hizi. Naomba sana Wilaya ya Kishapu ipewe kipaumbele na wananchi hawa tusiwakatishe tamaa tuhakikishe tunawapelekea fedha kwa ajili ya kuhakikisha maeneo haya yanafanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni upande wa Waheshimiwa Madiwani na nataka nizungumzie maslahi yao. Nimekuwa Diwani kwa zaidi ya miaka 20 na nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri kwa zaidi miaka 10. Nataka nizungumze Madiwani wana shida kubwa sana na kusema ukweli hawa Madiwani ndiyo wanaosimamia shughuli za maendeleo, ndiyo wanahamasisha shughuli za maendeleo. Hawa Madiwani ndiyo wanaotoka jasho kwa ajili yetu sisi Wabunge ili mradi tupate ushindi pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna kila sababu Mheshimiwa Ummy, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Dkt. Dugange oneni huruma kwa hawa viongozi wenzetu waongezeeni posho, laki tatu na siyo hela. Jamani tuangalieni majukumu waliyonayo na wananchi wanaowahudumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine hawa watu posho zao za vikao ni matatizo makubwa sana, ipo shida kubwa. Pengine na mimi nilikuwa naungana mkono tuhamishe posho hizi za madaraka ziwe zinalipwa na Serikali

Kuu tubaki na hizi posho za vikao kwa sababu mzigo kwa baadhi ya Halmashauri unakuwa ni mkubwa na Halmashauri zinashindwa kulipa. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

T A A R I F A

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika zangu zilindwe.

NAIBU SPIKA: Haya wakati naangalia nani mtoa taarifa naambiwa kengele ya pili imeshagonga.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Butondo, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nilikuwa nimetaja Mheshiwa Tunza Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde na Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sisi sote kukutana kwenye ukumbi huu tukiwa salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kuzungumzia *issue* ya elimu kwa sababu ni mwalimu na nina *interest* kubwa sana kwenye elimu. Tumekuwa tukizungumza suala la miundombinu ya elimu kwa maana kuanzia Shule ya Msingi mpaka Kitando cha Sita kwa TAMISEMI. Pia tumekuwa

tukizungumzia uhaba wa nyumba za walimu, hilo linajukana hivyo Serikali tunawaomba mwendelee kulifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Mtwara. Changamoto kubwa ninayoiona kwenye Mkoa wetu ni kwamba kuna baadhi ya maeneo upungufu wa walimu hali yake inatisha. Inatisha kwa maana ipi? Unakuta shule moja ina walimu wawili au watatu. Ukimwuliza Afisa Elimu, anasema, sisi tunagawa walimu kulingana na idadi ya wanafunzi; mwalimu mmoja wanafunzi 45, sawa. Kwa mfano, shule ina wanafunzi 90, maana yake unapeleka walimu wawili. Sasa wakati unapeleka walimu wawili ujue wale watoto kuanzia Chekechekeea au kuanzia Awali mpaka Darasa la Saba wanasona masomo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hao walimu wawili, maana yake pale una Mkuu wa Shule, una Makamu wa Mkuu wa Shule, hapo anatakiwa atokee Mtaaluma, atokee mtu wa nidhamu, atokee mtu wa mazingira, apatikane Mwalimu wa Zamu; hawa walimu wawili, pata picha wanajigawaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, hao hao walimu wawili, Mkuu wa Shule kila siku anaitwa kwenye vikao. Maana yake na huyu mmoja akiumwa au akipata tatizo, shule inafungwa, watoto wanakaa nyumbani. Kwa hiyo, wakati tunapiga kelele sana kwamba mtaala ubadilishwe, sijui kitu gani kibadilishwe, tuangalie pia, hao tunaowapa kazi ya kufundisha watoto wetu wako katika mazingira gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta Darasa la Saba lina masomo saba lakini una walimu wawili. Mimi ni mwalimu, ndiyo maana nimeanza kusema hivyo. Kuna kitu tunaita *content mastery*, yaani mimi leo kwa sababu nimesoma *Physics*, *Chemistry* na *Biology*, huwezi kuniambia nitakuwa mzuri kwenye *Chemistry*, nitakuwa mzuri kwenye *Biology* na nitakuwa mzuri kwenye *Physics*, never! Kwa hiyo, ni saw ana wale walimu wawili waliopo kwenye shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo shule ambazo nitakuletea Mheshimiwa Waziri, siongei kutoka hewani. Wale walimu wawili waliokuwa kwenye zile shule, unamtaka huyo mwalimu afundishe *history*, afundishe *geography*, afundishe hesabu na kadhalika, mtu mmoja haiwezekani. Ndiyo hapo tunapoanza kuwaharibu Watoto. Wakija huku juu tunataka wawe *competence based. Competence* hiyo wameipata wapi ikiwa kule chini alikotoka hali ilikuwa hiyo bora liende!

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu suala la kufundisha niwaambie ndugu zangu, haliishi darasani, ama halianzii darasani. Kuna kitu kinaitwe *Scheme of Work* unatakiwa uandae kila somo, kuna kitu kinaitwa *Lesson Plan*, unatakiwa uandae kila somo na kila kipindi. Mwalimu kwa siku anaingia madarasa matano au sita, tofauti tofauti aandae hivyo vitu vyote, unategemea atamfundisha mtoto vizuri! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule ziko Halmalshauri ya Wilaya ya Newala. Ninayo orodha hapa, zipo kama tisa, zina walimu wawili au watatu. Nikutajie kwa mfano, halafu ufuatilie na mpeleke walimu. Matokeo yanapotoka, hatutaki kusikia Mtwara imekuwa ya mwisho, tunataka iwe ya kwanza kwa maana watoto wapate walimu, wafundishwe vizuri. Wanazo akili, lakini hawapati mazingira bora ya kuweza kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna shule inaitwa Mpali, ina walimu watatu; kuna shule inaitwa Mpotola, ina walimu watatu; kuna shule inaitwa Chikalule, ina walimu wawili; ziko nyingi, orodha ninayo na nitakuletea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kulisema, walimu wetu hawapati mafunzo kazini. Mwalimu akishamaliza mafunzo yake yaye ya cheti au ya nini, akiingia ndiyo tumemsahau hiyo mazima. Tunaomba walimu wapatiwe mafunzo kazini. Kuna *TRCs* kwenye Vyuo vya Ualimu viliwekwa kwa sababu ya kuwasaidia walimu kutoka kwenye hizi shule kwenda kupatiwa ujuzi, kama mnabadilisha vitabu, mtaala, na kadhalika, tunategemea walimu wale

waendee kule. Hata hivyo, sasa hivi ukienda zimekufa.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetokea Chuo cha Ualimu ndio nikawa Mbunge, naelewa hakuna kinachoendelea kule. Kwa hiyo, hizo *Teachers Resource Centre* ziliwa zinawasaidia sana walimu kwenda kunolewa ili kuongeza ujuzi kwa sababu elimu kila siku inabadilika, kuna mambo mapya, kuna zile *crosscutting issues* ambazo tunategemea mwalimu aweze kuzipata na kuongezewa ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu huyu mwenye *stress* ya kutokupandishwa madaraja, kutokuongezewa mshahara, hana nyumba ya kuishi, anakotoka ni mbali mpaka afike kazini, bado leo unamlundikia vipindi kufundisha kutoka awali mpaka Darasa la Saba, halafu tunakuja humu ndani tunalalamika kwamba watoto wetu sasa hivi hawaelewi, hawafanyi nini, hata wale kule wanachoka. Tuwaangalie kwa jicho la huruma. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hayo, sasa naomba nizungumzie *issue* ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Suala hili naliunga mkono sana kwa sababu najua umuhimu wake, lakini naomba Serikali iangalie, hata ukisoma hotuba ya Kamati imewapa ushauri. Tusiwaze sana kwenye mambo madogo madogo. Leo siyo wakati wa kumpa tu mtaji wa shilingi 50,000, anafanya nini? Ndiyo swali tujiulize. Mnawaambia watu wakae kwenye vikundi 10, wanakaa hapo, wanazunguka usajili mpaka waje wasajiliwe unawapa shilingi 500,000. Tunataka tuwatoe kweli kwenye umasikini? *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu mfuko kwanza uangalie vizuri, uwekewe utaratibu vizuri na watu tuwe na *mind* kubwa ya kuona kwamba tunataka tuwawezeshe watu. Unaweza ukampa mtu shilingi milioni 100 akafanya shughuli, akaajiri watu hata 20, 30, wakawa wanapata kipato kuititia yeye. Tusiangularie sana kwenye *mind* ndogo. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea kidogo kwenye Jimbo la Mtwara Mjini, Manispaa ya Mtwara Mjini. Niliuliza swali juzi, tuna tatizo kubwa Mheshimiwa Waziri mkatuangalie, maji yanajaa sana. Yaani watu wa Mtwara Mjini sasa hivi wakiona wingu limekaa huko juu, wanajiuliza, hii mvua ikishuka hapa itakuwaje? Mkatuchimbie mifereji, barabara nyingine zinajengwa, maana yake zinasababisha yale maeneo yawe chini. Sasa kama yako chini na mifereji haiko ya uhakika, matokeo yake kila siku maji yanaingia ndani ya nyumba za watu. Kata ya Magomeni, Kata ya Chuno, Kata ya Likombe, Shangani, maji yanaingia kweli kweli ambapo zamani maji yalikuwa hayaingii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kabisa, mfanye jitihada za makusudi mwende Manispaa ya Mtwara Mikindani, mkaangalie tatizo lile na mjue mnalitatuaje kwa sababu wananchi wale walipimiwa viwanja, wananchi wale wana maeneo yao ya biashara, lakini kila siku maduka yanaingia maji. Hiyo haileti afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana. Mimi ni mtu wa kwenda muda. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, tutamalizia na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami nianze kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na ninaamini wataendelea kuifanya katika kuimarisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika kuishauri Serikali katika namna bora ya kuendelea kutafuta fedha ya kuifanya *TARURA* iweze kufanya kazi vizuri. Nakubaliana na michango iliyotolewa na Mheshimiwa Mussa Zungu na Mheshimiwa Moshi Kakoso ya namna bora ya kuweza kupata fedha za kuifanya *TARURA* ifanye kazi. Kifungu cha 8(1) cha *Government Notice No. 211* ya mwaka 2017

ilitengeneza utaratibu wa namna ambavyo *TARUTA* watapata fedha (*source of funds*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika jambo ambalo halijasemwa humu lakini naamini linaweza litakaleta tija. Kabla ya *TARURA*, Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya zilikuwa zikitenga bajeti ya barabara kuititia Idara ya Ujenzi. Sioni ni kwa nini zisiendelea kufanya hivyo kwa sababu tunamhudumia Mtanzania mmoja. Kama waliweza kuzitenga hapo awali, kwa nini wasiendelee tena kutenga? Ndiyo maana namwomba Mheshimiwa Waziri waende kulisimamia jambo hili na inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wakati anawaapisha Mawaziri, alisema hili pia. Waende wakafanye *coordination* nzuri ndani, Halmashauri zitenge fedha, vilevile na fedha ya *TARURA* itaendelea kutumika. Lengo hapa ni kuhakikisha mfuko huu unaendelea kuwa na fedha za kutosha. Naamini Mheshimiwa Waziri atakuwa ameshakutana na hii nyaraka, ukienda ofisini, uko waraka ambao aliutoa aliyekuwa Katibu Mkuu, Iyombe ya kuzitaka Halmashauri za Majiji, Manispaa na Wilaya kutenga hizi fedha. Mheshimiwa Waziri naomba isiwe hiyari, iwe lazima fedha hizi zikatengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka niishauri Serikali ni katika eneo la mapato ya malipo ya mbele kwenye ardhi (*premium*). Katika miji yetu yote zoezi la upimaji wa viwanja na urasmishaji linaendelea, lakini ndani ya zoezi hilo wananchi huwa wanalipa fedha ya *premium* ambayo imeelekezwa katika kuboresha huduma za kijamii na hasa miundombinu. Kwa nini fedha hii isitengewe utaratibu mzuri ikaingia *TARURA* kwa ajili ya kuweza kusaidia kwenye majukumu ya *TARURA*? Kwa sababu hivi sasa inabaki katika Halmashauri na kupangiwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa, kwa sababu katika upimaji wa viwanja vipyta inatozwa asilimia 2.5 malipo ya *premium* na katika urasmishaji ni 1%, hizi ni fedha nyingi sana. Tuna uwezo pia wa kutumia chanzo hiki kwa ajili ya

kuifanya *TARURA* iwe na mfuko ambao utafanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri una uwezo wa kukaa na Waziri wa Ardhi mkakubaliana tu, vizuri kabisa namna ya utaratibu huu kwa sababu mwenye mamlaka kwa mujibu wa Kifungu cha 31(1) cha Sheria ya Ardhi ni Waziri wa Ardhi. Mkukubaliane kwa pamoja ukawekwa utaratibu mzuri ili fedha hizi ziingie katika *TARURA* na wafanye kazi ya kutuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilichangie hapa, Dodoma hivi sasa ni katи ya maji jи ambayo yanakuwa kwa kasi sana. Kwa mtandao wa barabara za lami, Dodoma ndiyo inaongoza kuliko jiji lolote Tanzania nzima kwa kuwa na mtandao mrefu wa barabara za lami. Huu tuliupata kupitia mradi wa *TSCP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mwingine ambaao unakuja, baada ya kuona mafanikio ya *TSCP* kuna mradi wa *TACTIC* hatujui umekwamia wapi? Tunaiomba Serikali, wakati Mheshimiwa Waziri unakuja kujibu hoja, atueleza jambo hili kwa sababu lina manufaa makubwa sana. Miradi hii ikitekelezeka, inaboresha miundombinu, inachochea uchumi katika eneo husika, inakuza na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiliona leo soko la Ndugai, ukiona stendi ya ma-*bus* pale ni mradi wa *TSCP*, una mchango mkubwa sana. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri akija atuambie umefikia hatua gani kwa sababu tumesubiri muda mrefu katika jambo hilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi ukikamilika, unakugusa wewe pale kwenye Jiji la Mbeya, unamgusa Naibu Waziri Tanga, unanigusa mimi hapa Jiji la Dodoma, unakwenda Arusha, Mwanza na matokeo yake ni makubwa sana. Pia tuna jambo ambalo linaendelea...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, shukrani. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, nikiwa naenda kufunga dimba kabisa kwa siku ya leo, nikushukuru sana. Nami niungane na wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na timu yake nzima ya TAMISEMI, Katibu Mkuu na wasaidizi wake kwa kuendelea kuaminipa na Serikali ili waweze kuitumikia na kututendea kazi ambayo Serikali inakusudia kuifanya kupitia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapindunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianzie pale ambapo Mheshimiwa Mavunde ameishia. Ukweli ni kwamba majiji yetu na Manispaa, Miji pamoja na Halmashauri ambazo zinakua, zimenufaika sana na mradi wa *TSCP* na sina shaka, kwa rekodi peke yake kutoka mwaka 2010 mpaka mwaka 2020 kwa hii miaka 10 peke yake majiji yapatayo sita, Manispaa karibia nane pamoja na miji zaidi ya 16 imefaidika sana kwa miradi ya *TSCP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda hata Babati, Manispaa ya Illemela, Mwanza, Tanga, Mbeya kule kwako zaidi ya kilometra 438 zimejengwa. Sasa naiomba sana Serikali, Mheshimiwa Waziri atakapokuja, kama Mheshimiwa Anthony Mavunde alivyosema, tuone namna gani mradi wa *TACTIC* ambao tayari wataalam kutoka *World Bank* na wataalam wa ndani, wameshatembelea Halmashauri zetu na kujiridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana yapo mambo machache tu yamekwama huko kwenye Wizara, hebu tuyatazame tuone namna ya kuruhusu mradi huu uanze mara moja tuweze kuona tija ambayo tumeipata kutoka miradi ya *TSCP* na hatimaye tuone mafanikio na turahisishe, tupunguze mzigo kwa *TARURA* ambapo wote humu ndani

tunalalamika kwamba fedha hazitosh. Mradi huu tuna uhakika utahudumia zaidi ya Halmashauri 45 ukilinganisha na Halmashauri 18 na 9, jumla 27 peke yake kwa kipindi kilichokwisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nianze na hilo kwa sababu ni jambo muhimu. Naamini ukienda kule Mbeya, Tanga, Mwanza na hapa Dodoma na maeneo mengine ya Arusha, bado zipo barabara ambazo zinaunganisha miji hii na zitaleta tija sana katika mchango wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Mwanza peke yake tunategemea kuwa na barabara zisizopungua Kilometra 27 hadi 33. Barabara ya kutoka Buhongwa kwenda Igoma, barabara ya kutoka Sauti kwenda Luchelele, barabara ya kutoka Buhongwa kwenda Bulale inayokwenda kuungana na daraja la Masongwe kwenye Halmashauri nyingine ya Misungwi. Haya yote ni mafanikio ambayo yanaweza kuchagizwa sana na barabara hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni juu ya masuala mazima ya ardhi na upimaji. Utakubaliana nami kwamba jukumu la upimaji na Sheria ya Ardhi Na. 8 imezipa mamlaka zetu haki ya kupima, kumilikisha pamoja na kupanga. Sasa nimejaribu kuangalia kwenye kitabu, sioni maeneo ambayo Wizara imekumbuka kupeleka fedha kwenye Halmashauri zetu ili jukumu la kupima, kupanga na kumilikisha liweze kufanyika huko kwenye Halmashauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miji yetu bado ina changamoto kubwa. Kama Wizara inafanya jukumu lake la kupeleka watumishi na kuwalipa mishahara kupitia Wizara ya Ardhi, lakini jukumu la kwetu kama Wizara ya TAMISEMI ni kuhakikisha Halmashauri inaendelea kupima, kupanga na kumilikishwa ili tutoke hapa kwenye maeneo ambapo tupo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la muhimu kwenye Sekta ya Afya, upo mpango ambao ulipokelewa hapa na Wakurugenzi pamoja na watendaji kwenye

Halmashauri. Maelekezo ya namna gani kila Halmashauri kulingana na mapato yake, kwa mfano, Jiji la Mwanza peke yake tumepangiwa kujenga vituo vya Afya vitatu, tujenge madarasa 100. Sasa nadhani hapa bado kuna changamoto tuiangalie vizuri. Mipango iliyopangwa kwenye Halmashauri na kuletwa bajeti kwetu, maana yake ni kwamba haitatekelezeka kama Halmashauri zitapokea maelekezo haya ambayo zinayo leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi leo hatuhitaji madarasa, maana yake tukisema madarasa, tunataka tukaongeze darasa kwenye kila shule. Sisi tunataka shule mpya. Tunazo shule 28; kila shule moja kati ya shule hizi, shule 27 kila shule ina watoto wasiopungua 2,400 sawa na shule nne. Kwa hiyo, tunadhani sisi leo tukiamua tunataka tujenge shule mpya zitakazowasaidia watoto hawa kukaa kwenye mazingira bora, salama na rafiki na yanayoweza kufundishika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naona umewasha kengele hapa, muda wenyewe umebarani, lakini nakushukuru sana. Niseme tu kwamba tunahitaji mipango iliyopangwa na Halmashauri iweze kupokelewa na kuruhusiwa kufanya kazi ili iweze kuleta matunda na faida kwa wananchi kuliko maelekezo haya.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru kwa michango yenu wale ambao mmepata fursa ya kuchangia hapa. Ni dhahiri kwa orodha zinazoletwa hapa mbele na maombi yanayokuja hapa mbele, Wabunge wengi wana hoja nydingi kutoka kwenye majimbo yao wangependa kuzisemea kwenye hii Wizara maalum kabisa inayohusu mambo ya msingi kwenye maeneo yao, lakini kwa sababu muda wetu huwa hautoshi, Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi, msipochangia TAMISEMI ziko Wizara nydingi zinazohusika na mambo mahsusisi yalikoyoko katika majimbo yetu tutayasema. (*Makofi*)

Yule aliyepata fursa sasa ameshataja na barabara zote kule kwake. Itakapokuja Wizara ya Ujenzi atataja mwengine ambaye hakupata fursa wakati huu. Itakapokuja Wizara ya Afya, atasema mwengine ambaye hakupata fursa ya kusema wakati huu. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi kwamba sasa nikikosa hii, nitasema wakati gani? Muda huwa umebana kidogo, lakini tutajitahidi kuweka utaratibu mzuri, Wabunge wale ambao wameshachangia huku mwanzo; na wenzenetu wa vyama mnaoleta orodha hapa, mtusaidie kutazama nani ameshachangia na nani hajazungumza kabisa. Kwa sababu majina tunapoita hapa mbele yaliyotoka huko kwenu, sisi tunafuata zile orodha mlizoleta. Mara chache sana mtu anakuwa ameomba huku moja kwa moja halafu akaitwa. (*Makofi*)

Sasa zile orodha ziangalie kwanza wale ambao hawajapata fursa kabisa ya kuzungumza. Itatusaidia sana kwa sababu kila Mbunge hapa ana kundi, ana jimbo, ana watu anaowawakilisha apate fursa ya kusema. Sasa kwa orodha iliyokuwa imetoka Chama cha Mapinduzi hatujaweza kuimaliza lakini nataka kuamini kwa sababu Katibu wa Wabunge wa CCM yuko hapa, atafahamu ni Wabunge gani hawakupata fursa leo wapate kipaumbele kesho wale ambao waliletwa kwenye orodha, hawakuitwa leo wapate kipaumbele kesho. Halafu ambao hawatafanikiwa hata hiyo kesho kuchangia, basi wasiwe na wasiwasi, Wizara zinazokuja wapewe kipaumbele wale ambao hawajapata fursa ya kuzungumza sasa. (*Makofi*)

Yamechangiwa mambo mengi sana hapa na yote ni ya msingi sana, nami nimefurahi kwamba Mheshimiwa Waziri yupo hapa muda wote na Manaibu Waziri wake wapo hapa, wanaandika kwa bidii sana. Naamini yale mnayoyachangia Waheshimiwa Wabunge, watayafanya kazi. Kwa kweli Wabunge wamezungumza sana kuhusu *TARURA*. Sasa Mawazo yao myachukue na ya wataalam wenu, maana hapa mawazo yanatolewa mengi, lakini ni dhahiri *TARURA* haina fedha za kutosha. Nami mwenye ni shahidi. Unajua ukishakuwa na jumbo mahali, aliwahi kuongea hapa Makamu wa Rais, akasema baada ya kwenda kule kwenye uchaguzi, sasa ameelewa. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Wabunge wakitaja hapa jambo fulani halijafanyika, inakuwa kidogo shida. Hata mimi kwangu kule kuna daraja tangu 2019 na watu watano walifariki, mpaka leo hakuna chochote. Ukiuliza, upembuzi yakinifu, upembuzi sanifu, yaani ni hadithi. 2019 mpaka leo na watu wamekufa ni dhahiri jamani watu huko kuna taabu. Mheshimiwa Naibu Waziri alishafika pale.

Kwa hiyo, najaribu tu kuonesha mfano wa mambo mazito ambayo Waheshimiwa Wabunge wanachangia hapa. Kwa kweli hao watu wangu watano jamani wananiuma mpaka leo, lakini ndiyo mambo kama hayo yanatokea na ninatamani maeneo kama hayo *TARURA* ikiwa ina changamoto, basi waambie *TANROADS*. Kwa sababu mpaka sasa hivi hakuna hayo mawasiliano. Kwa hiyo, mazingira kama hayo yanaleta shida kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana. Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge lilahirisha mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 21 Aprili, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*